# Nipashe

Jumanne Oktoba 22, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580055

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710






UKURASA 13



## Ofisa Takukuru matatani kwa tuhuma za kuua mke kwa risasi

UKURASA 3



# Madai rushwa uchaguzi mitaa waizindua CCM

**YABAINISHA** joto uchaguzi mkuu 2020, yatoa kauli nzito kwa wanaojihusisha, baadhi ya wagombea na wanachama wachapana makonde... *Endelea uk. 2*

Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally

## WAKURUGENZI KIKAANGONI MAKUSANYO YA MAPATO



UKURASA 3






## IPTL yapinga mahakamani madai ya benki Hong Kong

UKURASA 2

MICHEZO YANGA: MBAO DARAJA LA PYRAMIDS KIRUMBA UK. 32 · MAONI, KATUNI UK.6

# Madai ya rushwa yaizindua CCM

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimeibuka na kuweka wazi madai ya kuwapo rushwa katika kura za maoni za uchaguzi wa serikali za mitaa, huku kikiwaonya wanaojihusisha na vitendo hivyo.

Wakati kikitoa onyo hilo, chama hicho ambacho kinatawala nchi kwa sasa kimesema vitendo hivyo na madai ya upendeleo ni dalili za kupanga safu kwa ajili ya uchaguzi mkuu ujao wa Rais, wabunge na madiwani, utakaofanyika mwakani.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, alisema anatoa salamu za Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais John Magufuli, kuwa amefurahishwa na uandikishaji unaoendelea na mwamko wa wananchi.

"Malalamiko tunayoyapokea yanagusa uvunjifu wa kanuni kwa mtazamo wa rushwa au upendeleo au kupanga safu. Upangaji wa safu mwingine nasikia wanadhani wanaweza kupanga kwa ajili ya uchaguzi. Mchezo huo tumeshauzuia na hatutauvumilia," alisema.

Dk. Bashiru alisema Mwenyekiti anawapongeza viongozi wa chama, wanachama na Watanzania kwa mwitikio mkubwa wakati wa uandikishaji na kwamba anaamini mwitikio utaendelea hadi wakati wa kupiga kura.

"Napenda kusisitiza haki itendeke, malalamiko tunayoyapokea yanavunja uvunjifu wa kanuni," alisema.

Katibu mkuu huyo alisema kanuni za kuchuja wagombea hazikuzingatiwa kwenye baadhi ya maeneo na kwamba baadhi ya viongozi walichezea muhtasari kiasi cha kupishana kati ya tawi kata na uamuzi wa wilaya.

"Tunaelekeza maeneo hayo uchaguzi urudiwe, hakuna kuchukua fomu upya, hakuna mchujo bali wote walioomba wapigiwe kura. Kokote ambako uchaguzi utaporudiwa wagombea wote wataruhusiwa. Mfano wilaya za Kawe na Kinondoni wagombea watakuwa wote na si wale waliokwisha kuteuliwa," alisema.

Dk. Bashiru alisema wengi walikuwa wamepoteza imani na kwamba ili kurejesha imani wagombea watakuwa wote walioomba na kwamba maeneo kulikuwa na zogo na fujo, uchaguzi urudiwe bila kuwachuja wagombea.

Katibu Mkuu huyo alisema kulikuwa na rafu za kuchomoa majina kwenye masanduku ya kura na masanduku kubomolewa na wengine wakitumia jina la Katibu Mkuu kuwa amewapa maelekeo ya kufanya wafanyayo.

Alisema nyingine ni wasimamizi kuchelewa na kura za maoni zikaanza kupigwa baada ya saa tisa alasiri, na kwamba wagombea wote walioomba warudishwe kupigiwa kura.

"Marudio yanarekebisha uteuzi, kote uchaguzi urudiwe bila kuwachuja wapiga kura ili tweke imani, ilikuwa tumaliza Oktoba 29 tunaongeza siku mbili hadi Octoba 31, mwaka huu" alisema.

Alisema kwa mfano Mbeya kuna mgombea amempiga kibao mwenzake na kwamba wana CCM wanapaswa kuwa mfano bora na kuwa na uvumilivu hata wanapopishana kwa kutotumia lugha chafu au kuhamaki .

"Tunahimiza kuwa Takukuru inakamata wala rushwa wakati wa uchaguzi na wakati usikio wa uchaguzi ndani ya CCM na nje, chombo hiki tumeunda sisi na moja ya ahadi zetu ni kupambana na rushw ana ufisadi," alisema.

Dk. Bashiru alisema chama kimeweka utaratibu wa kutoa taarifa kwenye chama na tuyo mwenye jukumu hilo, na kwamba anayezungumza atapaswa kutoa idhibni kwa msemaji mkubwa na kwamba hawataruhsiwa kutangaza matokeo kwa kuwa mchakato wa uchaguzi ni wa ndani.

WAGOMA KUPIGA KURA

Wanachana wa CCM Tawi la Kasanga B, Kata ya Mindu, Morogoro Mjini, juzi waligoma kupiga kura za maoni kwa ajili ya kuchagua wanachama watakaogombea katika uchaguzi wa serikali za mitaa baada ya kukosa mwafaka wa kusikilizwa madai yao.

Madai ya wanachama hao ni pamoja na kutaka uongozi wa CCM Wilaya ya Morogoro Mjini kuingilia kati na kurudisha majina ya wagombea wote waliojitokeza katika

INAENDELEA UK 8



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akifungua mkutano wa siku tano wa 58 wa Mwaka wa Shirika la Mashauriano ya Kisheria kwa Nchi za Asia na Afrika (AALCO), katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OMR**

# IPTL yapinga kortini madai ya benki

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Independent Power Tanzania Limited (IPTL), imeomba Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam itamke rasmi kwamba Standard Chartered Bank (Hong Kong) Limited (SCBHK), si wadai wake na ibatilishe tuzo mbalimbali, ambazo ilipewa huko Ulaya bila kuwepo mhusika mkuu katika migogoro hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa IPTL, Joseph Makandege, kampuni yake inaidai SCBHK fidia ya Dola za Marekani billioni 3.240 (Sh.trilioni 6.5).

Kampuni ya IPTL haijawatambua SCBHK kama wadai wake na inahoji mahakamani uhalali wa madai yao hayo.

Kampuni ya IPTL imeifungulia SCBHK kesi mbalimbali za madai ikiwamo namba 60/2014, namba 801 na 802/ 2016, na kesi za biashara namba 67 na 75/2017 zinazoendelea katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Dar es Salaam.

Imeeleza kustaajabishwa na taarifa zilizochapishwa kwenye vyombo vya habari nchini, kwamba SCBHK imepata tuzo ya Dola za Marekani 185,449,440 (Sh. 426,533,712,000) dhidi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kesi ya usuluhishi namba ARB/05/04 / 2015 katika Baraza la Kimataifa la Utatuzi wa Migogoro ya Uwekezaji London, Uingereza (ICSID).

Makandege aanasema IPTL pia imepokea tamko la serikali kupitia vyombo vya habari, lililotoa msimamo kwamba Serikali na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) haziwajibiki kuilipa SCBHK fedha hizo; kwamba serikali si mdaiwa bali ni mdhamini tu katika masuala ya IPTL; kwamba mdaiwa anayewajibika kulipa fedha hizo ni IPTL; na kwamba IPTL ilitoa kinga inayoikinga serikali na taasisi zake dhidi ya madai yoyote yatokanayo na IPTL kupewa fedha zilizokuwa katika iliyokuwa "Tegeta Escrow Account"

INAENDELEA UK 8

# RC aagiza jeshi kuhamisha ofisi za halmashauri

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ameamuru magari ya majeshi ya ulinzi na usalama kwenda kubeba nyaraka za serikali wakati wa kuhamisha ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kutoka katikati ya Jiji la Mbeya.

Chalamila alitoa agizo hilo jana, wakati wa kikao cha dharura cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri, alichokiitisha kwa lengo la kujadili utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli alilolitoa akiwa ziarani mkoani Rukwa kwa kutoa mwezi mmoja kwa halmashauri kuhamia kwenye maeneo yao badala ya kukaa kwenye miji.

Alisema tangu Rais Magufuli atoe agizo hilo, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya haijachukua hatua yoyote ya utekelezaji na zimebaki siku saba tu kwa muda uliotolewa ndiyo maana ameamua kuitisha kikao hicho.

Alisema Rais ni Amiri Jeshi Mkuu na kwamba anapotoa agizo linatakiwa kutekelezwa mara moja, hivyo akasisitiza ofisi hiyo kuhamishwa ndani ya saa 24.

Alisema katika uhamisho wa ofisi hiyo, magari ya vyombo vya ulinzi na usalama yatumike kubeba nyaraka za serikali ili kuhakikisha usalama wake huku akisisitiza unatakiwa kufanywa kama ilivyofanyika kuhamisha baadhi ya wizara kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma. "Naagiza magari kutoka Jeshi la Wananchi, Polisi na Magereza yaende kubeba nyaraka za serikali kwa ajili ya usalama kuwapeleka mnapohamia, ila mtakakokwenda mimi sijui," alisema Chalamila.

Alisema mahali ambako ofisi za halmashauri hiyo zitahamia zitakaa kwa muda wakati Baraza la Madiwani likijadili ni wapi wakajenge ofisi za kudumu.

Popote watakapohamia, alisema ni lazima waende kwenye majengo ya serikali yenye miundombinu yote inayohitajika huku akipiga marufuku matumizi yoyote ya fedha za umma kwa ajili ya ukarabati wa majengo yatakayotumika kwa muda.

Alisema fedha zozote kama zipo, zielekezwe kwenye ujenzi wa ofisi za kudumu za halmashauri hiyo kama kianzio sahihi cha upatikanaji wa ofisi za kudumu.

Baada ya kutolewa kwa agizo hilo, madiwani walianza majadiliano huku baadhi wakitaka zijengwe katika Kata ya Tembela, wengine Inyala na wengine Isangati na kila watu wakielezea maeneo wanayotaka kuwa yana miundombinu ya kutosha.

Baada ya majadiliano ya muda mrefu, maeneo matatu ya Inyara, Tembela na Isangati yaliainishwa kuwa yanafaa na ndipo Mkuu wa Mkoa akaagiza ziundwe timu tatu za kwenda kuyatembelea na kuangalia mojawapo linalofaa.

## HABARI KITAIFA

# Ofisa Takukuru mbaroni madai mauaji mke wake

**Na Stevie Chindiye, TUNDURU**

OFISA wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) wilayani Tunduru, James Paulo (27), anashikiliwa na polisi kwa tuhuma za kuua kwa kumpiga risasi mke wake.

Mtuhumiwa huyo anadaiwa kufanya kitendo hicho usiku wa kuamkia Oktoba 21, mwaka huu, baada ya kutokea ugomvi kati yao.

Kamanda Polisi Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, amethibitisha kuwapo kwa tukio hilo na kwamba chanzo cha kifo hicho ni ugomvi uliosababishwa na tukio la wivu wa kimpenzi.

Kamanda alimtaja mtu aliyeuawa kuwa ni Beatha Kufuru (25), ambaye alikuwa muuguzi katika Hospitali ya Wilaya ya Tunduru.

Kamanda Marwa ambaye alikuwa akizungumzia tukio hilo akiwa njiani kwenda Tunduru ili kujiridhisha na hali halisi, alisema mtuhumiwa huyo alimpiga risasi tatu kichwani na kusababisha kifo chake papo hapo.

Alisema polisi wanaendelea na uchunguzi wa tukio hilo na kwamba mtuhumiwa atafikishwa mahakamani baada ya kukamilika kwa taratibu za kisheria.

Mganga aliyeufanyia uchunguzi mwili wa marehemu, Dk. Stephen Hokororo, alisema chanzo cha kifo hicho kilitokana na ku-



tokwa na damu nyingi baaada ya kupigwa risasi kichwani.

Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Ruvuma, Ustina Chagaka, alikiri kupokea taarifa za ofisa wake kudaiwa kumuua mkewe na kwamba anakwenda Tunduru kufuatilia jambo hilo.

Hata hivyo, alisema ofisi yake haiwezi kuzungumzia lolote kwa sababu liko mikononi mwa polisi.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Dk. Wendi Robert, alisema walipokea mwili wa marehemu hospitalini hapo na kuufanyia uchunguzi huku akisema Beatha ameacha mtoto wa miezi tisa na kwamba mwili wa marehemu unatarajiwa kusafirishwa kwenda Mbozi mkoani Songwe.

# Wakurugenzi wazembe kwenye mapato wategwa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imewaonya wakurugenzi wote wazembe wa halmashauri nchini ambao wanasuasua kwenye ukusanyaji mapato na kuwataka kujitathmini kwa miezi mitatu ijayo.

Angalizo hilo lilitolewa jana jijini hapa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, alipokuwa akitoa taarifa ya mapato ya vyanzo vya ndani vya halmashauri kwa kipindi cha Julai hadi Septemba, kwa mwaka wa fedha 2019/20.

Alisema bajeti iliyoidhinishwa ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa mwaka huo ni Sh. bilioni 765.48, na kwamba kwa robo ya kwanza (Julai hadi Septemba, 2019) Halmashauri zimekusanya Sh. bilioni 166.24 sawa na asilimia 22 ya makisio ya mwaka.

Alisema halmashauri zilipaswa kukusanya mapato kwa asilimia 25 ya makisio yake ya mwaka, lakini halmashauri 121 hazikuweza kufikisha kiwango hicho, huku 54 pekee zikikusanya zaidi ya asilimia 25.

Alisema kwa kipindi kilichopita wakurugenzi ambao hawakufikia malengo walihojiwa na hatua zimeshachukuliwa.

"Nitoe salamu kwa wakurugenzi wengine huu ni ujumbe mwingine, msione kwa wenzenu waliopita, niwaambie ukusanyaji mapato ndio kigezo kikubwa cha kuwafanya mkae kwenye nafasi zenu, umeteuliwa kumsaidia Rais, lazima mkusanye na kusimamia mapato," alisema.

Alisema Oktoba hadi Desemba mwaka huu ni miezi ya kujitathmini wakurugenzi hao kuhakikisha malengo yao ya ukusanyaji yanaendana na asilimia ya ukusanyaji wake.

"Kinyume cha hapo watu wasije wakalaumu mbele ya safari kwa kushindwa kutimiza wajibu wao. Hizi taarifa za ukusanyaji wa mapato zinatumika kuwaondoa wakurugenzi kwa kuwa ni moja ya 'factor' muhimu zinazotumika kuwapima wakurugenzi atakayebweteka asijekumlaumu mtu," alisema.

Aliongeza: "Ukiona boti inapunguza watu eleweni haya mambo yote, Rais amefanya mabadiliko mbalimbali ya wakurugenzi, hizi ninazosoma hazitoki bure hayo mabadiliko unayoyaona miongoni mwa factor kubwa inayotumika ni mapato."

Jafo alisema wakurugenzi wanaofanya uzembe kwenye ukusanyaji mapato na matumizi ya mapato waende kuwauliza waliondolewa kwa kuwa waliondolewa kwa sababu hiyo na inafanya kazi.

MKURUGENZI BUHIGWE

"Mkurugenzi wa Buhigwe anapaswa kujitathmini, naomba Katibu Mkuu uliweke vizuri kwa sababu nilienda kutembelea Buhigwe hata utekelezaji wa miradi ya maendeleo unasuasua, hata miradi iliyopelekewa fedha na serikali kuu," alisema.

INAENDELEA UK 8




# Mbowe na wenzake kujitetea Novemba 4

**Na Hellen Mwango**

**Hakimu alisema kuhusu utetezi kutumia vielelezo ikiwamo CD ya video ya maandamano wanayodaiwa washtakiwa kuyahamasisha, uandike barua ya siku tatu kabla ya siku ya kesi ili mahakama iandae ukumbi wa kuangalia kielelezo hicho.**

MWENYEKITI Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe na wenzake wanane wanatarajia kuanza kujitetea kupangua tuhuma zinazowakabili za uchochezi baada ya siku 14.



Kesi hiyo imepangwa kuanza kusikilizwa ushahidi wa utetezi siku tatu, Novemba 4, 5 na 8, mwaka huu katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam.

Uamuzi huo ulitolewa jana na Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba baada ya kupitia hoja za pande zote mbili. Awali, utetezi uliomba siku 21 kwa ajili ya kujiandaa lakini Jamhuri walipinga.

Hakimu alisema kuhusu utetezi kutumia vielelezo ikiwamo CD ya video ya maandamano wanayodaiwa washtakiwa kuyahamasisha, uandike barua ya siku tatu kabla ya siku ya kesi ili mahakama iandae ukumbi wa kuangalia kielelezo hicho.

Alisema mahakama imekubali kutoa kielelezo hicho, lakini watatumia vitendea kazi vya mahakama chini ya usimamizi wa Mtendaji wa Mahakama hiyo.

Mbali ya Mbowe, washtakiwa wengine ni Katibu Mkuu Dk. Vicent Mashinji; Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko; Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu; Mbunge wa Kibamba, John Mnyika; na Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche.

Wengine ni Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa; na Mbunge wa Kawe, Halima Mdee; na Mbunge wa Bunda Mjini, Ester Bulaya.

Washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka 13 likiwamo la kula njama, ambapo wote wanadaiwa kuwa Februari 1 na 16, mwaka jana, Dar es Salaam waliku a njama ya kutenda kosa la kufanya mkusanyiko usio halali na kukiuka tamko kutawanyika.






Wananchi wakishangaa mwili wa kijana ambaye alikutwa amekufa chini ya daraja linalounganisha Tabata Matumbi na Buguruni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Afrika, Asia zatakiwa kusimamia maslahi yao

**Na Romana Mallya**

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, amezitaka nchi wanachama wa Shirika la Mashauriano ya Kisheria za Asia na Afrika (AALCO) kusimama pamoja ili kutetea maslahi ya nchi zinazoendelea kupitia taasisi imara za kisheria pamoja na sheria za kimataifa.

Samia aliyasema hayo jana kwa niaba ya Rais John Magufuli wakati akifungua mkutano huo wa 58 wa mwaka ambao unafanyika Tanzania kwa mara ya tatu.

Akizungumza katika mkutano huo ambao umewakutanisha zaidi ya wanachama 40, Samia alisema wanashuhudia vita vya wenyewe kwa wenyewe katika nchi zinazoendelea zikichochewa na nchi zilizoendelea ili kujipatia rasilimali za nchi husika.

Alisema nchi zinatakiwa kupambana kuhakikisha zinakuwa na taasisi imara ambazo zimeanzishwa kwenye misingi ya usawa na kuheshimu utu ili kulinda maslahi ya mataifa.

"Tunapopambana kufikia malengo yetu, tunahitaji kusimama pamoja na kuimarisha umoja tulio nao kupitia mashauriano ya mara kwa mara," alisema.

Samia alizitaka nchi wanachama kuendelea kushirikiana ili kuendeleza na kuimarisha sheria za kimataifa zilizopo za mataifa ya Asia na Afrika.

Alisema ushirikiano utachangia pakubwa kwenye maendeleo ya sheria za kimataifa hasa katika maeneo yanayohusiana na biashara za kimataifa, uwekezaji, ulinzi na usalama kikanda.

Samia aliuambia mkutano huo kwamba Tanzania imekuwa na amani na majirani zake na ni kinara wa amani katika ukanda wa Maziwa Makuu na inachangia kwa kiasi kikubwa katika ukombozi wa kisiasa.

"Tumekuwa na imani madhubuti kwamba mahali ambako kuna utawala wa sheria kuna utengamano na sehemu ambako kuna utengamano kuna ustawi na maendeleo," alisema.

Alisema Tanzania inaendelea kulinda amani katika nchi za Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC), Sudan katika eneo la Darfur na Lebanon.

Samia alitumia fursa hiyo kuzitaka nchi zilizoiwekea vikwazo Zimbabwe, kuviondoa akisema nchi hiyo ni taifa huru ambalo linahaki ya kujiamulia mambo yake.

"Tunaamini nchi wanachama zitatoa sauti ya pamoja ya kukemea tabia ya baadhi ya mataifa kuingilia mambo ya ndani ya mataifa mengine ambayo yapo huru," alisema.

# Askofu aibua neno chumvi na mafuta katika maombi

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

ASKOFU wa Kanisa la Morovian Jimbo la Magharibi, Ezekiel Yona, amewataka wachungaji na mashemasi wa kanisa hilo kutojihusisha na vitendo vya udanganyifu vinavyofanywa na baadhi ya wana maombi ambao wamekuwa wakitumia chumvi, maji na mafuta kuwahadaa waumini.

Kauli hiyo aliitoa juzi wakati wa hafla maalumu ya kuliweka wakfu wa jengo jipya la kanisa la Morovian Jimbo la Kahama Mjini pamoja na kuwasimika mashemasi na makasisi 17.

Alisema wako baadhi ya viongozi wa dini wamekuwa wakiwadanganya waumini kutumia chumvi, maji, mafuta na kubusu kinywa cha nguruwe wanapofanyiwa maombi kwamba anaponunua na kuvitumia, anaweza kupona matatizo yake jambo ambalo si kweli.

"Baadhi ya watoa huduma za maombi kwenye madhehebu mengine wanaowanywesha mafuta waumini wao na kisha wanaanguka chini kwa kugalagala na baadaye wanawaombea na kuamka. Vitendo hivi msivifanye na havikubaliki katika kanisa la Mungu," alisema.

Askofu Yona aliwataka makasisi kuendelea kuliombea taifa ili amani iendelee kudumu na kumwombea Rais John Magufuli ili aendelee kuwatetea wanyonge sambamba na kurudisha nidhamu serikalini kwa kusimamia rasilimali za nchi.

Mmoja wa makasisi wapya waliopewa daraja hilo, Emmanuel Sangosango kutoka Kanisa la Morovian kituo cha Mwanza, alisema atahakikisha anakuwa mwaminifu kwa waumini wake na kujiepusha na maombi ya kutumia mafuta na maji.

Naye Yona Mbogo kutoka Singida, alisema atahakikisha anawaelekeza watoa maombi ambao wana tabia ya kuwadanganya waumini juu ya vitu hivyo na kubusu kichwa cha nguruwe ili wapone maradhi, huku wengine wakigeuza maombi kama biashara.

# MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

TRA

## IDARA YA KODI ZA NDANI

# TAARIFA KWA UMMA

## WAJIBU WA KUTOA NA KUDAI RISITI/ANKARA ZA MASHINE ZA KIELEKITRONIKI (EFD).

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), inapenda kuwataarifu Wafanyabiashara wote na umma kwa ujumla kwamba, kulingana na kifungu namba 36 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015, kinawataka watoa Huduma au wafanyabiashara wanaostahili kutumia mashine za kielektroniki za kutolea risiti (EFD) kutoa risiti za kielektroniki kwa mauzo yote ya bidhaa au huduma yanayofanywa. Utoaji huu wa risiti za EFD ulianzishwa ili kuboresha utunzaji wa kumbukumbu za Walipakodi, kurahisisha ukadiriaji wa kodi na kuongeza ulipaji kodi kwa hiari na hivyo kuongeza pato la Taifa.

Uchunguzi uliofanywa na TRA umebaini kwamba, baadhi ya wafanyabiashara wanaendelea kutotoa risiti kwa makusudi na wengine kutoa risiti zenye viwango vya chini visivyoendana na gharama ya bidhaa au huduma iliyouzwa. Kitendo cha kutotoa risiti kupitia mashine za Kielekitroniki (EFD) ni hujuma juu ya juhudi za Serikali kukusanya mapato yanayolenga kuleta maendeleo kwa watanzania wote.

Mamlaka ya Mapato Tanzania inaendelea kuwakumbusha Wafanyabiashara kuwa, kwa mujibu wa kifungu tajwa hapo juu, muuzaji wa bidhaa au mtoa huduma anawajibika kutoa risiti/ankara sahihi kupitia mashine ya kielekitroniki (EFD).

TRA, inautangazia umma kwamba, itaendesha msako kwa biashara zote nchi nzima ili kukagua matumizi sahihi ya mashine za kielektroniki na kujiridhisha utekelezaji wa sheria husika. Mfanyabiashara yeyote ambaye atabainika kutotumia vyema mashine hizi katika biashara yake au kukaidi kutimiza wajibu huu wa kisheria atakuwa ametenda kosa na atachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwa ni pamoja na kutozwa faini inayoanzia **Shilingi 3,000,000 /-** na isiyozidi **Shilingi 4,500,000 /- au kifungo cha miaka 3 jela** au vyote kwa pamoja, kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015 kifungu cha 86.

Pia wanunuzi wote wanatakiwa kudai risiti pindi wafanyapo manunuzi ikiwa ni haki ya msingi kisheria kwa kila manunuzi. kwani kutokufanya hivyo ni kosa linaloweza kupelekea kupata adhabu kali ikiwa ni kutozwa faini inayoanzia **Shilingi 30,000 /-** na isiyozidi **Shilingi 1,500,000/-** kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015.

**Taarifa za msingi ambazo risiti/ankara inahitaji kuwa nazo ni pamoja na zifuatazo;**

1. **Jina la Mnunuzi.**
2. **Namba ya usajili ya mnunuzi (TIN)**
3. **Namba ya Usajili wa Kodi ya Ongezeko la Thamani ya mnunuzi (VRN kwa waliosajiliwa VAT).**
4. **Jina la bidhaa/huduma iliyouzwa au kutolewa.**
5. **Thamani halisi ya bidhaa/huduma iliyouzwa**

Kwa ufafanuzi zaidi tafadhali wasiliana na kituo cha huduma na elimu kwa mlipakodi kwa kupiga simu za bure: **0800780078 / 0800750075 au Barua pepe Huduma@tra.go.tz**

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

**Abdul Y. Mapembe**
**KAIMU KAMISHNA WA KODI ZA NDANI**

215466002

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ziongezwe juhudi zaidi kuwahudumia wazee

**TAARIFA** kuwa baadhi ya halmashauri na manispaa nchini zinatenga fedha kwa ajili ya kutengeneza vitambulisho vya matibabu ya wazee yanayoelezwa kuwa yatatolewa bure, zinatia moyo.

Wazee ambao wamelitumikia taifa hili kwa miaka mingi wamekuwa waathirika wa kukosa huduma za matibabu.

Licha ya kuwa na juhudi na vitambulisho hivyo, wazee wanakabiliwa na usumbufu unaowasababishia kukosa huduma kwa vile wengi hawana fedha na hawana msaada.

Ni sawa, halmashauri kutenga fedha na kuwaandalia vitambulisho lakini, suala la usumbufu ukiwamo kupewa barua za watendaji wa serikali za mitaa na barua za Idara za Ustawi wa Jamii za hospitalini wanapotakiwa kufanyiwa vipimo na kupata huduma za kibobezi zinawakatisha tamaa zaidi.

Itoshe kusema kuwa mzee atambulike kwa kitambulisho cha taifa alicho nacho ambacho kinaainisha taarifa zake zote, kuanzia umri, kabila, makazi na shughuli zake.

Mara nyingi wazee wanapokwenda hospitalini kusaka tiba wanalazimika kupitia kwa ofisa za serikali za mitaa.

Ni sawa na utaratibu bora wenye malengo mema, lakini mara nyingi ni usumbufu. Si hivyo tu ni kama kuwapa usumbufu wa ziada kwa vile wanafahamika kutokana na kadi za utambulisho walizo nazo.

Pengine suala la kuomba tena kupata msamaha wa matibabu kwenye ofisi za Ustawi wa Jamii hospitalini ni usumbufu mwingine usio na sababu wanaopitia wakati wakifuatilia vipimo vikubwa kama CT - Scan na MRI au Ultrasound.

Wakati mwingine tunashawishika kusema kuwa hakuna sababu ya kuwa na vitambulisho hivyo. Pengine wangetumia vitambulisho walivyo navyo kama vile vya kupigia kura au vya utaifa.

Taarifa hizo zinaweza kutosha kumtambulisha mtu kuwa ni mzee, yote hayo yakifanyika ili kuwaepushia usumbufu usio na sababu hasa kwenye kuwafikia madaktari bingwa na wabobezi.

Licha ya serikali kufanya jitahidi mbalimbali kutatua changamoto lukuki zinazowakabili wazee hasa kwa upande wa matibabu, upatikanaji wa dawa ni matatizo yananayowakabili watu wazima hawa.

Mara nyingi wazee wamekuwa wakikabiliwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa matibabu hasa dawa kwa vile wapo wasio na uwezo wa kununua.

Wazee wengine wanaona kuwa licha ya kupewa vitambulisho hivyo vya matibabu bure, lakini wanapokwenda hospitalini mara nyingi huambiwa hakuna dawa.

Tunaona kuwa ni wakati wa kuwa na dirisha la wazee lakini, pia kuanzisha kanzi data yenye taarifa zao, kama ilivyo kwa daftari la wapiga kura.

Licha ya kwamba baadhi ya hospitali zimeshatenga madirisha ya wazee kwenye huduma za afya ni wakati wa kuwa na madirisha hayo katika hospitali za mikoa na rufani.

Aidha, tunashauri kuwa ni vyema pia kuwa na maduka ya dawa za wazee ikichukuliwa kuwa magonjwa ya uzeeni yanahitaji tiba muhimu na yana gharama kubwa na hata kutumia wabobezi.

Wazee husumbuliwa na matatizo ya moyo kupanuka, maradhi ya mifupa, mishipa ya fahamu na wakati mwingine saratani.

Magonjwa hayo yanachunguzwa kwa vipimo vya gharama kubwa na wakati mwingine wagonjwa wanakutana na misururu mirefu ya kungojea matibabu (appointment).

Kwa hiyo ni wakati wa kuwafikiria wazee na kuona uwezekano wa wakuwaondoa kwenye misururu hiyo.

Kuwapa vipaumbele kwenye vipimo vya MRI, CT-Scan na tiba nyingine zenye misururu ya kuwafikia wabobezi ni jambo muhimu kwenye kuwahudumia wazee na kuwapa tiba kwa utaratibu rafiki.

Baadhi ya huduma ambazo pengine watu wanalazimika kuzichangia itabidi serikali kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii, izipatie ufumbuzi wa namna ya kuzipata ili kuwasaidia wagonjwa hao.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Ziara ya JPM muhimu utatuzi madai wakulima wa pamba

Na Raphael Kibiriti

**KWA** walio na maslahi katika ustawi wa wakulima na hasa wale wadogo wadogo ambao ndio wengi nchini ukilinganisha na wakulima wa kibiashara, wataungana na mtazamo wa Muungwana.

Ni kuhusiana na ziara za Rais John Magufuli maeneo tofauti nchini ambazo amekuwa akizifanya kwa lengo la kukagua shughuli za maendeleo na kutatua changamoto zinazowakabili wananchi.

Hii ni kwa sababu ziara hizo zimeleletea neema kundi hili linalotegemea kilimo kama chanzo kikubwa cha kiuchumi kwa minajili ya kukidhi mahitaji ya kimaisha na maendeleo kwa ujumla wake.

Muungwana anataja ziara ya Rais Magufuli katika mikoa ya Lindi na Mtwara kuhalalisha anachojaribu kukieleza katika safu hii.

Ziara ambayo pamoja na mengine imetatua changamoto ya madai ya baadhi ya wakulima wa korosho, ambao walikuwa bado hayajalipwa fedha zao.

Akiwa wilayani Masasi mkoani Mtwara wakati wa ziara yake iliyomalizika hivi karibuni, Rais Magufuli alibainisha kwamba kiasi cha Sh. bilioni 72 tayari kimeshatengwa na serikali kulipa wakulima wa zao hilo waliokuwa bado wanaidai serikali.

Akatoa maagizo kupitia kwa Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, fedha hizo zianze kulipwa mara moja.

Kwamba wakulima wote wenye madai wawe wamelipwa fedha zao kabla ya kuingia kwenye mnada mpya wa zao hilo unaoanza mwisho wa mwezi huu.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, malipo hayo yanatarajiwa kuanza kutolewa leo na hivyo kumaliza sakata la madai hayo ya wakulima wa korosho.

Ndivyo pia ilivyokuwa katika ziara yake aliyoifanya mikoa ya Rukwa na Katavi, ambako changamoto mbalimbali za wakulima, wakiwamo wa zao la pamba alizitatua.

Akizungumza na wananchi kwenye mkutano wa hadhara katika uwanja wa Azimio mjini Mpanda, Oktoba 10, Rais Magufuli alitoa siku 14 kwa mawakala wote mkoani humo wanaonunua pamba kuhakikisha wamewalipa wakulima fedha zao.

Agizo hilo lilifuatia malalamiko waliyoyatoa mbele yake kwamba pamoja na kuuza pamba yao na kusafirishwa na wanunuzi kutoka kwenye Maghala ya Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS), hawajalipwa fedha zao kwa muda sasa.

Kwamba baadhi yao hawajalipwa madai yao kwa zaidi ya miezi miwili hadi sasa, wakati msimu wa kilimo ukiwa mbioni.

Mbali na kutatua changamoto hizo za wakulima, ziara hizo zimeleta neema karibu katika sekta zote kuanzia kwenye miundombinu ya barabara, maji, afya, stendi, masoko, matatizo ya kawaida ya wananchi na maeneo mengine yaliyoguswa kwa njia moja au nyingine na ziara hizo.

**Akiwa wilayani Masasi mkoani Mtwara wakati wa ziara yake iliyomalizika hivi karibuni, Rais Magufuli alibainisha kwamba kiasi cha Sh. bilioni 72 tayari kimeshatengwa na serikali kuwalipa wakulima wa zao hilo waliokuwa bado wanaidai serikali.**

Sasa wakati Rais Magufuli akiwa ametatua changamoto hizo ikiwamo ya madai ya fedha za wakulima wa korosho katika mikoa ya Lindi na Mtwara, na ya wakulima wa pamba katika mkoa wa Katavi, anaona ni vyema akawa na ziara mahsusi katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Anasema hivyo kutokana na ukweli kwamba bado kuna wakulima wengi wa pamba ambao hadi sasa hawajalipwa fedha zao, wengine ikiwa ni zaidi ya miezi miwili wakati tayari pamba yao imeshasombwa kupelekwa kwenye viwanda ya pamba na wanunuzi kutoka AMCOS.

Wakulima hawa wanaendelea kusubiri wanunuzi wawalipe fedha zao ili pamoja na mengine wazitumie kwenye kilimo kwani msimu wa kilimo tayari umeshaanza katika kanda hiyo.

Wengi wanategemea fedha hizi ili pamoja na mengine waweze kugharimia mbegu, mbolea, dawa, upandaji, palizi, na mnyororo mzima wa kilimo ambao takribani kila hatua unahitaji fedha.

Muungwana anaona suluhu ya haraka kwa wakulima ambao hawajalipwa fedha zao hadi sasa ni ziara ya Rais Magufuli katika Kanda hiyo.

Ninasema hivyo kwa sababu Rais Magufuli atasikia moja kwa moja kilio hiki kutoka kwa wakulima wenyewe na atachukua hatua mara moja kutatua changamoto hii kama alivyofanya katika mikoa ya Rukwa na Katavi na kwenye mikoa ya Lindi na Mtwara.

# Mabucha ya nyama ya porini Desemba

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

WIZARA ya Maliasili na Utalii, imeshaanza kutekeleza agizo la Rais John Magufuli alilolitoa hivi karibuni mkoani Katavi la kuanzisha mabucha ya kuuza nyamapori kwa wananchi wanaoishi pembezoni na hifadhi za taifa.

Wizara hiyo pia imesema ifikapo Desemba mwaka huu, wananchi wataanza kunufaika na kitoweo hicho katika maeneo yao.

Akizungumza jijini Arusha, Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Prof. Adolf Mkenda, alisema ofisi yake imeshapitisha kanuni na rasimu ambayo imeshawasilishwa kwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangalla ili ijadiliwe. "Tumeshaanza kutekeleza agizo la Rais Magufuli kwa ajili ya kuunza nyamapori kwa ajili ya wananchi kama kitoweo ili kupunguza vitendo vya ujangili vinavyofanywa na baadhi ya wananchi wanaoishi pembezoni mwa hifadhi zetu za taifa," alisema Prof. Mkenda.

Alisema kanuni hiyo itatoa mwongozo wa aina ya wanyama watakaowindwa na utaratibu mzima wa uwindaji, bei ya kuuza na namna ya kufungua mabucha hayo kabla ya Desemba.

Alisema wanyama wote watakaowindwa kwa ajili ya kuuzwa kwenye mabucha hayo, lazima wapimwe na madaktari kwa sababu wana magonjwa mengi ambayo yanaweza kuleta athari kwa binadamu.

Alisema wananchi wengi wa mikoa ya kusini wanaoishi karibu na hifadhi za taifa, chakula kikuu chao ni cha asili ambacho ni wanyamapori, hivyo mabucha hayo yatakuwa mwarobaini wa kudhibiti ujangili wa kitoweo.

Oktoba 10, mwaka huu Rais Magufuli akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Katavi wakati akihutubia wananchi wa mji wa Mpanda, aliiagiza Wizara ya Maliasili na Utalii, kufungua mabucha ya wanyamapori ili wananchi wapate kitoweo.



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakipita jirani na shimo kubwa lililopo katika makutano ya Mtaa wa Libya na Bandi, jana, ambalo ni hatari kwa waenda kwa miguu na vyombo vya moto. **PICHA: JOHN BADI**

# Wanawake wapigiwa debe usalama chakula

**Na Mwandishi wetu**

WANAWAKE wana nafasi kubwa ya kuongeza usalama wa chakula, upatikanaji na uhakika wake kwa ngazi ya familia na taifa.

Licha ya umuhimu wao katika jamii bado hawajapewa kipaumbele na kuthaminiwa kutokana na mfumo dume ambao umewaweka nyuma katika nyanja mbalimbali za kimaendeleo.

Mtafiti na Mshauri wa Sera wa Shirika la Oxfam Tanzania, Dk. George Mwita, ameyasema hayo katika andiko lake kuhusu Siku ya Chakula Duniani na mchango wa wanawake.

Katika andiko hilo alilolitoa karibuni, alisema wanawake hawazifikii fursa mbalimbali ikiwamo umiliki na matumizi ya rasilimali.

Pia alisema wanawake hawapati mafunzo na taarifa za kutosha kuhusiana na masuala ya kilimo, jambo ambalo ni kinyume cha ibara ya 14 ya mkataba wa kuondoa aina zote za ukandamizaji dhidi ya wanawake.

"Wanawake wanafanya kazi kubwa sana katika jamii, lakini nguvu na jitihada zao hazijatambuliwa. Wanawajibika na shughuli za nyumbani kama kutafuta maji, nishati, kilimo na ufugaji, ikiwamo kuuza mazao kwenye masoko ya maeneo yao," alisema.

Aidha, alisema wanawake wana wajibika kutunza mifugo, uvuvi na shughuli za misitu, lakini kwa bahati mbaya mchango wao haujathaminiwa.

Dk. Mwita alisema Oxfam Tanzania inafanya utafiti kuthaminisha kazi hizo ambazo wanawake huzifanya bila kulipwa ili kutambua na kupunguza ugumu na muda wa kazi, ikiwamo kuzigawa kwa usawa kwa wanaume.

# Msako mkali wakaidi EFD

**Na Gwamaka Alipipi**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imetangaza kuendesha operesheni kuwabaini wafanyabiashara ambao hawatumii mashine za kielektroniki (EFD) katika miamala yao ya kibiashara.

Sambamba na hilo imesema mtu yeyote atakayebainika atatozwa ama faini kuanzia Sh. milioni tatu hadi milioni 4.5, kifungo cha miaka mitatu jela au vyote kwa pamoja.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kaimu Kamishna wa Kodi za Ndani wa mamlaka hiyo, Abdul Mapembe, viwango hivyo vya faini ni kutoka katika Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015 kifungu cha 86.

Mapembe alisema wanunuzi nao wanatakiwa kudai risiti pindi wanaponunua vitu vinginevyo wakibainika watatozwa faini kuanzia Sh. 30,000 hadi Sh. milioni 1.5.

Alisema taarifa za msingi ambazo risiti inahitaji kuwa nazo ni pamoja na jina la mnunuzi, namba ya usajili ya mnunuzi, namba ya usajili ya kodi ya ongezeko la thamani ya mnunuzi, jina la bidhaa, huduma iliyouzwa au kutolewa, thamani halisi ya bidhaa au huduma iliyouzwa.

"TRA inautangazia umma kwamba itaendesha msako kwa biashara zote nchi nzima ili kukagua matumizi sahihi ya mashine za kielektroniki na kujiridhisha utekelezaji wa sheria husika," alisema Mapembe.

Alisema uchunguzi uliofanywa na TRA imebaini kwamba baadhi ya wafanyabiashara wanaendelea kutotoa risiti kwa makusudi na wengine kutoa risiti zenye viwango vya chini visivyoendana na gharama ya bidhaa au huduma iliyouzwa.

Alisema kitendo cha kutotoa risiti kupitia EFD ni hujuma juu ya juhudi za serikali kukusanya mapato yanayolenga kuleta maendeleo kwa Watanzania wote.

**"TRA inautangazia umma kwamba itaendesha msako kwa biashara zote nchi nzima ili kukagua matumizi sahihi ya mashine za kielektroniki na kujiridhisha utekelezaji wa sheria husika," alisema Mapembe.**

# Madai ya rushwa yaizindua CCM

INATOKA UK 2

kinyang'anyiro hicho ili kufanya uamuzi wenyewe baada ya baadhi ya majina kukatwa na uongozi wa kata.

Sakata hilo lilianza juzi asubuhi baada ya wanachama hao kujitokeza katika viwanja vya CCM Kasanga B ili kushiriki kupiga kura za maoni, lakini ghafla walikuta baadhi ya wagombea majina yao hayapo na kuanza kwa mzozo huo.

Mmoja wa wanachama hao, Juma Abdul, alisema baada ya kufika katika viwanja hivyo majira ya saa 2:00 asubuhi wakiwasubiri wasimamizi wa uchaguzi ambao walichelewa na hadi saa 7:00 mchana huku wanachama wakiwa wamekata tamaa na baadhi yao kuondoka.

Alisema baada ya wasimamizi hao kufika, walianza kusoma majina ya wagombea huku wengine majina yao yakiwa hayapo ndipo ulipoanza mzozo huo na kutaka majina mengine yarudishwe ndipo kura zipigwe.

Naye Amina Rashid alisema viongozi wa CCM wa kata hiyo wamefanya ujanja na kuweka majina wanayotaka ikiwamo kukata majina ya wanawake walioingia katika kinyang'anyiro hicho na kubakisha wanaume, hivyo hawako tayari kufanya uchaguzi mpaka uongozi wa wilaya ufike kutatua tatizo hilo.

Baada ya mzozo huo, Katibu wa CCM Kata ya Mindu, Hamisi Halili, alisema wamerudisha majina hayo sita baada ya kufanya mchujo ili wanachama wachague hatua ambayo ilipingwa vikali na kuamua kususia uchaguzi huo.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Morogoro Mjini, Fikiri Juma, alikiri kutofanyika uchaguzi huo na kwamba tayari wameingilia kati mchakato huo ikiwa pamoja na kurudisha majina yote ya wagombea waliomba nafasi hiyo ili wanachama wafanye uamuzi wa kuchagua wale wanaowataka. Alisema walitarajia uchaguzi huo ufanyike jana.

**DODOMA KURUDIWA**

KATIBU wa CCM Mkoa wa Dodoma, Janath Kayanda, ameagiza vituo vyote ambavyo uchaguzi haukufanyika, mchakato huo ufanyike leo.



Kayanda alisema jana kuwa changamoto mbalimbali zilijitokeza na kukwamisha uchaguzi na kuagiza majina yote ya wanachama walioomba nafasi ya uenyekiti ndani ya chama katika maeneo yao, yaingie kwenye utaratibu wa kupigiwa kura upya.

Kayanda alisema hayo alipokuwa akizungumza na wananchama wa CCM alipotembelea baadhi ya vituo ambavyo havikufanya uchaguzi katika Jiji la Dodoma jana kutokana na kuwapo kwa malalamiko mbalimbali kutoka kwa wanachama.

Aliagiza marudio ya uchaguzi huo kusimamiwa kwa karibu na viongozi wa chama kuanzia ngazi ya tawi hadi wilaya ili kusikiliza malalamiko yanapojitokeza kwenye vituo vya kupigia kura.

Naye Selemani Issa, aliyekuwa mgombea katika nafasi ya Mwenyekiti wa Mtaa wa Mkwajuni Kata ya Kiwanja cha Ndege Wilaya ya Dodoma, alitaja changamoto zilizosababisha wanachama hao kukata rufani ofisi ya wilaya ni kutoridhishwa na utaratibu uliotumika kurudisha majina ya wagombea.

Aliitaja changamoto nyingine ni wagombea kutopewa nafasi ya kujinadi kwa wapiga kura kama utaratibu ulivyoelekeza kuwa kabla ya uchaguzi kufanyika lakini matokeo yake wanachama wamekutana na majina kwenye vituo vya kupigia kura bila kuwajua wahusika sura zao.

Pia alisema sababu nyingine ni kukatwa kwa baadhi ya majina ya wagombea ambao walichukua fomu kuomba kuchaguliwa kwa nafasi za wenyeviti na wajumbe wa mitaa husika.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Dodoma Dodoma, Robert Mwinje, alisema katika eneo lake kuna baadhi ya vituo katika kata zisizozidi 10 havikupiga kura kutokana na changamoto hizo zilizojitokeza.

Alizitaja baadhi ya kata ambazo vituo vyao hawakupiga kura kwa sababu ya malalamiko yaliyojitokeza kuwa ni Chang'ombe, Nkuhungu, Msalato, Dodoma Makulu, Kiwanja cha Ndege, Matumbulu na Hombolo.

Mwenyekiti huyo baada ya kutembelea kituo cha Njedengwa Magharibi aliagiza kurudiwa kwa uchaguzi katika kituo hicho jana mchana na wanachama wote walioomba kuchaguliwa, majina yao yaingie kwenye orodha ya wagombea.

***Imeandikwa na Mwandishi Wetu, DAR, Ashton Balaigwa, MOROGORO na Ibrahim Joseph, DODOMA.***

# Wakurugenzi wazembe kwenye mapato wategwa

INATOKA UK 3

Jafo alisema hali hiyo ni udhaifu wa hali ya juu na kwamba halmashauri hiyo inapaswa kujitathmini na ufuatiliaji ufanyike ili kujua tatizo la Buhigwe kukusanya Sh. milioni 35.15 na ikiwezekana mamlaka ya uteuzi ishauriwe.

**MSALALA KINARA**

Akizungumzia mwenendo wa ukusanyaji, Jafo alisema Halmashauri ya Wilaya ya Msalala imekuwa ya kwanza kiasilimia kwa kukusanya mapato kwa asilimia 52 ya makisio ya mapato ya ndani kwa mwaka huu.

**KWERWA MKIANI**

"Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa imekuwa ya mwisho kwa kukusanya mapato ya ndani kwa asilimia tatu ya makisio yake," alisema.

**JIJI DODOMA MAPATO MENGI**

Hata hivyo, alisema Halmashauri ya Jiji la Dodoma imeongoza kwa kuwa na makusanyo ya mapato mengi zaidi kuliko halmashauri zote kwa kukusanya Sh. bilioni 13.10 huku, Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe ikiwa ya mwisho kwa kukusanya Sh. milioni 35.15.

**HALI ILIVYO KWA MIKOA**

Jafo alisema Mkoa wa Rukwa umeongoza kiasilimia kwa ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa wastani wa asilimia 31 ya makisio yake ya halmashauri za mkoa huo.

Aidha, alisema mkoa wa mwisho kwa kigezo hicho ni Mtwara ambao umekusanya wastani wa asilimia 13 ya makisio ya mwaka ya halmashauri za mkoa huo.

Kuhusu wingi wa mapato kwa mikoa, Waziri Jafo alisema Dar es Salaam umeongoza kwa wingi wa mapato ambapo umekusanya Sh. bilionin 39.53.

"Mkoa wa mwisho katika wingi wa ukusanyaji wa mapato ni Mkoa wa Kigoma ambao umekusanya Sh. bilioni 2.12 katika kipindi hicho, Kigoma hii ni sehemu ya kujitathmini mwangalie ni kwa namna gani mtaongeza mapato," alisema.

Sambamba na hilo, alisema kwa upande wa halmashauri za majiji, Jiji la Dar es Salaam limeongoza kiasilimia kwenye makusanyo kwa asilimia 38 ya makisio yake ya mwaka.

"Halmashauri ya Jiji la Dodoma imekuwa ya mwisho katika kundi hili ambapo imekusanya kwa asilimia 18 ya makisio yake ya mwaka, "alisema.

Kwa upande wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga imeongoza kwa kukusanya kwa asilimia 42, huku Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma ni ya mwisho ambapo imekusanya kwa asilimia tisa.

Jafo alisema Halmashauri ya Mji wa Tunduma imeongoza kwa kukusanya kwa asilimia 39 ya makisio ya mapato ya ndani, huku Halmashauri ya Mji wa Nanyamba imekuwa ya mwisho kwa kukusanya asilimia nne.

Hata hivyo, alisema kwa ujumla kwa Halmashauri za Wilaya, Halmashauri ya Wilaya ya Msalala imeongoza kiasilimia kwa kukusanya asilimia 52, huku Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa ni ya mwisho kwa kukusanya asilimia tatu ya makisio yake.

"Kwa ujumla kwa Halmashauri za Majiji, katika kipindi hicho, Halmashauri ya Jiji la Dodoma imeongoza kundi la Halmashauri za Majiji kwa kukusanya Sh. bilioni 13.098, huku Jiji la Mbeya likiwa la mwisho katika kundi hili la wingi wa mapato kwa kukusanya Sh. bilioni 2.74,"alisema.

Halmashauri za Manispaa, Manispaa ya Ilala imeongoza kwa kukusanya Sh. bilioni 13.05 huku Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma imekuwa ya mwisho katika kundi kwa kukusanya Sh. milioni 235.11.

"Katika kipindi hiki, Halmashauri ya Mji wa Geita imeongoza kwa wingi wa mapato katika Halmashauri za Miji ambapo imekusanya Sh. bilioni 2.34, huku Halmashauri ya Mji wa Nanyamba ikiwa ya mwisho katika kundi hili, ambapo imekusanya Sh. milioni 74.72," alisema.

Pia alisema kwa Halmashauri za Wilaya, Chalinze imeongoza kwa kukusanya mapato mengi kwa Halmashauri za Wilaya ambapo imekusanya Sh. bilioni 2.05, huku Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe imekuwa ya mwisho katika kundi hilo ambapo imekusanya Sh. milioni 35.

Alizitaka halmashauri zifanye jitihada kuhakikisha zinachangia mapato yake ya ndani kulingana na

asilimia inayopaswa kuchangiwa kwa mujibu wa bajeti zake kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

# IPTL yapinga kortini madai ya benki

INATOKA UK 2

katika Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Kimsingi, IPTL tunakubaliana na msimamo huo wa serikali. Tunatambua kwamba, kama mdhamini wake, serikali haiwajibiki kuilipia madeni yake, jukumu hilo ni lake. Serikali inawajibika tu kusimamia na kuhakikisha kwamba IPTL inalipa madeni yake yote halali inayodaiwa na wadai wake, deni hilo la SCBHK likiwamo, kama kweli ni deni halali la IPTL.

Hata hivyo, madai na tuz0 hiyo ya SCBHK ni miongoni mwa masuala ambayo bado yanabishaniwa na ambayo IPTL bado ina haki ya kuyahoji na fursa ya kuyabatilisha mahakamani. SCBHK pia bado inapaswa kuthibitisha uhalali wa tuzo hiyo katika mahakama za Tanzania. Maamuzi ya Mahakama za Tanzania (Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani, kama yeyote atakayekata rufani) ndiyo yatahitimisha mzozo kama kweli SCBHK ni mdai halali wa IPTL au vinginevyo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, IPTL hatimaye itashinda katika mashauri yake hayo, SCBHK yaweza kupoteza kabisa uhalali wa kuendelea kuibughudhi IPTL na serikali kwa madai yake au yaweza kukata deni lake hilo Sh. bilioni 426.53 katika Sh. trilioni 6.5 inazodaiwa na IPTL na kuilipa IPTL kiasi kitakachobakia. Na hatakama hatimaye itashindwa katika mashauri yake hayo, IPTL haitashindwa kulipa deni hilo la SCBHK; kwani kiwanda na rasilimali zake zingine zinatosha kuuzwa na kulipia madeni yake sambamba na hilo la SCBHK. Na hata kama hatimaye, mazungumzo yatahitajika, IPTL (siyo Serikali) ndiyo itazungumza na kukubaliana na SCBHK, kwani IPTL na SCBHK ndiyo wadau katika mashauri husika, wenye haki na wajibu huo.

"Katika muktadha huo, IPTL inakubaliana na inaunga mkono kwa dhati msimamo wa serikali na inaahidi kufanya kila liwezalo kulipa madeni yake, lakini inaomba iwezeshwe kufanya hivyo kwa kulipwa madeni yake na kurudishiwa leseni yake ya kufua na kusambaza umeme wa bei nafuu na wa uhakika kwa maendeleo ya Watanzania na Taifa zima katika uchumi wa viwanda," ulisema.

**"Katika muktadha huo, IPTL inakubaliana na inaunga mkono kwa dhati msimamo wa serikali na inaahidi kufanya kila liwezalo kulipa madeni yake, lakini inaomba iwezeshwe kufanya hivyo kwa kulipwa madeni yake na kurudishiwa leseni yake ya kufua na kusambaza umeme wa bei nafuu na wa uhakika kwa maendeleo ya Watanzania na Taifa zima katika uchumi wa viwanda," ulisema.**

HABARI KITAIFA

# Wagonjwa saratani wachangiwa damu

Na Mwandishi Wetu

WAGONJWA wa saratani katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road jijini Dar es Salaam, wamechangiwa damu ili kuwezeshwa kupata matibabu.

Uongozi wa taasisi hiyo umesema kuwa kuna changamoto ya upatikanaji wa damu kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa wa saratani.

Damu hiyo ilichangwa na wafanyakazi wa Benki ya NMB Kanda ya Dar es Salaam mwishoni mwa wiki ili kuwawezesha wagonjwa wa saratani wanaotibiwa katika taasisi hiyo kupata matibabu.

Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Tiba wa Ocean Road, Dk. Mark Mseti, alisema kwa siku za hivi karibuni hospitali hiyo imekuwa ikikabiliwa na upungufu mkubwa wa damu hali inayokwamisha utoaji huduma kwa kiwango kinachostahili.

Mseti alisema mahitaji ya damu katika hospitali hiyo ni makubwa kutokana na tiba zote za mionzi na Cemotherapy kuhitaji wagonjwa kuwa na damu ya kutosha ili ziweze kufanya kazi sawasawa.

"Tunahitaji chupa za damu 50 kila siku, kuna wakati Mpango wa Taifa wa Damu Salama unaileta kwa kiwango kinachostahili tunapata chupa 50 au 40 na tunaweza kufanya kazi kama inavyostahili lakini hivi karibuni kwa takribani wiki mbili hivi kumetokea upungufu mkubwa wa damu kwenye taasisi yetu. Kwa mfano jana na juzi tulipata chupa zisizozidi 30 kwa siku," alisema Dk. Mseti.

Akizungumza wakati wa uchangiaji damu ulifanyika Dar es Salaam juzi Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Badru Idd, alisema lengo la kushiriki zoezi hilo ni kuangalia jinsi ya kuokoa maisha ya Watanzania wenzao wenye maradhi hayo.

Idd alisema kupitia zoezi walilolifanya linapaswa kuwa wito kwa Watanznaia wengine kuona sababu ya kushiriki kutoa damu katika hospitali hiyo ili kuwezesha utoaji wa huduma kwa wagonjwa.

"Nimetembezwa hospitalini unakuta hata hiyo damu inayohitajika haipo ni kidogo, Watanzania tujitolee kama tulivyofanya NMB ili kuweza kuokoa maisha ya watu kama tunavyoona wengi wanahitaji huduma hiyo," alisema Idd.

**"Tunahitaji chupa za damu 50 kila siku, kuna wakati Mpango wa Taifa wa Damu Salama unaileta kwa kiwango kinachostahili tunapata chupa 50 au 40 na tunaweza kufanya kazi kama inavyostahili lakini hivi karibuni kwa takribani wiki mbili hivi kumetokea upungufu mkubwa wa damu kwenye..."**

# Wananchi washauri ujenzi wa makao ya halmashauri

**Restuta Damian, BUKOBA**

BAADHI ya wakazi wa Halmashauri ya Bukoba mkoani Kagera, wamewaomba viongozi kuzingatia maamuzi ya kikao cha baraza la madiwani kupendekeza eneo la kujengwa makao makuu ya halmashauri.

Wamesema uongozi unapaswa kuzingatia maslahi ya wananchi.

Wananchi hao walitoa kauli hiyo kwa nyakati tofauti wakati wakifanya mahojiano na Nipashe ilipofika katika Tarafa ya Rubale ambayo inadaiwa kuwa na sifa za kujengwa kwa makao makuu ya Halmashauri ya Bukoba kwa mujibu wa maelekezo ya Rais John Magufuli kusogeza kuduma karibu na jamii.

Peter Kasiga, mkazi wa Tarafa ya Rubale, alisema kitendo cha Rais kuamua kuhamisha halmashauri kuzipeleka karibu na wananchi amekuwa na mtazamo mpana kwa sababu anapenda kuwahudumia wananchi wake na wapate huduma stahiki.

Kasinga alisema ameshangazwa na hatua ya halmshauri yao kuhama kilomita saba kutoka Manispaa ya Bukoba umbali wa kilomita sita kwenda wilayani Muleba.

"Makao makuu ya halmashauri yanatakiwa kuwa katikati ambapo ni Rubale na sio Bujunangoma pembeni mwa halmashauri," alisema Kasiga.

Joel Kamugisha, mwenyekiti wa Kijiji cha Rubale, alisema katika kutenga eneo la makao makuu hawakuwafikiria wananchi wa pembezoni kama wanaotoka Kijiji cha Kamkole wanaotembea umbali mrefu na kufika Bujunangoma eneo lililopendekezwa wanalazimika kutumia Sh. 12,000. Kamugisha, alisema kutoka Bujunangoma kwenda Rubale ni Sh. 3,000, lakini kutoka Bujunangoma yalipopendekezwa kuwa makao makuu kwenda Bukoba Manispaa ni Sh. 1,000.

Alisema upande wa Rubale ndio una kata nyingi ukilinganisha Bujunangoma iliyopendekezwa kwa madai kuwa Rubale kuna kata 20 na Bujunangoma kuna kata tisa na jumla ya kata zote za halmashauri ni 29.

Edmin Terugwa, alisema makao makuu ya halmashauri kuwa Tarafa Rubale ni sahihi kwa kuzingatia idadi ya wakazi na watu wanaohitaji huduma karibu.

Alisema haoni sababu ya halmashauri kuhamia Kemondo na kupanga nyumba kwa ajili ya osifi kuwa ni matumizi mabaya ya fedha za serikali kwa sababu eneo la kuanzia kuna majengo zaidi ya sita mali ya halmashauri yenye huduma muhimu za umeme na maji.

Damian Ishengoma, alisema lengo la serikali ni kusogeza huduma karibu na jamii.

Katika kikao cha Baraza la Madiwani Oktoba 16, mwaka huu baada ya mvutano wa kupendekeza eneo la makao makuu ya halmashauri hiyo, waliamua kupiga kura kwa kutumia kanuni ya 28 na jumla ya kura zilkuwa 29, Bujunangoma walipata kura 22, Rubale kula 16 na Kyema kura moja.

Kabla ya kupiga kura mwenyekiti wa halmashauri, Murshid Ngeze, aliwaeleza madiwani kuhakikisha wanafuata mwongozo wa Rais wa kusogeza huduma karibu na wananchi.



Katapila la kampuni ya ukandarasi likichonga barabara ya Kitunda yenye urefu wa kilomita 3, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wakulima korosho wachangamkia msimu

**Na Hamisi Nasiri, NEWALA**

ZAIDI ya tani 200 za korosho zimeshakusanywa kwenye maghala ya Chama Kikuu cha Ushirika cha Newala pamoja na Tandahimba Cooperative Union (TANECU) mkoani Mtwara kwa msimu wa mwaka 2019/2020.

Hayo yalisemwa wilayani Newala na Mkuu wa Wilayani ya Newala, Aziza Mangosongo, baada ya kutembelea maghala ya Tanecu, Agrofocus na Splenders Control Ltd, na kusema kuwa baada ya msimu kufunguliwa, angefanya ziara hiyo ili kuona hali ya maghala na jinsi yalivyoanza kufanya makusanyo ya korosho kwa msimu huu.

Alisema hali ya maghala inaridhisha na kuwa matumaini yake ni kuwa mwitikio wa wakulima umekuwa chanya zaidi katika kukusanya korosho hizo.

"Kwenye Amcos nilizotembelea nimekuta tayari zipo tani 400 ambazo zinatarajia kufika kwenye vyama muda si mrefu mambo yote yako vizuri na tumejipanga kwenye magunia na kuhakikisha usalama wa wakulima wakati wa kuleta korosho zenye ubora kwa wakati," alisema Mangasongo.

Makamu Mwenyekiti wa TANECU, Shaibu Njauka, alisema kwa Wilaya ya Tandahimba kwenye ghala la Tandahimba limeshapokea kiasi cha tani 76,565 za korosho kutoka kwa baadhi ya AMCOS na bado zoezi linaendelea kwa kasi kubwa.

"Makusanyo yameanza kwa kasi kubwa na upo uwezekano wa kupata mzigo mkubwa ndani ya wiki, hivyo msimu umeshafunguliwa... korosho zipelekwe Amcos zikiwa kwenye madaraja ili kuziwahisha sokoni, maghala yako wazi korosho za msimu uliopita hazipo sasa tunakusanya korosho mpya kwa Newala na Tandahimba," alisema Njauka.

Mashua Said, Mwenyekiti wa Chama cha Msingi cha Enganero Kata ya Mkunya wilayani Newala, alisema ndani ya siku tatu amefanikiwa kukusanya zaidi ya tani 60, hali ambayo imempa hofu kutokana na wingi huo wa korosho.

# WEZA yawawezesha wanawake tril. 1.5/-

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

WANAWAKE wa Zanzibar kwa miaka 4 wamefanikiwa kujiwekea akiba ya Sh. trilioni 1.5, jambo lililowawezesha kujiongeza kiuchumi, kimapato na ushindi kwenye vita ya umaskini.

Taarifa ya Asha Abdi Makame, Kaimu Mkurugenzi, Chama cha Wanawahabari Wanawake Tanzania (Tamwa Zanzibar), ilisema na kuongeza kuwa kukusanya akiba hiyo kulianza tangu Januari 2016 hadi Juni 2019.

Iliongeza katika jitihada za kuwasaidia na kuwainua wanawake wa Zanzibar, kinamama walihamasishwa kujiwekea akiba ya Sh. milioni 213, fedha zilizowekwa kuanzia mwaka 2016.

Kuanzia mwaka 2016 wanawake hao waliweza kujiwekea Sh. milioni 312 na ilipofika Juni 2019 kipato chao kiliongezeka kwa asilimia 80 na kufikia trilioni 1.5.

Awali wakati mradi unaanza wanavikundi walikuwa wakiweka akiba ya Sh. 250 kwa wiki, miaka miwili baadaye kwa kuwa kipato chao kilikua waliweka Sh. 3,800 hivyo kuanzia Januari hadi Juni waliweka Sh. 224,672,000, ilisema taarifa ya Tamwa Zanzibar.

Makame alisema Tamwa Zanzibar ikishirikiana na Milele Zanzibar Foundation (MZF) waliendesha programu maalum ya kukuza uwezo wa kiuchumi wa wanawake Zanzibar uliopewa jina la WEZA II ili kupunguza umaskini.

Dhamira kuu ya WEZA II ilikuwa ni kupunguza umaskini kwa wanawake na kuweza kusimamia masuala yanayogusa maisha yao ya kila siku, ilisema taarifa ya Tamwa Zanzibar. Iliongeza kuwa vikundi 280 vyenye watu 6,000 vilifikiwa na kuhamasishwa ili kujikwamua kutoka katika lindi la umaskini, kwanza kwa kuanzisha vikundi vya kuweka na kukopa (VSLs) na kufundishwa uzalishaji mali kwa ajili ya kujiongezea kipato (IGAs).

Ilisema mradi huo ulitekelezwa katika wilaya nane ambazo kwa upande wa Unguja ni Wilaya ya Kusini, Wilaya ya Kati, Kaskazini A na Kaskazini B, Pemba mradi wa WEZA II ulifanya kazi katika Wilaya za Wete, mkoani Chakechake na Micheweni.

Aidha, Tamwa Zanzibar imevihamasisha vikundi 24 vya kuweka na kukopa Unguja na Pemba kuanzisha miradi maalum ya kujiongezea kipato na kuvigawa vikundi hivyo katika kongano (clusters) nne za uzalishaji ambazo ni za wazalishaji wa vipodozi, mikoba, mboga na ufugaji wa kuku.

Kwa ujumla kuna kongano nane, nne Unguja na nne Pemba, vikundi hivyo tayari vimeshasajiliwa na pia vimepata vibali vya biashara na uzalishaji wa bidhaa kutoka mamlaka husika kama vile Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali (BPRA) na Wakala wa Chakula na Dawa (ZFDA), ilisema taarifa ya Tamwa.

"Katika ufuatiliaji wa harakati za wanawake kujikwamua kiuchumi, Tamwa Zanzibar, imegundua kuwa wanawake wengi hususan wa vijijini hawana mitaji ya kuwawezesha kufanya biashara wala kufanya shughuli za kilimo chenye tija, hivyo wanahitaji kusaidiwa kwa kupewa mikopo, ujuzi na vitendea kazi," ilisema taarifa.

Kadhalika, wajasiriamali wadogo hupata shida kupata masoko ya bidhaa zao kwa sababu nyenzo zao za kujitangaza ni finyu. Mathalan hushindwa hata kushiriki katika maonyesho ya biashara kwa sababu hawawezi kulipia mabanda kwani banda hukodiwa kwa Sh. 200,000, alieleza Makame katika taarifa yake.

"Hivyo tunawashauri waandaaji wa maonyesho wawafikirie wazalishaji wadogo kwa kuwapunguzia gharama za kukodi mabanda," aliongeza.

Wakati mradi wa WEZA II ukimalizika, hivi sasa Tamwa Zanzibar kwa kushirikiana na (MZF), inasimamia mwendelezo wa mpango huo wa uwezeshaji wa wanawake kiuchumi katika mpango unaoitwa WEZA III ambao umejikita katika kuwaongezea uwezo wazalishaji kwa kuwapa mbinu za kujitegemea.

Walengwa wa mradi huo wako kwenye shehia 11 za Unguja Kaskazini A, Kusini na Magharibi na kwa upande wa Pemba Shehia 11 za Wete, Micheweni na Mkoani.



Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, Benjamin Sitta (katikati), akipokea maelezo kutoka kwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Bongoyo, Aloyce Benjamin, kuhusu ukarabati ulioratibiwa na mwalimu wa shule hiyo, Badru Musoke (kushoto). Kulia ni Mwalimu Majera Munyaga. **MPIGAPICHA WETU**

# Wazee watengewa mamilioni ya tiba

**Na Marco Maduhu, KISHAPU**

HALMASHAURI wilayani Kishapu Mkoa wa Shinyanga, imetenga Sh. milioni 3.5 kwa ajili ya kutengeneza vitambulisho vya matibabu ya wazee yatakayotolewa bure.

Kishapu ana takribani wazee 15,462, lakini walio na vitambulisho vya matibabu hayo ni 12,148 wakati 3,314 hawana.

Kukosa vitambulisho hivyo huwasababishia kukosa huduma kwa vile wengi hawana fedha.

Hayo yalibainishwa na Ofisa Maendeleo wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu Joseph Swalala, kwenye kikao cha Shirika la Tawlae linalotetea haki za wazee mkoani Shinyanga, wakati likitambulisha mradi wa kuhamasisha halmashauri hiyo kuingiza masuala ya wazee kwenye mipango yao.

Alisema halmashauri hiyo imejitahidi kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wazee hasa kwa upande wa matibabu, ambapo kwa mwaka wa fedha (2019-20) zimetengwa Sh. milioni 3.5.

"Halmashauri ya Kishapu katika bajeti ya mwaka wa fedha (2019-20) kupitia mapato ya ndani, tumetenga fedha hizo kutatua changamoto mbalimbali za wazee ikiwamo kuwapatia vitambulisho, ili kuwaondolea adha ya kukosa matibabu," alisema Swalala.

Mwenyekiti wa Baraza la Wazee Kishapu Suzana Masebu, alisema wazee wilayani humo wamekuwa wakikabiliwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa matibabu hasa wale ambao hawana vitambulisho.

Alieleza kuwa wengine wametelekezwa na watoto wao na hivyo kukosa pesa za matibabu. Nao baadhi ya wazee hao akiwamo Edward Kasapa, walisema licha ya kupewa vitambulisho hivyo vya matibabu bure, lakini wanapokwenda hospitalini mara nyingi huambiwa hakuna dawa ili wakanunue na kuiomba serikali ilitatue tatizo hilo la ukosefu wa dawa kwa wazee.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya Nyabaganga Taraba, aliwatoa wasiwasi wazee hao kuwa changamoto zote ambazo wanakabiliwa nazo serikali itazitatua, ambapo kwa sasa wameshatenga madirisha ya wazee kwenye huduma za afya wilayani humo na kueleza kuwa suala la dawa nalo litakwisha.

Aidha, Mratibu wa Shirika la Tawlae linalotetea haki za wazee mkoani Shinyanga, Eliasenya Nnko, alisema mradi wao huo utakaodumu kwa mwaka mmoja umelenga kuhamasisha halmashauri kutenga bajeti za kutatua changamoto za wazee hasa upande wa matibabu.

# 'Wazalishaji, mashirika ya udhibiti shirikianeni'

**Na Felix Andrew**

MASHIRIKA ya Viwango (TBS) na la Kuendeleza Viwanda Vidogo (Sido), yametakiwa kushirikiana na wajasiriamali ili kuwapata maeneo bora ya kuzalishia bidhaa zao zikiwamo karakana za Sido.

Wito huo ulitolewa jana mkoani Simiyu na Waziri wa Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu, Jenister Mhagama, alipotembelea banda la TBS.

Alifanya ziara hiyo wakati wa kilele cha maonyesho ya tatu ya mifuko ya uwezeshaji programu na vikundi vya kifedha yaliyoandaliwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC).

Mhagama alitoa wito huo kufuatia maelezo ya ofisa waTBS Roida Andusamile, kuwa wajasiriamali wengi wanashindwa kuthibitisha ubora wa bidhaa wanazozizalisha kutokana na kutokuwa na majengo bora ya kuzizalishia.

"TBS mnapaswa kushirikiana na SIDO ili kuwawezesha wajasiriamali kuzalisha kwenye karakana za Sido na hatimaye waweze kuzalisha kwa viwango na kuthibitisha ubora wa bidhaa hizo," alisisitiza Mhagama.

Akizungumza na washiriki wa maonyesho hayo, Waziri Mhagama, aliitaka mifuko inayotoa mikopo kwa wajasiriamali kuongeza kasi ya utoaji wake ili iweze kufikia wajasiriamali wengi nchini.

Mhagama, alisema utoaji huo wa mikopo uwe na riba nafuu ili wajasiriamali wengi wanufaike nayo na amelitaka baraza hilo kusimamia mifuko ya uwezeshaji kuendelea kujitambulisha na kujitangaza kwa wananchi kupitia programu mbalimbali.

Mtendaji Mkuu wa NEEC, Beng Issa, aliwataka wananchi wa Simiyu kuchangamkia fursa zilizotolewa katika maonyesho haya kwani uwepo wake haya utaibua chachu ya maendeleo kwa wananchi wa Simiyu.

Alisema maonyesho hayo pia yanakutanisha wajasiriamali na taasisi za serikali lengo likiwa ni kuwawezesha kurasimisha biashara zao na kuhamasisha matumizi ya mifuko ya ya kijamii pamoja na mtandao kwa wajasiriamali.

Katika maonyesho hayo TBS iliwatembelea wajasiriamali 60 wanaozalisha bidhaa mbalimbali na kuwapatia utaratibu ili waweze kusajili majengo wanayozalishia, bidhaa na kuthibitisha ubora wake.

Pia, wananchi waliotembelea banda la TBS walielimishwa umuhimu wa kutumia bidhaa zilizothibitishwa ubora na TBS na kuangalia muda wa matumizi wa bidhaa wanazozinunua badala ya kuangalia bei.

## RC awafagilia DC, DED utendaji

**Na Allan Isack, ARUSHA**

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, amesema ameridhishwa na utendaji kazi wa Mkuu wa Wilaya ya Kiteto, Tumaini Magessa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, kwa usimamizi mzuri wa miradi ya maendeleo.

Mnyeti alitoa pongezi hizo wakati akizungumza na wananchi wa mji mdogo wa Kibaya kwenye ziara yake ya kikazi ya siku tano wilayani humo.

Alisema Magessa ni mchapakazi mzuri akishirikiana na Mkurugenzi wake, Tamim Kambona, hivyo amewaomba wananchi wa Kiteto kutoa ushirikiano kwa viongozi hao ili kufikia malengo ya kuihudumia jamii.

Hata hivyo, alisema kuna baadhi ya wananchi wamekuwa wakimlalamikia mkuu huyo wa wilaya kutokana na misimamo yake ya kupinga mambo ambayo siyo mazuri kwenye jamii.

"Napenda kuwakumbusha wananchi kuwa viongozi hawa ni wachapakazi kazi na wamefanya mambo makubwa kwenye wilaya hii nyie mkiona hawafai maeneo mengine wanatamani wawe viongozi wao," alisema Mnyeti.

"Pamoja na changamoto zilizopo Kiteto kama ningekuwa natoa maksi za utendaji kazi basi viongozi hawa ningewapa asilimia 95, kati ya asilimia 100, kutokana na kazi hii waliyofanya kwa kipindi kifupi kwenye wilaya hii," aliongeza Mnyeti.

Alisema ubora wa viongozi hao, umetokana na usimamizi mzuri wa miradi ya maendeleo, hivyo wanapaswa kupongezwa kwa jitihada zao.

Mnyeti alisema viongozi wengine wa wilaya na halmashauri zilizopo katika mkoa wa Manyara wanapaswa kuiga mfano kutoka kwenye wilaya ya Kiteto ili kufikia malengo ya kuwahudumia wananchi.

"Ukifika kwenye wilaya hii utaona miradi ilivyotokelezwa kwa ubora na kiwango cha juu, na miradi yote imetekeleza kwa fedha kidogo," alisema Mnyeti.

"Wakuu wa wilaya na wakurugenzi wengine waliopo katika mkoa wa Manyara wanapaswa kuiga mambo mazuri yaliyofanywa na Wilaya ya Kiteto ," alisema Mnyeti.

Mkuu wa Wilaya ya Kiteto, Mhandisi Magessa, alishukuru pongezi hizo kutoka kwa Mkuu wa Mkoa na aliahidi kuwa wilaya hiyo haitarudi nyuma katika usimamizi wa miradi ya maendeleo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, Kambona, alisema lengo la halmashauri hiyo ni kuhakikisha wanasimamia miradi ya maendeleo ipasavyo ili iweze kuwanufaisha mwananchi husan maeneo ya vijijini.

# Japan yaridhishwa ujenzi wa madarasa

**Na Allan Isack, ARUSHA**

UBALOZI wa Japan nchini, umeridhishwa na utekelezaji wa ujenzi wa mradi wa vyumba vya madarasa uliofadhili katika Shule ya Sekondari Sokon II, Halmashauri ya Arusha DC wilayani Arumeru.

Akizungumza na Nipashe wakati alipotembelea kukagua mradi huo, Mratibu wa Miradi wa ubalozi huo nchini, Ayumi Kasai, alisema ameridhishwa na utekelezaji wa ujenzi wa vyumba vya madarasa kwani yamekidhi viwango.

Ayumi alisema ujenzi huo ulianza Mei mwaka huu, na hadi sasa umekamilika kwa zaidi ya asilimia 55, jambo ambalo linatia moyo na kuleta matumaini ya kukamilika kwa wakati kulingana na mkataba wa ujenzi.

Aliupongeza uongozi wa halmashauri hiyo kwa usimamizi imara wa miradi.

Alisema Japan imejipanga kufadhili miradi mingine katika halmashauri hiyo.

Ofisa Elimu Taaluma wa halmashauri hiyo, John Charles, alisema halmashauri inathamini mchango mkubwa uliotolewa na Japan, kwa kusapoti sekta ya elimu, ambayo ni nyeti kwa manufaa ya taifa na vizazi vijavyo.

Aidha, alisema halmashauri itahakikisha mradi huo unakamilika kwa wakati, na madarasa hayo yataanza kutumika haraka, kwa ajili ya kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani unatokana na uhaba wa vyumba vya madarasa.

"Nikuhakikishie kuwa ujenzi huu utakamilika kwa wakati, na wanafunzi wataanza kuyatumia madarasa hayo ndani ya mwaka huu, kwa ajili ya kupunguza msongamano wa wanafunzi uliopo," alisema Charles.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Sokon II, Mwamvita Kilonzo, alisema, vyumba hivyo vya madarasa vitachukua jumla ya wanafunzi 180, kwa uwiano wa wanafunzi 45, kwa kila darasa moja.

Aliongeza kuwa, Shule ya Sokoni II, ina vyumba 11, vya madarasa ikiwa na uhitaji wa zaidi ya vyumba 11, kwa idadi ya wanafunzi 993, waliopo.

Japan ilitoa Sh. milioni 195, kwa ajili ya ujenzi wa msingi wa ghorofa, kukamilisha vyumba vinne vya madarasa, ujenzi wa vyoo vya wanafunzi pamoja na kuweka samani kwenye madarasa hayo.



Mtoto Mary Lyimo (4) wa Mji Mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, akijiandaa kupatiwa chanjo ya surua na rubella ambapo watoto 272,633 chini ya miaka mitano wa mkoa huo wamepatiwa chanjo hiyo jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Ushauri wazazi kubana watoto mitandao kijamii

**Na Allan Isack, ARUSHA**

WAZAZI na walezi , wametakiwa kuwasimamia watoto katika malezi mazuri ili kuwaepusha na matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Shule ya Star High Kata ya Mbuguni wilayani Arumeru, Sister Monica Massawe, katika mahafali ya 10, ya shule hiyo.

Sister Massawe alisema mitandao ya kijamii ni mizuri endapo itatumika vizuri, ikiwamo kutafuta kazi na nafasi za masomo ila ikitumika vibaya inaweza kuwapotosha vijana.

Alisema mitandao ya kijamii inapotumika vibaya haiwezi kuwa na tija katika jamii na taifa, hivyo wazazi na walezi nchini wanapaswa kuwa makini katika kufuatilia suala hilo.

"Wazazi na walezi wa watoto nchini wanapaswa kuchukua tahadhari kwa kufuatilia maisha ya watoto wanavyoishi pamoja na makuzi yao tangu wakiwa wadogo hadi kufikia mtu mzima anayejitambua," alisema Sister Massawe.

Hata hivyo, alisema kwa mwaka huu wanafunzi 92, walihitimu elimu ya sekondari kidato cha nne wakiwamo wasichana 31 na wavulana 61.

"Tunamshukuru Mungu kwa kufanikisha miaka 10, ya shule yetu tumeweza kuwalea wanafunzi kwa kuwafundisha taaluma bora na maadili mema," aliongeza.

Sabrina Jumbe, mmoja kati ya wahitimu wa kidato cha nne, alisema matarajio yake ni kufaulu mtihani wake wa kidato cha nne ili aendelee na sekondari kwa kidato cha tano na sita.

"Malengo yangu ni kuwa daktari ili niwasaidie wagonjwa nitakapomaliza elimu ya kidato cha sita na chuo, ninapenda mno kazi ya kuwatibu watu nina wito nayo kutoka moyoni," alisema Jumbe.

Mhitimu mwingine, Mary Matiku, alisema wanamshukuru Mungu kwa kuhitimu na anatarajia kufaulu na kuendelea na elimu ya kidato cha sita.

Naye Allen Stephen, aliwashukuru walimu na wanafunzi wa shule hiyo kwa ushirikiano mkubwa waliyompatia kwa kipindi cha miaka minne walipokuwa wakisoma shuleni hapo.

# Bodi yafurahishwa ujio wa ATM maziwa

**Na Mwandishi Wetu, MOSHI**

KAIMU Msajili wa Bodi za Maziwa Nchini, Sofia Mlote, ameeleza kufurahishwa na ujio wa teknolojia mpya ya ununuzi wa maziwa kwa njia ya mashine za ATM.

Mlote alisema ujio wa mashine hizo utarahisisha wananchi wa Kilimanjaro kunywa kiwango sahihi cha maziwa ambacho ni lita 200 kwa mwaka kwa mtu.

Alieleza imani yake hiyo jana, wakati wa mahojiano na Nipashe kuhusu teknolojia mpya mashine za ATM za maziwa ambazo zimewekwa katika wilaya za Hai na Manispaa ya Moshi.

Alisema kwa sasa Mtanzania anakunywa lita 49 za maziwa kwa mwaka, wakati anatakiwa kunywa lita 200.

Alisema kazi ya bodi ni kusimamia sheria na kanuni za uzalishaji wa maziwa pamoja na wadau wanaozalisha chakula hicho nchini na kwamba uzalishaji ni lita bilioni 2.7 kutoka ng'ombe wa maziwa milioni 1.294.

Alisema kutokana na uzalishaji huo, asilimia 10 ndizo zinazokwenda kwenye mfumo rasmi za usindikaji wa maziwa na kwamba asilimia 90 inaenda kwenye mifumo isiyo rasmi.

Alisema usindikaji ni lita 154,000, lakini mikakati ni kusindika zaidi ya lita 815,000 za maziwa, na kwamba bado uhitaji upo kwa kuwa maziwa yanayoingizwa nchini kwa mwaka ni lita milioni 20.

"Kunatakiwa nguvu ya pamoja ya kuundwa kwa vikundi vya ushirika ili kuweza kutetea na kusimamia kinachoaminiwa na wadau wa tasnia ya maziwa ili kuweza kufikia mbali," alisema.

Aidha, alisema kila mwanachama wa ushirika lazima awe na shamba la malisho, ili kuwapa mifugo chakula bora pamoja na kupata maziwa salama yakutosha.

Kutokana na mafanikio hayo, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, aliwataka maofisa ugani kuwafikia wazalishaji walipo ili waweza kupata mbegu bora za ng'ombe zinzaozalisha maziwa yaliyo bora.

Alisema sambamba na upatikanaji wa maziwa, pia wafugaji wahamasishwe kunywa maziwa na si kuuza yote kama walivyozoea.

Mkurugenzi wa Match Maker, Peniel Uliwa, alisema, mradi huo wa Faida Maziwa umefadhilia na Shirika la Maendeleo ya Uholazi (SNV) kupitia Match Maker Associate, ambao umewapatia vikundi mashine za kuchakata chakula cha mifugo pamoja na teknolojia mpya na ya kwanza hapa nchini ya milk ATM.

Alisema mitambo hiyo inabeba lita 300 na kwamba ATM inagharimu Sh. milioni 19 na zimepatiwa kwa mikundi viwili vya vijana ambao ndiyo watakaosimamia mradi huo.

# Kijiji charejesha ardhi iliyoporwa

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

WANAKIJIJI 16 wa Kiterini wa Wilaya ya Moshi wamegeuka mashujaa na kusherehekea ushindi baada ya kurejesha ardhi ya mwanakijiji mwenzao iliyoporwa kwa zaidi ya miaka 16 iliyopita.

Mashujaa hao walipigania haki ya jirani yao Benjamin Thomas (68), aliyekuwa amepokwa eneo lake la makazi na kilimo lenye ukubwa wa ekari moja.

Thomas asiyejiweza alipokwa ardhi hiyo tangu mwaka 2013 na mtu aliyedai amemuuzia shamba hilo, aitwaye Peter Jerald.

Akizungumza jana, baada ya Mahakama ya Ardhi ya Wilaya ya Moshi, kumpa ushindi katika kesi namba 164 ya mwaka 2018, Benjamin alisema anaishukuru jamii ya watu wa Kiterini kwa kumpa moyo wa kujitokeza kutoa ushahidi katika Baraza la Ardhi la Kijiji, Kata na Mahakama ya Ardhi ya Wilaya ambako kote alipata ushindi.

"Eneo nililopokwa, liliuzwa kinyemela na jirani yangu ambaye alishirikiana na mlalamikaji, nilifukuzwa kwenye shamba langu mwaka 2013 na 2014 tukaanza kusumbuana kila siku na akaniambia nisiruke shambani. Kwa kuwa sina nguvu wala uwezo nikaondoka, lakini majirani zangu walijitokeza na kunipigania hadi kupata haki yangu Septemba 30 mwaka huu katika Mahakama ya Ardhi ya Wilaya ya Moshi," alisema Thomas.

Akizungumzia mchakato mzima hadi kupatikana kwa haki hiyo, Msaidizi wa Kisheria wa Kata ya Kilema Kusini anayefanya kazi na Shirika la kiraia la Kwieco, Getrude Terry, alisema baada ya kufika katika kikundi cha amani na upendo kilichopo Kijiji cha Chereni na kujitambulisha kazi yake, ndipo alipoelezwa mkasa huo na kuamua kuchukua hatua za kumshauri na kufungua kesi ngazi ya kijiji na kata.

"Kwanza niliomba nionane na Thomas na nilipokutana nae alinieleza hali halisi ya mgogoro wa shamba, nikaenda kulionana na nikamshauri kama ilivyo ada kwetu kushauri mteja kwamba sehemu stahiki ya kupata haki ni baraza la ardhi la kijiji, aliridhia na tulikwenda, kesi ikaunguruma na alipata ushindi.

"Lakini mlalamikiwa hakuridhika kesi iliendelea baraza la ardhi la kata na alishinda tena, mlalamikiwa hakuridhika akakata rufani kwenda Mahakama ya Ardhi ya Wilaya, baada ya kupokea wito huo tuliongozana na Thomas hadi ya mwisho na wiki iliyopita alipata tena ushindi kwamba yeye ni mmiliki halali wa eneo hilo na akarudishiwa shamba lake." Alisema Terry.

Alipoulizwa nini hatima ya ushindi, Terry alisema, "Hatujaishia hapo, kwa sababu Thomas ameshapata shamba lake, sio kwamba ndiyo mwisho wa safari yetu kama wasaidizi wa kisheria, tuna nafasi ya kumshauri apate hati miliki ya eneo lake Idara ya Ardhi ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi ili asitokee tena mtu mwingine kumsumbua, "alisema Terry.

Mkazi wa Kiterini, Wilson Myombe, akitoa ushuhuda kuhusu mgogoro huo, alisema sehemu ambayo Thomas alikuwa amemuuzia mlalamikiwa ni ekari moja na hiyo ekari moja na robo nyingine iliyokuwa imebakia anaimiliki.

"Sisi majirani tuliingilia kati na kukubali kuwa mashahidi wake katika kila ngazi ya mashauriano au mahakama ili apate haki yake. Wanamdhulumu kwa sababu hana nguvu, yeye ni mnyonge na sisi tukasema tutamsaidia kupambania haki yake. Sisi majirani wote tuliomzunguka tunathibitisha kwamba eneo hili ni mali yake," alieleza Myombe.



Mkazi wa Jiji la Dar es Salaam akiwa amejitwisha mzigo mkubwa kichwani, kwa ajili ya kujipatia ujira wa siku katika Barabara ya Uhuru, eneo la Kariakoo, jijini humo jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Walalamikia uchaguzi wa mitaa

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

BAADHI ya wanawake mashuhuri na wenye ushawishi katika jamii mkoani Kilimanjaro, wamevunja ukimya, wakidai rushwa ya ngono ni kikwazo kwa wanawake wanaogombea nafasi za uongozi kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa.

Uchaguzi huo unaotarajiwa kufanyika mwezi ujao Novemba 24, unaelezwa kuwa umegubikwa na kashfa ya ngono na kuwa moja ya vikwazo vinavyowavuruga wenye nia ya kugombea.

Akizungumza jana, wakati wa mafunzo ya uongozi, demokrasia na utawala bora kwa wanawake, Mweka Hazina wa Chama cha Watu Wenye Ulemavu mkoani Kilimanjaro (Chawata), Rabia Mshana, alisema wanawake wasikate tamaa.

Aliwataka wagombee nafasi mbalimbali za uongozi hata kama wanaungwa mkono na wachache.

"Changamoto kubwa ambayo inatukabili sana sisi wanawake ni mazingira ya kuombwa rushwa ya ngono na viongozi au baadhi ya wananchi ili upigiwe kura. Hao wanaoomba kugombea hasa wanawake wanashawishiwa sana kwenye ngono ili wapitishwe na wapate kura."

Mafunzo hayo yaliandaliwa na Shirika la kiraia la Kwieco, kwa ufadhili wa Women Fund Tanzania (WFT).

Mwenyekiti wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi Manispaa ya Moshi, Joyce Ndosi, aliwataka wanawake kuungana na kushirikiana.

Aidha, Katibu wa Jukwaa la Wanawake Manispaa ya Moshi, Consolatha Lyimo, aliwataka waamke anaposimama mwanamama wasidharauliane wala kuumizana majukwaani na wasikwamishane kwa sababu ambazo hazina mantiki.

"Tushikamane wakati mwanamke kasimama, hata kama wanaume hawatamchagua, lakini kwa wingi wetu tunaweza kushinda kama tukimpigia kura," alisema Lyimo.

Nipashe
# TESA
Jumanne Oktoba 22, 2019
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

Ukurasa 15



## Ziba; Ni sekondari ya kata inayozifunika shule kongwe

Ukurasa 18



## JE, WAJUA?

Shule za kurekebisha tabia zatesa watu kama wanyama



Ukurasa 19

## Mtu anajulikana kwa jina au kwa majina?




# Siri shule zilizoingia 10 bora kitaifa kutoka Shinyanga

Ukurasa 16

## ELIMU KUTOKA POLISI

# Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Mwenyekiti wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama aongoza Kamati ya Ulinzi na Usalama Taifa kukagua vipenyo salama na visivyo salama katika mpaka wa Tanzania na Msumbiji



Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Mwenyekiti wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama (CDF), Jenerali Venance Mabeyo (wapili kulia), akiangalia eneo la kumbukizi ya shujaa UD 5826 L/CPL Ahamad Mzee, alipoangushia ndege mbili za Ureno. Aprili 1972. **PICHA ZOTE: JESHI LA POLISI**





Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini (IGP) Simon Sirro (aliyenyosha mkono), akiongea na wananchi wa Kijiji cha Kitaya baada ya kutoka kutembelea eneo la kumbukizi ya shujaa UD 5826 L/CPL Ahamad Mzee. Msafara huo umeongozwa na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Mwenyekiti wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama (CDF), Jenerali Venance Mabeyo (kulia kwa IGP).



## TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**

marobarnabas@yahoo.com

# Akili nyingi huondoa maarifa

KUJITIA werevu mwingi huweza kuondoa busara aliyo nayo mtu akaishia kuyaharibu ayafanyayo.

Methali hii huweza kutumiwa kumkanya mtu anayepuuza ushauri anaopewa kwa kujiona ana akili kuliko wengine.

Kumbe ndio maana wahenga walisema “Akili ya mtu ndiyo wazimu wake.” Kwamba akili ya mtu yaweza kuwa wazimu wake pia. Methali hii yatumiwa kuelezea kuwa akili ya binadamu yaweza kuzua mema na mabaya pia.

Kama Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) halitokuwa makini, tusishangae tukipitwa na Kenya. Yapo maneno kadhaa ya Kiswahili fasaha* na sanifu* yasiyotumika Tanzania lakini yanatumiwa ipasavyo nchini Kenya.

*Fasaha ni –enye matamshi safi ya maneno; -enye usahihi wa matumizi ya maneno: Kiswahili fasaha.

*Sanifu ni kitendo cha kutunga kitu kwa ufundi ili kivutie; kitendo cha kuchora ramani ya kitu kitakachotengenezwa kama vile jengo. Pia –enye kufuata vigezo vilivyokubaliwa.

Wakati Kenya wakiwa na baadhi ya maneno sahihi ya Kiswahili, sisi wenyewe twazungumza na kuandika maneno yasiyo Kiswahili au yenye maana tofauti!

Tuanze na neno ‘muhanga/mhanga.’ Neno hili maana yake ni mtu anayejitolea nafsi yake kwa kujiingiza au kufanya jambo linalosababisha kifo chake. Kifo cha mtu anayejitoa muhanga/mhanga sio cha bahati mbaya, ni cha kupangwa na chenye dhamira maalumu.

Kwa hiyo watu wanaokufa kutokana na majanga kama vita, moto, zilizala (tetemeko la ardhi), mafuriko, ajali za barabarani, angani au baharini, si sahihi kuwaita ‘wahanga’, kwani hawa ni waathiriwa wa matokeo hayo.

Ng’ombe, mbuzi na kuku au hata binadamu huweza kuwa wahanga wanapochinjwa au kuuawa kwa imani ya kuzuia au kupata jambo fulani, mathalan utajiri.

Wanaojitoa muhanga ni wale wanaojivisha mabomu na kwenda kuyalipua katikati ya kundi au makundi ya watu wakiwa na madai ya kisiasa au kidini.

Pia muhanga ni mtu anayejitosa mtoni au baharini ili kumwokoa mtu aliyezama au anayeingia katika nyumba inayoungua ili kuwaokoa watu waliomo ndani. Watu wa aina hiyo ndio wahanga.

Hukereka sana nisikiapo watangazaji wakisoma taarifa za habari au waandishi wa magazeti kuandika: “wahanga waliokufa kwenye ajali ya treni, ndege, gari au meli ni …”

Kandarasi ni mkataba wa kufanya kazi kama ujenzi wa majengo, barabara, madaraja n.k. Pia kazi inayofanywa kwa makubaliano ya pande mbili kwa malipo na muda maalumu. Hivyo kampuni moja huitwa mkandarasi. Nyingi huitwa wakandarasi sio makandarasi kama ilivyozoeleka!

‘Lakini’ ni tamko la kuonesha kasoro ya jambo; uwepo wa upungufu au hitilafu. Mfano: Nilitaka kwenda mpirani ‘lakini’ nimeghairi. Ilikuwa nisafiri leo ‘lakini’ nimeahirisha. Pamoja na ufafanuzi huu, utamsikia waziri akisema, kwa mfano: “Serikali imejenga hospitali ya mkoa ‘lakini’ pia imejenga daraja. ” Msemaji angesema: “Serikali imejenga hospitali ya mkoa na daraja.”

Siku hizi watu hukosea sana wanapoomba msaada au kitu kutoka serikalini au kwa watu wengine. Utamsikia mtu anasema “nilikuwa naomba …”

Isemwapo ‘nilikuwa’ maana yake ni wakati uliopita. Mfano: “Jana tulipokutana nilikuwa natoka hospitali” au “nilikuwa nakwenda kuwasalimu wazee.”

Huwezi kuomba kitu kwa wakati uliopo kisha ukasema ‘nilikuwa naomba.’ Isemwapo hivyo maana yake shida yako ilikuwa wakati ule si sasa.

‘Athari’ ni neno lenye maana tatu: i) taathira, yaani alama au hisia inayobaki kwa muda kutokana na kutokea jambo fulani; kasoro au dosari kwenye kitu; hali ya kuambukizwa mtu tabia au mazoea yake.

2) Ukosefu wa kimaumbile wa ukamilifu wa kitu na 3) athari, masalio ya ukumbusho wa utamaduni wa watu kama vile magofu* (masalio ya majengo yaliyobomoka).

*Magofu ni mchezo wa kuingiza mpira mdogo kwenye kishimo maalumu, baada ya kurushwa kwa kupigwa kwa gongo maalumu; mpira unaotumiwa kwenye mchezo huo. ‘Wasilisha’ na ‘wakilisha’. Haya ni maneno yanayowakanganya (kitendo cha kusababisha mtu kuemewa/babaika); kutofahamu jambo vizuri.

‘Wasili’ ni kitenzi sielekezi (kitenzi kisichofuatwa na nomino kisichochukua yambwa yaani nomino au kundi nomino ambayo inaathiriwa na kitenzi katika sentensi; kitendwa.) ‘Wasili’ ni fika mahali ulipotarajia baada ya safari.

‘Wasiliana’ (kitenzi sielekezi) ni peleka na pokea taarifa kutoka kwa mtu au watu. Maana ya ‘wasilisha’ (kitenzi elekezi) ni fikisha kitu au ujumbe ulipohitajiwa; toa maelezo au mhadhara kwa kikundi cha watu au mbele ya watu.

‘Wakili’ ni mwanasheria anayemtetea mtu katika kesi. ‘Wakilisha’ ni kitendo cha kufanya jambo kwa niaba ya mtu mwingine. Neno hili pia lina maana ya kuonesha seti ya thamani kwa kutumia michoro au grafu.

**Methali: Upishi ni kuni.**

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

UCHAMBUZI

NA SANULA ATHANAS, IGUNGA

# Ziba; Ni sekondari ya kata inayozifunika shule kongwe

IKO umbali wa kilometa 57 Magharibi mwa Mji wa Igunga. Ni shule ambayo sasa inatoa mwanga mpya wa elimu wilayani Igunga mkoani Tabora ikishika nafasi ya kwanza kiwilaya kwa shule za serikali katika mitihani ya taifa ya kidato cha nne kwa miaka minne mfululizo.

Si nyingine bali ni Shule ya Sekondari Ziba ambayo sasa ina jumla ya wanafunzi 914 (wavulana 317) na walimu 18 (wanawake wanane).

Katika matokeo ya mtihani wa taifa wa kidato cha nne mwaka jana, shule hiyo ya Kata ya Ziba iliyoanzishwa mwaka 2000, ilishika nafasi ya kwanza kwa shule za serikali wilayani Igunga, ikitoa mwanafunzi aliyepata daraja la kwanza kwa alama nane.

Kiwango hicho cha ufaulu wa mwanafunzi huyo kilikuwa cha juu kuzidi wanafunzi wote wa baadhi ya shule kongwe mkoani Tabora, zikiwamo Nanga na Igunga (zote za Igunga) na Tabora Girls iliyoko mjini Tabora.

Kwa mujibu wa Makamu Mkuu wa Shule ya Sekondari Ziba, Mwalimu Frank Milazi, kati ya wanafunzi 63 waliofaulu kwa daraja la kwanza hadi la tatu katika mtihani huo, 41 walichaguliwa kujiunga kidato cha tano, 21 walichaguliwa kujiunga na vyuo mbalimbali vya serikali na mmoja hakuchaguliwa.

### SABABU 5 ZA UFAULU

Mwalimu Milazi anabainisha mambo matano yaliyochagiza mafanikio ya shule hiyo kitaaluma, akieleza kuwa jambo la kwanza ni mshikamano wa walimu kuhakikisha wanakamilisha mapema mada za kila somo.

"Mafanikio haya tumeyasaka kwa muda mrefu sana. Yalianza kuonekana mwaka 2015. Walimu tulishikamana kuhakikisha 'topics' (mada) zinamalizika mapema," anasema na kuongeza:

"Tulipofanikiwa katika hilo, tukaanzisha utaratibu wa mitihani maalum, inayofanyika kuanzia saa 12:30 asubuhi. Kutokana na kufanya mitihani mingi, wanafunzi wakajiamini, mtihani wa taifa wanauona wa kawaida tu, hawana woga tena."

Milazi anataja jambo la pili ni ile la kuhakikisha hakuna utoro.

Kwamba wanafunzi wote waliokuwa wanasuasua kuja shuleni waliwafuatilia na kuwabana.

Mwalimu Milazi anasema ufaulu huo pia umechagizwa na kujengwa kwa hosteli katika shule hiyo, akieleza kuwa wanafunzi wengi, hasa wa kike, sasa wanasoma kwa utulivu wakiwa shuleni muda wote.

"Hosteli pia zimesaidia kutatua changamoto ya mimba kwa watoto wetu...mwaka huu hatuna tukio la aina hiyo hapa kwetu," anasema.



Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwamri. **PICHA: MTANDAO**

> Pia, hatuna nyumba za walimu za kutosha. Tuna nyumba tatu tu, hivyo walimu 15 hawaishi karibu na maeneo ya shule, wanaishi huko mitaani wamepanga.

Kiongozi huyo wa shule anaeleza zaidi kuwa uamuzi wa Mbunge wa Manonga, Seif Gulamali (CCM), kuwalipia ada wanafunzi wote wa jimbo hilo wanaofaulu kujiunga na kidato cha tano na sita, pia umechagiza kupaa kwa ufaulu shuleni hapo.

"Kwa kweli, tunamshukuru Mheshimiwa Gulamali, ahadi yake imechochea sana ufaulu maana wanafunzi wengi wamehamasika kusoma kwa sababu sasa wana uhakika wa kulipiwa ada kidato cha tano na sita," anasema na kuongeza:

"Mbunge pia amechangia kupanda kwa ufaulu wa wanafunzi kutokana na kuanzisha mashindano ya michezo kwa shule za sekondari kwenye jimbo hili."

### MWANAFUNZI

Hoja hiyo inaungwa mkono na Mwajuma Luchembele, mwanafunzi wa kidato ca nne katika shule hiyo ambaye anasema wanafunzi wengi sasa wanasoma kwa bidii kwa kuwa wana uhakika wa kulipiwa ada na mbunge kidato cha tano na sita.

"Mbunge wetu amejitoa sana, amefanya kazi kubwa kusomesha wanafunzi wanaofaulu kwa kupata daraja la kwanza hadi la tatu. Kwa kweli, ametuhamasisha kusoma kwa bidii zaidi na amesaidia sana Ziba kuwa na kidato cha tano na sita," anasema Mwajuma na kuongeza:

"Pia ninamshukuru Mkuu wa Shule aliyepita, Madam Pendo, kwa mipango yake iliyoipa sifa kubwa shule hii. Kwa kweli tutakumbuka sana."

### MBUNGE ANENA

Gulamali anasema aliamua kuchukua uamuzi wa kulipa ada kwa wanafunzi wote wa jimbo hilo wanaofaulu kujiunga na kidato cha tano mwaka 2016, baada ya kubaini baadhi ya wanafunzi hukosa fursa ya kuendelea na masomo kutokana na kukosa ada.

"Nilikuwa ziarani jimboni. Nilipofika Choma, nilikutana na kijana ambaye ni mwanafunzi lakini hakuwa shuleni... nilipomuuliza, alinijibu kuwa alilazimika kukaa nyumbani kutokana na kukosa ada," anasema na kuongeza:

"Nilipofuatilia kwa undani, nikabaini wapo vijana wengi wanaoshindwa kuendelea na masomo kutokana na kukosa ada, nikaona kuna haja ya kuwalipia wote wanaofaulu katika jimbo langu."

Anabainisha kuwa mwaka 2017 wakati anaanza kutekeleza uamuzi wake huo, alianza kwa kuwalipia ada wanafunzi 77, mwaka jana wanafunzi 163 na mwaka huu wanafunzi 245.

"Changamoto katika utekelezaji wa suala hili ni kutokuwa na uhakika wa bajeti maana unakuwa hujui kutakuwa na idadi ya wanafunzi wangapi na inaongezeka kila mwaka," anasema na kuongeza:

"Unatenga bajeti ya wanafunzi 100, lakini unajikuta una wanafunzi 200 wameongezeka na inabidi utekeleze kwa sababu umeshaamua kuwasaidia na umeshawaahidi."

Gulamali anaongeza kuwa huenda uamuzi wake huo umechochea kupaa kwa ufaulu katika Halmashauri ya Igunga, ambayo mwaka jana ilishika nafasi ya 10 katika matokeo ya mtihani wa taifa wa kidato cha nne kati ya halmashauri 195 nchini.

### CHANGAMOTO YA WALIMU

Mwalimu Milazi anasema uhaba wa walimu wa masomo ya sayansi ni miongoni mwa changamoto kubwa zinazoikabili shule yake, akibainisha kuwa kwa sasa shule hiyo haina hata mwalimu mmoja wa somo la Fizikia aliyeajiriwa na serikali.

Anasema wanao walimu wawili wanaojitolea kufundisha somo hilo na kwamba changamoto ya uhaba wa walimu pia iko katika masomo ya Kemia na Baiolojia ambayo wana walimu wawili tu.

Ili kutatua changamoto hiyo, Mwalimu Milazi anaiomba serikali kuipa shule hiyo walimu wanne; wawili wa Fizikia na wawili wa Kemia na Baiolojia.

Anasema changamoto ya pili katika shule hiyo ni uhaba wa madarasa, akibainisha kuwa kwa sasa wanavyo vyumba 15 ilhali mahitaji ni vyumba 19 na watakuwa na uhitaji zaidi mwakani watakapoingia katika mwaka wa pili wa kupokea wanafunzi wa kidato cha tano.

Aidha, Milazi pia anasema shule yake haina maktaba na anaona kutotatuliwa haraka kwa changamoto hiyo huenda kutakuwa na madhara makubwa kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita.

"Hatuna jengo kwa ajili ya maabara. Kwa sasa vifaa vya maabara tumevihifadhi kwenye moja ya vyumba vya madarasa," anasema na kuongeza:

"Pia, hatuna nyumba za walimu za kutosha. Tuna nyumba tatu tu, hivyo walimu 15 hawaishi karibu na maeneo ya shule, wanaishi huko mitaani wamepanga."

### HALI ILIVYO KITAIFA

Mei 22, 2017, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, ililiambia Bunge mjini Dodoma kuwa, imebaini Tanzania inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa walimu 182,899 wa shule za msingi na 69,794 wa shule za sekondari.

Taarifa ya kamati hiyo iliwasilishwa bungeni siku hiyo na aliyekuwa mjumbe wake, Hussein Bashe (sasa Naibu Waziri wa Kilimo), wakati wa mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2017/18.

UVUMBUZI

**NA NEEMA SAWAKA, KAHAMA**

# Siri shule zilizoingia 10 bora kitaifa kutoka Shinyanga




Wanafunzi wa Shule ya Msingi Little Treasures wakiwa katika mazingira yao. Ni moja ya shule zilizoingia 10 bora kitaifa katika matokeo ya mtihani wa darasa la saba.

WAKAZI katika mkoa wa Shinyanga, wamefarijika baada ya kutangazwa kwa matokeo ya mtihani wa darasa la saba, ambapo shule tatu za mkoa huo, zimeingia kwenye shule 10 bora kitaifa.

Hizo ni Shule ya Msingi Little Treasure, iliyoko mjini Shinyanga, ambayo imeshika nafasi ya nne.

Vilevile, Shule ya Msingi Kwema Modern, iliyo wilayani Kahama ambayo imeshika nafasi ya saba, huku ikitoa mwanafunzi aliyeshika nafasi ya tisa kitaifa.

Aidha, Shule ya Msingi Rocken Hill Academy, nayo ya wilayani Kahama, iliyoshika nafasi ya 10 kitaifa.

Mwandishi wa makala haya alifanya mahojiano na wazazi, wamiliki pamoja na walimu wanaofundisha shule hizo ili kubaini siri ya mafanikio hayo yanayoendelea kuupa sifa mkoa huo.

> Isipokuwa mwaka 2017, tulishika nafasi ya 11 kitaifa na mwaka 2011, 2012 na 2013 mfululizo tulishika nafasi ya kwanza... hatubahatishi kuwepo kwenye nafasi hii.

**LITTLE TREASURES**

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, katika Manispaa ya Shinyanga, Paul Kiondo, anasema siri ya mafanikio hayo ni pamoja na wahitimu kufanya majaribio 135, kabla ya mtihani wao wa darasa la saba wa kitaifa.

Kiondo anabainisha kuwa mitihani hiyo ya majaribio ndiyo iliyochangia matokeo hayo, ikiwa ni pamoja na kutoa wanafunzi watatu kitaifa, wawili wakiwa katika kundi la 10 bora upande wa wasichana.

Mbali na majaribio, Mwalimu Kiondo anajumuisha pia jitihada kubwa zilizofanywa na walimu, wanafunzi na wazazi.

Anasema kutokana na jitihada kubwa za kufundisha na kuwaandaa vizuri wanafunzi kwa ajili ya mitihani yao ya mwisho, walitarajia kupata matokeo hayo mazuri kama ilivyotokea.

"Kujituma, nidhamu na ushirikiano ni chachu ya mafanikio yetu," anasema.

Katika shule hiyo mwanafunzi Daniel Ngassa ameshika nafasi ya saba kitaifa na wanafunzi wawili wa kike, Scholastica Yohana na Suzan Fridoline, wakiingia 10 bora upande wa wasichana, ikielezwa kuwa ni jambo la kihistoria katika shule hiyo.

"Mpaka sasa shule yetu ina jumla ya wanafunzi 726 na ilitoa toleo lake la kwanza la darasa la saba mwaka 2017 ambapo ilikuwa ya 64 kitaifa, mwaka 2018 ilishika nafasi ya 15 na mwaka 2019 imeshika nafasi ya nne kitaifa," anasema na kuongeza:

"Wanafunzi waliofanya mtihani walikuwa 91, wavulana 40 na wasichana 51."



Wanafunzi wakiwa darasani katika Shule ya Msingi Kwema Modern mkoani Shinyanga. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**WAZAZI**

Kwa upande wa wazazi ambao watoto wao wameingia 10 bora kitaifa akiwamo mwanafunzi Daniel, wanasema wanamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwawezesha watoto wao kufanya vizuri.

"Ninaahidi kufanya kila linalowezekanalo nihakikishe anaendelea zaidi kielimu," anasema Ngassa, mzazi wa mwanafunzi Daniel.

Naye Yohana Shelembi, mzazi wa mwanafunzi Scholastica, anasema siri kubwa ya mafanikio ya mtoto wake ni kujituma, nidhamu na kuwasikiliza walimu wake wanapofundisha darasani.

"Muda mwingi alikuwa anakaa bweni tangu alipoingia darasa la saba," anasema na kuongeza:

"Mwenyezi Mungu ametenda miujiza yake kwa kuonyesha uwezo alionao mtoto wetu, hivyo ni jambo la kumshukuru na hatutasita kumwendeleza zaidi kielimu."

**DC**

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, anasema ushindi wa wanafunzi wa shule ya Little treasures ni wa kuungwa mkono kwani mbali na kuitangaza wilaya yake kielimu, umeutangaza mkoa.

"Nilikuwa na imani watafanya vizuri kutokana na maandalizi yao mazuri," anasema.

**KWEMA MODERN**

Emanuel Ang'ulo ni Meneja wa Shule ya Msingi Kwema Modern wilayani Kahama.

Anasema, tangu kuanzishwa kwake, shule hiyo imeweka historia ya kuingia kwenye nafasi ya 10 bora kitaifa.

Anabainisha shule hiyo iliyoanzishwa mwaka 1995 ni ya kwanza kutumia lugha ya Kiingereza katika masomo mkoani Shinyanga.

Anasema historia ya kuingia 10 bora kitaifa ilianza mwaka 2002 baada ya kushika nafasi ya saba kitaifa na ya kwanza kimkoa na kiwilaya.

"Mwaka 2003, shule yetu ilishika nafasi ya tatu kitaifa, ya kwanza kimkoa na kiwilaya vilevile...mwaka 2005 ikashika nafasi hiyo hiyo na mwaka 2011, ilishika nafasi ya pili kitaifa, mwaka 2013, ya nne kitaifa na ya pili kimkoa na kiwilaya," anasema na kuongeza:

"Mwaka 2014, ilishika tena nafasi ya nne, mwaka 2015 haikuwamo katika 10 bora baada ya kushika nafasi ya 12 kitaifa...mwaka 2016 ilishika nafasi ya kwanza kitaifa na kimkoa."

Ang'ulo anafafanua kuwa mwaka 2017 ilishika nafasi ya 24 kitaifa na mwaka jana ilishika nafasi ya nne, huku mwaka huu wa 2019, ikishika nafasi ya saba kitaifa.

Meneja huyu anasema matokeo hayo ni matunda ya mikakati, ushirikiano na ukaribu kuanzia kwa mkurugenzi, walimu na wazazi kwa kupokea maoni pamoja na maelekezo wanayoyatoa.

"Bila kusahau walimu kujituma katika suala zima la ufundishaji ambapo kuna ushindani wa kimasomo kwa walimu katika suala zima la kufaulisha katika majaribio ya kila wiki, wakipigania nani awe namba moja katika somo lake," anasema.

Anabainisha kuwa kutokana na kushika nafasi ya saba kitaifa mwaka huu, wanaanza kujipanga ili waweze kurudi kwenye nafasi ya kwanza waliyoishika mwaka 2016, ambapo pia walitoa wanafunzi nane walioongoza kitaifa kwa mwaka huo.

Kwa upande wake Mwalimu wa Taaluma katika shule hiyo George Pande, anabainisha kuwa wamekuwa mstari wa mbele katika suala zima la ufundishaji na kwamba walimu kukosa vipindi hutokea kwa nadra sana.

"Tunahakikisha kila mwalimu anaingia darasani. Pia utaratibu uliopo ni mwalimu wa darasa kukaa darasani akimsikiliza mwalimu mwenye somo husika kama anaenda vizuri na watoto wanamwelewa," anasema na kuongeza:

"Na wanafunzi hufuatiliwa kwa ukaribu kuhakikisha wanaandika na kulifahamu somo wanalofundishwa kwa ufasaha."

**CHANGAMOTO**

Mwalimu Pande anataja changamoto kuwa ni pamoja na ile ya vitabu vya mitaala ambavyo wao kama shule binafsi wamekuwa wakipata shida kutafsiri lugha ya msamiati iliyoandikwa katika baadhi ya vitabu vya masomo.

"Tunaiomba serikali kujaribu kuangalia tatizo hili kwa sababu tuko pamoja nayo kuhakikisha sekta ya elimu nchini inapanda," anasema.

**ROCKEN HILL ACADEMY**

Mkurugenzi wa Shule ya Msingi Rocken Hill Academy, Alexander Kazimili, anasema shule hiyo ilianza mwaka 2005 na kuingia kwenye 10 bora.

"Isipokuwa mwaka 2017, tulishika nafasi ya 11 kitaifa na mwaka 2011, 2012 na 2013 mfululizo tulishika nafasi ya kwanza...hatubahatishi kuwepo kwenye nafasi hii," anasema.

Mkurugenzi huyu anasema siri ya mafanikio yao ni jitihada, juhudi na kujituma kunakofanywa na walimu pamoja na umakini katika kazi zao.

Aidha, anasema ratiba kwenda sawasawa na ufuatiliaji wa ratiba, lakini na wanafunzi kuzingatia kile wanachofundishwa.

"Kuingia nafasi ya 10 bora kitaifa kwetu ni jambo la kawaida, si la kubahatisha... kuna baadhi ya miaka tuliwahi kushika nafasi ya sita na nafasi ya saba," anasema na kuongeza:

"Siri ya ufaulu ni ufundishaji wa kujituma na wanafunzi kufanya majaribio ya mara kwa mara."

HAKI, UWAJIBIKAJI & VITA YA RUSHWA

# Rushwa inapungua nchini, kona za vita zinaongezeka



Wanafunzi wa Shule ya Sheria Tanzania. Nao wameingia ubia katika vita dhidi ya rushwa. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Nickolaus Kasera**

WIKI iliyopita kwenye safu hii ya makala, tulitazama msimamo na hatua za Rais wa kwanza, Mwalimu Julius Nyerere, kwenye dhana na suala nzima la uwajibikaji

Ni vyema sasa tukajiuliza, tulikosea wapi huko nyuma? Hapo kitaalamu linakuja jibu la kukosekana elimu ya utambuzi? Tujiulize, je, tuliwezaje kuzipa ukakamavu na uimara wenye kipaumbele, badala ya kujikita kwenye utambuzi; uwezo wa kuchambua kipi kibaya na kizuri?

Ni ukweli usiopingika kwamba ili Tanzania kufikia kiwango cha kipato cha kati, sharti liwe utekelezaji wa bidhaa za umma, uwe katika kiwango bora. Ili kufikia malengo ya hapo juu, kunatakiwa kila mmoja awe sehemu hiyo, yaani anakuwa mwangilizi wa matumizi ya bidhaa za umma na kufikia kiwango kilicho bora kinachopaswa kuwapo.

Taasisi iisyo ya kiserikali ya Twaweza, ikiwa mstari wa mbele kupambana na rushwa kupitia uelimishaji wa umma, inataja matokeo ya utafiti kupitia ripoti yake iitwayo 'Sauti ya Wananchi' imebainisha mambo kadhaa.

Mosi, Twaweza inautaja utafiti wa mwaka 2017 kwamba asilimia 80 ya rushwa nchini imepungua, ingawa inatajwa baadhi ya maeneo hayajakaa sawa katika malalamiko ya kuombwa rushwa, kwa mujibu wa utafiti huo inayourejea, polisi ikinyooshewa kidole kirefu kwa mujibu wa waliohojiwa kwenye utafititi.

Pia maeneo mengine yaliyotajwa kuptia ripoti ya utafiti kurejea waliohojiwa, ni Sekta za Ardhi, Afya, Mji na Mamlaka ya Mapato Tanzania, zikiwa nyuma ya Polisi.

Je, umma unaielewaje maana ya rushwa au mazingira yake? Mtazamo wa ripoti ya utafiti ni kama ifuatavyo na asilimia zake katika mabano: Kupokea kofia na pesa za kampeni (93%); kupewa hela na huduma (78%); watumishi hewa (65%); posho kwa watumishi (51%); mfanyabihashara mkubwa kumpa hela mwanasiasa wakati wa kampeni (3%).

Vivyo, hivyo adhabu ambazo wananchi wanafikiria zitolewe kwa wala rushwa nazo wananchi waliohojiwa wamekuwa na maoni kadhaa na asilimia zao katika mabano: Wafungwe watumishi wa halmashauri wanaojihusisha na rushwa (51%); wanasiasa wanaohusika na rushwa wafungwe (49%); na wanasiasa warudishe fedha za umma (31%).

Pia mkakati wa kupambana na rushwa na wanafunzi wanaombwa wasome kwa kina. Wanasheria nao upande wao wana wajibu.

Mawakili katika kuisaidia serikali kupambana na rushwa, kuna mchango wa mawakili wa kisheria katika kupambana dhidi ya rushwa katika sura kadhaa: Utungaji na utekelezwaji wa sera; elimu kwa jamii kuhusu falsafa ya makosa ya jinai; kusaidia usimamizi na ushauri wa kisheria; uendeshaji mashtaka; na kuwatetea watuhumiwa.

Mengine yanatajwa kwamba wakili wa sheria anapoteuliwa kwenye nafasi za maamuzi kama ilivyo kwa jaji au hakimu, kuna changamoto wanazokutana nazo katika dhidi ya rushwa. Hapo kunapatikana utata kama vile mgongano wa maslahi; wakili kusahau jukumu lake dhidi ya watoa rushwa; ushiriki wao duni katika utekelezaji baadhi ya sheria kama za Utakatishaji wa Fedha (Anti- Money Laundry Act).

Mapambano dhidi ya rushwa, yanakuwa magumu kufanikiwa, iwapo wakili atabaki katika mtazamo 'hii si vita yetu bali ni ya serikali.' Ni lazima rushwa ichukuliwe sura ya dhana 'Adui wa Taifa' kwanini kitendo kinachogharimu uchumi na maisha ya watu, kiendekezwe?

Kupitia mjadala wa 'Uwajibikaji' ninaamini matokeo kadhaayafuatayo yatakuwa na mchango kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu: Nianze na uanzishaji na kuendelezwa klabu za rushwa na uwajibikaji ndani ya Shule ya Sheria (The Law School of Tanzania.)

Nidokeze kwamba, baada ya mjadala, tulikuwa na kikao na uongozi wa The Law School, serikali ya wanafunzi, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) na tulikubaliana kuanzishwa kwa klabu hiyo na mpaka sasa kuna wanasheria 219 waliomba kujiunga na wako katika mchakato wa kuchagua viongozi wao.

Timu ya Wajibu, inaamini mijadala hii ya uwajibikaji itawajengea uwezo wanafunzi kuhusu dhana nzima ya uwajibikaji na mapambano dhidi ya rushwa, kabla ya kuingia rasmi kwenye soko la ajira. Lingine ni matarajio ya kuwapo wahitimu (mawakili) wanaowajibika, maadili na uzalendo, kwa manufaa ya taifa na kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya adui irushwa.

Wajibu kupitia katika kurasa zake za mitandao ya kijamii, hutoa ufafanuzi wa mbalimbali unaohusiana na uwajibikaji na rushwa, pia mapendekezo yanayotolewa na washiriki wa mijadala, ili kuwasilishwa kwa wahusika yatekelezwe.

**Mwandishi anapatikana kwa maoni na ushauri: samawatiarts@yahoo.com**

## RIPOTI

# Kutembea pole pole ukiwa na miaka 45, 'dalili ya uzee'



Mazoezi ya kutembea kama haya yanabashiri uzee wa mtu kulingana na utafiti. **PICHA: MTANDAO.**

KASI ya kutembea kwa watu waliofikisha umri wa miaka 40, ni ishara ya jinsi ubongo na miili yao inavyozeeka, wanasayansi wanasema.

Kwa kutumia kasi ya kutembea, watafiti wameweza kupima hali ya mtu kuzeeka.

Watu wanaotembea pole pole 'huzeeka haraka' na nyuso zao pia huonyesha kuzeeka sawa na bongo zao kuwa ndogo.

Watafiti hao pia wanasema matokeo ya uchunguzi huo, 'yalikuwa ya kushangaza."

Madaktari hutumia uwezo wa kutembea kubaini afya ya mtu kwa ujumla, hasa kwa watu walio na miaka zaidi ya 65, kwa sababu ni chanzo kikuu cha kupima nguvu ya misuli, utendaji kazi wa mapafu, uti wa mgongo na nguvu ya macho.

Kutembea pole pole ukiwa mzee pia kumehusishwa na hatari ya kupoteza uwezo wa kukumbuka.

**DALILI YA TATIZO**

Katika utafiti huo, kati ya watu 1,000 nchini New Zealand, waliozaliwa katika miaka ya 1970 na waliofuatiliwa hadi miaka 45, mwendo wao ulibadilika mapema.

Kama muendelezo wa utafiti, washiriki pia walifanyiwa vipimo vya mwili na jinsi bongo zao zinavyofanya kazi, kadri miaka yao ilivyoendelea kuongezeka.

"Utafiti huu umegundua kuwa kutembea pole pole ni tatizo ambalo limekuwepo kwa miongo kadhaa hata kabla ya kuzeeka," anasema Prof. Terrie Moffitt, mmoja wa watafiti hao kutoka Chuo Kikuu cha London nchini Uingereza na cha Duke nchini Marekani.

Hata wale walio katika miaka yao ya 45, walionyesha tofauti kubwa katika kasi yao ya kutembea, huku yule aliyetembea haraka zaidi akitembea kwa mita mbili kwa sekunde (bila kukimbia).

Kwa jumla washiriki waliotembea pole pole walionyesha dalili ya 'kuzeeka haraka' huku mapafu, meno na kinga ya miili yao ikiwa chini ikilinganishwa na watu wanaotembea haraka.

**UHUSIANO WA HALI HII NA MTINDO WA MAISHA**

Kundi la Watafiti wa Kimataifa (JAMA Network Open), limesema tofauti inayojitokeza katika uwezo wa ubongo kufanya kazi, huenda inatokana na mtindo wa maisha ya mtu binafsi.

Lakini pia linadai kuwa dalili ya kuzeeka mapema, inachangiwa na hali ya afya ya mtu alipokuwa mdogo.

Watafiti wanasema kupima kasi ya kutembea ya mtu akiwa mdogo ni njia itakayosaidia kutafuta tiba ya kudhibiti hali ya binadamu kuzeeka haraka.

Tiba kadhaa zimetolewa ikiwa ni pamoja na kuzingatia lishe iliyo na kiwango cha chini cha mafuta na kutumia dawa ya inayofahamika kama metformin.

Tiba hiyo ipo katika hatua ya uchunguzi. **BBC**

> Tiba kadhaa zimetolewa ikiwa ni pamoja na kuzingatia lishe iliyo na kiwango cha chini cha mafuta na kutumia dawa ya inayofahamika kama metformin.

## JE, WAJUA?

# Shule za kurekebisha tabia zatesa watu kama wanyama

POLISI nchini Nigeria, wamegundua zaidi ya vijana 70 wakiwa wamefungwa katika shule moja binafsi, Kaskazini mwa Nigeria.

Mamia ya vijana wametoroka kwenye shule mbalimbali za dini ya Kiislamu, katika siku za hivi karibuni nchini humo.

Shule za bweni za Kiislamu zinazojulikana kama Almajiris ni maarufu sana kwa Waislamu wengi Kaskazini mwa Nigeria.

Wazazi wanaowapeleka watoto wao katika shule hizo huwa wana matumaini ya kuwarekebisha tabia zao kwa kupata elimu ya dini ya Kiislamu.

Ingawa baadhi ya vijana wameokolewa katika vyuo hivyo, wanadai kuteswa na kunyanyaswa kingono.

Rabiu Umar Galadima mwenye umri wa miaka 26, ni miongoni mwa vijana waliookolewa katika moja ya shule hizo katika mji wa Daura, eneo ambalo Rais wa Taifa hilo, Muhammadu Buhari anatoka.

Galadima ameiambia BBC kuwa walikuwa wanatunzwa kama wanyama.

"Nilikuwa nachapwa fimbo 10 asubuhi, 10 mchana na jioni pia fimbo 10...nilikuwa nateswa, napigwa...nilikuwa kama mnyama."

Walimu wawili na mmiliki wa shule hiyo mjini Daura, anakotoka Rais Buhari, wamekamatwa.

Zaidi ya wanafunzi 300 waliandikishwa katika shule hiyo, lakini wengi waliweza kutoroka kabla ya polisi kufika, anasema mwandishi wa BBC, Ishaq Khalid.

Msemaji mkuu wa polisi kutoka Katsina aliiambia BBC kuwa mateka hao walikuwa wakiandamana, huku wengi wao wakitoroka wakiwa bado na minyororo.

Shule hiyo imekuwa ikifanya kazi kwa miongo kadhaa kama sehemu ya mafunzo ya kitabu cha dini cha Kiislam, ikishughulika hasa na wanafunzi wenye matatizo ya kitabia.

Kumekuwa na ripoti nyingi za unyanyasaji katika shule za bweni za Kiislam Kaskazini mwa Nigeria, huku wanafunzi wengi wakilazimika muda mwingine kwenda mitaani na kuanza kuombaomba. **BBC**



Baadhi ya vijana waliookolewa kutoka moja ya shule Kaskazini mwa Nigeria. **PICHA: MTANDAO.**

NA MICHAEL ENEZA

# Mtu anajulikana kwa jina au majina?

KUNA mabadiliko katika mazoea ya kujitambulisha katika baadhi ya vyombo vya habari na hasa redio, ambako suala la kujitambulisha linajitokeza katika vipindi maridhawa, kama mojawapo ya vielelezo vya ushiriki wa walengwa mbalimbali.

Inaweza kuwa ni hadhara kwa mfano ya maombezi ambako watu wanaleta ushuhuda wa yale yaliyotokea kuhusiana na madhabahu husika, eneo ambalo labda limekithiri kwa matumizi tofauti ya dhana ya jina la mtu katika kujitambulisha.

Badala ya jina mtu anakuwa na majina, na kwa maana hiyo mtu anakuwa na majina matatu badala ya jina moja, na hiyo inakuwa sahihi.

Kimantiki suala la kuwa mtu ana jina moja au zaidi, na kama anapotaja majina mengine kuacha lile la kwanza basi hayo ni majina na siyo jina lenye maneno (majina) matatu, ni suala la tabia lugha, au kwa kitaaluma 'semantics,' yaani mtu anapenda kusema nini kuhusu hilo.

Lakini anachochagua kusema au anachong'ang'ania kusema hakibadilishi lolote katika hali halisi, kuwa bado ni sahihi kusema 'jina langu ni Patrick Samueli Wakibanja' au kusema kwa staili mpya 'kwa majina naitwa.....,' halafu ukataja jina hilo kwa kusema kuwa ni majina yangu.

Suala ni kuwa hivi anatambulishwa mmoja au ni hao watatu?

Kwa mtazamo wa staili hii mpya kila jina katika hayo matatu linajitegemea, hivyo kwanza aliyetajwa hapo juu ni Patrick, halafu pia ni Samueli na isitoshe ni Wakibanja – dhana ambayo ni potofu kwa sababu yangekuwa yanajitegemea jina moja lingetosha.

Ina maana kuwa huwezi kujulikana ni nani, hadi ataje jina kamili, yaani yeye ni nani, mwanae nani, ndani ya ukoo gani, mtiririko ambao unakidhi mahitaji ya kihisia kuhusu utambulisho wa mtu huyo, na ndiyo maana inakuwa ni 'jina' lake.

Unaposema 'kwa majina' anaitwa (yote matatu) ni kama vile anajitambulisha yeye kwanza, halafu anataja jina la kwanza la baba yake, halafu na jina la ukoo wake. Sasa nani katika hadhara hiyo aliyetaka kumjua baba, au ukoo?

Suala hapa siyo kuwaeleza wanaosikiliza habari zako kwa undani (hivyo kumtaja baba na ukoo) ila kwa utoshelevu, utofautishwe na mtu mwingine.

Kwa mfano angepiga simu redioni akasema 'mini naitwa Patrick, tatizo langu ni...' lazima kungekuwa na mkanganyiko kiasi fulani kwani watu wanataka kujua ni nani hasa anayepiga simu, kwa maana kuwa ni 'Patrick yupi,' hivyo anapochukua tahadhari kuhusu swali hilo na kusema angalau 'mimi ni Patrick Samweli' anapunguza kiwango cha hizo shauku, kwani hapatakuwa na Patrick wengi wenye jina (la pili, au la baba) ambalo pia ni Samweli.

Kuongeza jina la ukoo ni ukamilishaji, kuwezesha wasikilizaji kupata picha pana zaidi nani anayeongea, ndugu yao au la.



Majina ya watu wa rangi tofauti tofauti duniani yana namna yanavyowatambulisha. **PICHA: MTANDAO**

Kwa maana hiyo hata yanapokuwa matatu bado si majina ila ni jina, kwani ni utambulisho wa mtu mmoja ambaye kwa maana hiyo ana jina, kama kusema gesi hii inaitwa 'oxygen' na nyingine inaitwa 'carbon dioxide.'

Huwezi kuingiza staili potofu kuwa zipo gesi zinaitwa carbon dioxide' kwa maana kuwa gesi hizo zina majina mawili, wakati ni kitu kimoja kinazungumziwa, siyo viwili.

Au yule mtu wa kale aliyeanza kukamilika anaitwa 'homo sapiens,' na siyo 'ana majina mawili ya homo na sapiens,' kwani 'homo' peke yake si jina ni neno tu, kama ilivyo 'sapiens,' na linakuwa jina yanapounganishwa.

Si rahisi kujua usemi huu umeanza katika mazingira gani, kama ni ya mizaha ya kwenye redio halafu ikaenezwa na kuwa fesheni au staili, au ni mtaalamu wa Kiswahili aliyeshauri hivyo.

Si ajabu wapo wataalamu wanaohesabu maneno na kusema kuwa ni 'majina' wakati jina ni muungano wa vipengele tajwa vinavyofanya kazi kwa mtu huyo. Ni sawa na utambulisho wa kimaumbile (biology) wa vianzio.

Kwanza kuna jina (species) ya mnyama, mdudu au mmea unaotambulishwa, halafu kuna 'family' yaani mkondo wa aina za wadudu, wanyama au mimea wanaofanana na kinachotajwa- kwa mfano kuna simba, chui au paka ambao wote ni jamii ya paka.

Inaitwa jamii ya paka kwa sababu kati yao mnyama anayefahamika kwa urahisi zaidi ni paka, ambaye ana maumbile ya hao wengine ila kwa kiwango cha chini zaidi, hali inayomtambulisha kwa urahisi, kuambiwa hawa wengine ni kama mapaka wakubwa.

Ila ukiwaangalia kwa karibu utagundua wana tofauti za kina, lakini haiwezekani wasifanane sana na paka.

Halafu baada ya utambulisho huo, bado kuna suala la kuwaonyesha kuwa ni wanyana wanyonyeshao (mammals) utambulisho ambao unawaweka pamoja na ng'ombe, swala, mbwa n.k, ambao wanaunda familia tofauti kila mmoja kwa kundi lake.

Ng'ombe wanakuwa pamoja na nyati au nyumbu, swala wanakuwa jamii ya mbuzi pamoja na digidigi na wengine, wakati mbwa anaungana na mbwa mwitu, fisi na kadhalika.

Ndiyo utambulisho ulivyo, kwamba kufahamu kundi la mtu huyo kwa karibu au kwa mbali (jina la baba au la ukoo likiwepo) ndiyo unapata picha ya mhusika. Hakamiliki kwa jina lake moja, katu.

Kitaaaluma utambulisho kwa maana ya jina la mtu au kumfahamu mtu ni 'binary' katika uhalisia wake, yaani ni kitakwimu fikirika chenye ncha mbili angalau, chenyewe na kundi linalohusika na uwepo wake.

Hivyo kwa ufinyu jina moja linatosha pale mtu anapokuwa anafahamika, hivyo ukimwita mtoto kwa jina lake nyumbani hakuna uwezekano kuwa yupo mtu ambaye hataelewa nani anaitwa, ila kama wapo watoto wawili wa jina hilo moja itabidi kuwe na jina kama 'Kulwa na Doto' kama ni mapacha, kujua unamwita yupi, na kama ni wengine labda kuwe na 'dogo' kati yao ili ijulikane anapoitwa.

Kwa hali hiyo jina halisi litabaki kwa yule mkubwa, na mdogo anaitwa tu 'dogo' kwani tayari yuko Patrick mwingine hapo hapo.

> Zanzibar ni tofauti, mtu anaitwa jina la babu hivyo anahitaji kutaja pia jina la baba halafu tena la babu ili utambulisho wake ukamilike, na siyo mbwembwe za kuitana.

Uwepo wa majina matatu ni kama fasaha ya ziada ya majina mawili, kufanya jina la mtu litosheleze mahitaji ya kufahamika kwa maana ya kuwekwa katika kundi fulani la kijamii kwa utambulisho wa kijinsia, kifamilia na kiukoo.

Kutumika kwa majina matatu kunaendana na tamaduni, halafu na ngazi ya utambulisho husika ambako mara nyingine wako wanaokubali jina moja tu na inakuwa vigumu kusikia lingine likitajwa, ambayo kadhaa husikika kwa wanamichezo wa Brazil.

Hapa nchini, majina mawili yanatosha kuunda jina la mtu na kuandika la tatu ni ufasaha wa ziada kwa mfano kama mtu anaelezea kwa kirefu kiasi fulani kuhusu mtu huyo.

Zanzibar ni tofauti, mtu anaitwa jina la babu hivyo anahitaji kutaja pia jina la baba halafu tena la babu ili utambulisho wake ukamilike, na siyo mbwembwe za kuitana.

Kimsingi hulka hii ya 'kwa majina naitwa' ni potofu na inaonyesha jinsi dhana zisizoiva zinavyopenya katika Kiswahili na kuteka akili za watu, wadhanie kuwa ni 'kwenda na wakati' ila ni uharibifu tu, kwani wanaua dhana halisi ya jina.

Wanadhani kuwa jina ni lile mtu analoitwa, yaani kwa mfano huo hapo juu ni Patrick, kana kwamba inatosha, kuwa watu watatambua tu kwa haraka kuwa ni Patrick.


Lakini jina ni utambulisho, na kwa kawaida ya binadamu na ndiyo maana vyombo vya habari vinavuta hisia za watu, tunapenda kujua kama kuna jambo limemfika mtu unayemjua; akisema tu Patrik anajificha, au anapuuza.



WADAU
**SABATO KASIKA**

# Sauti za wadau

SEKONDARI za kata zimeanzishwa ili kila mtoto anayefaulu elimu ya msingi aendelee na masomo karibu na kwao. Hata hivyo kuna mtazamo kwamba zinaweza kuwa chanzo cha kutoweka umoja wa kitaifa. Wadau wanajadili.



**BERLY BUSAGI (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

UKIFUATILIA historia, ni kwamba amani tuliyonayo imechangiwa pia na umoja wa kitaifa ambao umetokana na watu kuingiliana kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania, hasa kutokana na elimu.

Wanafunzi walikuwa wanatoka Dodoma kwenda kusoma Rukwa, Mbeya au mikoa mingine kwa pamoja kama Watanzania na si kama ilivyo sasa, ambapo zimeanzishwa shule za kata ili wanafunzi waweze kusoma maeneo wanayotoka.

Kwa utaratibu huu mimi ninadhani yasipofanyika mabadiliko ya haraka kwa kujenga mabweni kwenye shule hizo, umoja huu wa kitaifa utatoweka na mwishowe utakuja ukanda na hata u-mkoa.

Sisi tumeendelea kuwa kitu kimoja kutokana na mwingiliano huo ambao kwa kiasi kikubwa umechangiwa na elimu, lakini sasa tunataka kuuondoa kwa mtindo wa shule za kata.

Sikatai kwamba sasa hakuna wanafunzi wanatoka mikoa mingine kwenda kusoma kwingine, ila ukweli ni kwamba kwa mtindo wa shule za kata ni wanafunzi wachache watakaopata nafasi ya kwenda kusoma kwingine pale wanapohitimu kidato cha nne kutokana na ukweli kuwa miaka ya nyuma kulikuwa na wanafunzi wanaofaulu kwenda shule huku wakiwa hawajui kusoma wala kuandika na pia elimu inayotolewa kwenye hizo shule haimpi nafasi mwanafunzi kusonga mbele.

Kwa hiyo wahusika watafakari na kisha wachukue hatua za kunusuru elimu na umoja wa kitaifa ambao umedumu kwa miaka mingi na umesaidia Watanzania kuheshimiana na kujaliana kwa kila hali.



**JACKSON NACKON MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM**

NINALOLIONA kwenye shule hizi ni uchache wa walimu, ambao umekuwa ukichangia wanafunzi wasipate elimu, ambayo ni bora na badala yake baadhi yao wamekuwa wakienda kushinda shuleni na kurudi wakiwa hawana kitu kichwani.

Wanafunzi wa shule wakipata elimu bora watafaulu vizuri na kusonga mbele, kwa hiyo bado watakuwa na nafasi ya kwenda kusoma shule nyingine za hapa nchini na hivyo umoja wa kitaifa utaendelea kudumu.

Lakini zisipoboreshwa ndipo hilo tatizo litakuwa kubwa kwani wengi wao watakuwa wanaishia kidato cha nne na kurudi nyumbani. Hawatakuwa na nafasi ya kufaulu, ambapo wangeweza kwenda mikoa mingine ili kuendelea na masomo na vidato vya juu.

Kwa hali hiyo mimi ningeishauri serikali ifanye juu chini ili kuhakikisha kwamba shule hizo zinakuwa na walimu wa kutosha, kwani tumekuwa tukisikia kwenye vyombo vya habari kwamba zipo shule za kata, ambazo unakuta zina walimu wachache.

Idadi hii haiwezi kukidhi mahitaji ya wanafunzi na badala yake watakuwa wanakwenda kushinda shuleni tu na kurudi jioni bila kusoma kwa sababu walimu hawatoshi, sana sana watasoma masomo machache, ambayo hayawezi kuwasaidia kusonga mbele.

Cha kufanya hapa ni kuzidi kuziboresha ili ziweze kutoa elimu bora ambayo itasaidia kuzifanya zipendwe na watu wengi kwa ubora wa elimu na pia kuongeza vidato katika shule hizo za kata kwenye mikoa mbalimbali nchini, badala ya kutegemea shule kongwe ambazo ni chache zisizoweza kuchukua wanafunzi wengi.



**MWANAMTAMA RAMADHAN (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

KWANGU mimi binafsi sioni kwamba wanafunzi kusomea karibu na maeneo ya kwao kunaweza kusababisha kutoweka kwa umoja wa kitaifa, kwani wanapofaulu kwenda kidato cha tano ni lazima watapelekwa kwenye shule nyingine kulingana na ufaulu wao.

Kwa hiyo mwanafunzi anaweza kuwa anasoma hapa Dar es Salaam hadi kidato cha nne na akaufulu kwenda kusoma kidato cha tano na cha sita huko Dodoma, Mwanza, Kilimanjaro, Arusha au mikoa mingine.

Kwa hiyo mimi binafsi kwa kweli sioni tatizo lolote katika hili.

Shule za kata zimekuja kusaidia kupunguza kuwapo kwa watoto mitaani badala yake wanahudhuria masomo shuleni ingawa wakati mwingine unakuta shule zina walimu wachache na pia ukosefu wa vifaa vya kufundishia, lakini bora mwanafunzi akawa kwenye mazingira ya shule kuliko kukaa nyumbani.

Lakini mawazo yangu siyo kwamba ninakataaa mabweni yasijengwe kwenye shule za kata, kama uwezo upo yajengwe tu ili yaweze kupokea wanafunzi wanaotoka mikoa mingine.

Kingine ni kwamba matatizo yanayozikabili shule za kata yawe ni changamoto kwa wizara husika ili kubuni mbinu ambazo zinaweza zikasaidia kuyapunguza ama kuyamaliza kabisa ili elimu ya Tanzania iwe bora zaidi.



**MWANURU DIKOLAGWA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

ASILIMIA kubwa ya wanafunzi wa kidato cha nne ni wale, ambao wanasoma shule za sekondari za kata, wakati asilimia ndogo ni wale wanaokwenda kusoma kwenye shule za vipaji maalum, ambazo ziko katika mikoa mbalimbali nchini.

Hivyo bado umoja wa kitaifa upo na utaendelea kuwepo hasa kwa kuzingatia kwamba hata wale wanasoma shule za kata wanafundishwa na walimu kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini.

Pia ninapenda niwakumbushe Watanzania kuwa kuanzishwa kwa shule hizo kulilenga kuwapunguzia gharama wazazi, ambao hawana uwezo wa kuwasomesha watoto wao mbali.

Lakini siamini kama serikali imeshamaliza kazi ya kuimarisha shule hizo, bado inaendelea kuziboresha ikiwa ni pamoja na kuhakikisha zinakuwa na walimu wa kutosha, vifaa vya kufundisha, madawati na vitu vingine, ambavyo vinahitajika shuleni pamoja na mabweni.

Ni vyema tukumbuke kuwa hata Roma haikujengwa siku moja. Hata hivyo serikali haiwezi kufanya yote kwa mara moja, inaendelea kufanya jitihada ili kuhakikisha kwamba inaboresha shule hizo.

Kwa hiyo shule za kata ni za muhimu sana na sisi wananchi tutahakikishe zinaboreshwa na nina uhakika umoja wa kitaifa utaendelea kuwapo na wala shule hizi haziwezi kuuondoa kwani wale wanaofaulu kwenda kidato cha tano, huwa wanahamia shule yoyote hapa nchini kulingana na mchepuo wa masomo yao.



**STEPHEN MGOMBOZI (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

HUWA ninashangaa sana na pia nimekuwa nikiomba shule hizi ziweze kuwa na mabweni, ambayo yatasaidia kupokea wanafunzi kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Ni kweli kwamba iwapo hali itaendelea kuwa kama ilivyo, basi umoja wa kitaifa ambao ulianzishwa na Mwalimu Nyerere utatoweka, gharama ya kuurudisha itakuwa kubwa kuliko, ambayo tungetumia kujenga mabweni.

Wapo baadhi ya wabunge wamekuwa wakishabikia badala ya kuziimarisha ili ziweze kutoa elimu bora. Kwa sasa unakuta wanafunzi wanaohitimu shule za msingi zilizopo Kariakoo Dar es Salaam, wanapelekwa sekondari zilizopo eneo hilo. Bahati mbaya ni kwamba wengi wao huwa wanafanya vibaya kwenye mtihani wa kidato cha nne, kwa hiyo mwisho wa siku huwa wanaishia hapo na kubaki waliko na kuendelea na maisha mengine lakini kama wangehitimu elimu ya msingi na kupelekwa mikoa mingine ingekuwa ni rahisi kwao kuchanganyika na wenzao wa mikoa mingine kama njia ya kudumisha umoja wa kitaifa, kuliko mtindo huu tunaokwenda nao kwa sasa.

Kinachotakiwa ni kila shule ya sekondari ya kata kuwa na mabweni, ambayo yatakuwa yanapokea wanafunzi kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini, kwani mbali na kusoma watakuwa wanajifunza mambo mengi yanayohusu mila zao kama sehemu mojawapo ya kudumisha umoja wa kitaifa.



## Ukatili kijinsia wachochea VVU

**Na Grace Mwakalinga, CHUNYA**

UKATILI wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto kwenye maeneo ya migodi Chunya mkoani Mbeya umetajwa kusababisha ongezeko la maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi wilayani hapa.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Maryprisca Mahundi, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na Nipashe kuhusu hali ya ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto na wanawake ilivyo sasa.

Alisema matukio hayo yanayofanyika katika wilaya hiyo ni ubakaji kwa wanawake na watoto pamoja na ulawiti wa watoto wa kiume kwenye maeneo ya migodi ambao wakati mwingine unahusishwa na imani za kishirikina.

Mahundi alisema takwimu za wilaya hiyo zinaonyesha kuwa tangu Januari hadi Desemba, mwaka jana, matukio ya ubakaji 23 yalitokea na kwamba hao ni wale waliotoa taarifa za kufanyiwa unyama huo.

"Hatujui hao waliobakwa walinusurika kwa kiasi gani na maambukizi ya VVU lakini kuna baadhi huwa wanaamua kukaa kimya baada ya kufanyiwa unyama huo wakikwepa fedheha, hivyo yawezekana idadi ni kubwa zaidi," alisema Mahundi.

Alisema matukio hayo ni changamoto kubwa katika mapambano dhidi ya Ukimwi kwa kuwa yamekuwa yakichangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la maambukizi ya VVU.

Mahundi alisema mapambano dhidi ya virusi vya Ukimwi wilayani humo yanakabiliwa na changamoto nyingi ambazo zinarudisha nyuma mapambano hayo.

Alisema baadhi ya wananchi wanaopimwa na kubainika kuwa na maambukizi hayo, wanaishi mbali na vituo vya kutolea huduma na hivyo kushindwa kuhudhuria kliniki na kutumia ipasavyo dawa za kufubaza virusi hivyo (ARV).

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Sophia Kumbuli, aliwataka wazazi na walezi kutoona aibu katika kuwaelimisha watoto wao namna ya kuepuka gonjwa hilo hatari.

Aliwataka kuwa na madarasa huru ya familia kwa ajili ya kuwaelimisha watoto wao kuepuka kufanya ngono zembe ambazo zinaweza kuwasababishia kupata maambukizi.

Kumbuli alisema kwa sasa wameanza kupeleka huduma hiyo maeneo yote ya wilaya kwa kuwafuata wananchi hadi maeneo ya vijijini ambako huduma za afya hazipatikani kirahisi.

**"Hatujui hao waliobakwa walinusurika kwa kiasi gani na maambukizi ya VVU lakini kuna baadhi huwa wanaamua kukaa kimya baada ya kufanyiwa unyama huo wakikwepa fedheha, hivyo yawezekana idadi ni kubwa zaidi," alisema Mahundi.**

# Wabainika kusumbuliwa na tezi dume

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WAGONJWA 10 kati ya 20 wanaopimwa tezi dume kila siku katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya, wanabainika kuwa na ugonjwa huo.

Daktari bingwa wa radiolojia katika hospitali hiyo alisema hayo juzi wakati wa maadhimisho ya miaka 34 tangu kuanzishwa kwa taasisi hiyo.

Dk. Ngatunga alisema idadi hiyo ya wagonjwa inatokana na upimaji wa kila siku na kwamba wengi wanaobainika kuugua ni wanaume kuanzia umri wa miaka 45 na kuendelea na wengi wanabainika wakiwa katika hatua za mwisho za ugonjwa.

"Wanaume wengi tunaowapima katika idara yetu ya radiolojia tunawabaini kuwa na tezi dume na wengi hufika kupima wakiwa tayari ni wagonjwa jambo ambalo linatufanya tushindwe kutafuta njia sahihi ya kuwatibu. Ni wachache sana wanapima wakiwa katika hatua za mwanzo na hao tunawasaidia na wanaendelea vizuri," alisema Dk. Ngatunga.

Aliongeza kuwa: "Mwitikio wa wananchi kupima afya zao kabla ya kuugua ni changamoto hasa kwenye idara yetu ya mionzi jambo ambalo linafanya idadi kubwa ya wagonjwa wanaofika kupima afya zao kubainika kuwa katika hali mbaya hivyo kuwa vigumu kupona."

Daktari huyo alizitaja baadhi ya sababu zinazofanya watu kutojitokeza kupima afya mapema ni pamoja na baadhi ya magonjwa kutosababisha maumivu, hivyo mtu hujiona yuko salama wakati ugonjwa unaendelea kusambaa na kukomaa mwilini.

Mtaalamu wa radiolojia katika hospitali hiyo, Baita Ngwaji, alisema tangu kuanzishwa kwa idara ya radiolojia ambayo inatoa huduma mbalimbali kama X-Ray, Utra Sound na CT- Scan, kumekuwa na mwitikio mkubwa wa wagonjwa kupima afya licha ya kuwa walio wengi hufika wakiwa wamechelewa.

Ngwaji alisema kila siku hupokea wagonjwa 120 hadi 130 wanaopima magonjwa yao kwa kipimo cha Utra Sound na 25 hadi 30 CT- Scan huku X- Ray wakiwa 80 hadi 100.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya, Dk. Godlove Mbwaji, alisema hospitali hiyo inaendelea kuboresha huduma za afya ili kuhakikisha wananchi wote wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini wanafurahia huduma za matibabu.

Alisema katika kuadhimisha miaka 34 tangu kuanzishwa kwa hospitali hiyo, walifanya bonanza ambalo lilihusisha shughuli mbalimbali ikiwamo michezo ya kukimbia, mpira wa miguu na upimaji wa afya bure.

Mtendaji wa Kamati ya Amani kutoka madhehebu mbalimbali Mkoa wa Mbeya, Shekhe Juma Abdallah, aliwahamasisha wananchi kujenga utaratibu wa kupima afya zao mara kwa mara.



Mkurugenzi wa Shule za St. Marcus za jijini Mbeya, ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Songwe, Philipo Mulugo, akiwakabidhi zawadi za pikipiki walimu wawili wa shule hizo waliowawezesha wanafunzi kufanya vizuri kwenye mitihani ya kidato cha nne na darasa la saba na kuzifanya kuwa miongoni mwa shule bora, katika hafla iliyofanyika, jimboni humo juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# DC ataka msalaba mwekundu kubadilika

**Na Grace Mwakalinga, KYELA**

MKUU wa Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, Claudia Kitta, amekitaka Chama cha Msalaba Mwekundu nchini kuongeza weledi wakati wa utekelezaji wa majukumu yake.

Amekitaka chama hicho kutumia muda mwingi kuokoa maisha ya watu kabla ya maafa kutokea badala ya kusubiri majanga.

Kitta alitoa rai hiyo hivi karibu wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Maafa Duniani ambayo kitaifa yalifanyika wilayani Kyela na kuratibiwa na Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania.

Alisema kumekuwa na mazoea kwa baadhi ya taasisi zinazojihusisha na utoaji wa huduma kwa wananchi husubiri zile zitokanazo na matukio hatarishi, kuwahudumia watu baada ya matukio jambo ambalo alisema si malengo ya chama hicho.

"Mjielekeze zaidi katika kutoa elimu ya namna wananchi wanaweza kukabiliana na majanga mbalimbali na kuandaa namna nzuri ya kujisaidia iwapo maafa yatatokea.

"Chama cha msalaba mwekundu ni taasisi nyeti ambayo inahitaji kutekeleza majukumu yake kwa weledi ili kuepusha wananchi na majanga, lakini kuwaokoa yanapotokea. Tunapoadhimisha siku hii muhimu, naomba tutafakari mafanikio na changamoto ambazo zitatupa mwongozo wa namna ya kuboresha utendaji kazi wetu," alisema Kitta.

Alisema Wilaya ya Kyela kuwa miongoni mwa maeneo nchini yanayohitaji idadi kubwa ya wanachama wa msalaba mwekundu kutokana na historia kuonyesha uwapo wa maafa yakiwamo mafuriko na magonjwa ya mlipuko ikiwamo kipindupindu.

Mwenyekiti wa Chama hicho Mkoa wa Mbeya, Ulimboka Mwakilili, aliwashauri wananchi wilayani Kyela kutumia vizuri mradi wa miaka miwili wa kujikinga na maafa ili kuleta tija kwa wakazi ambao mara kwa mara wamekuwa wakikumbwa na maafa.

Mwakilili aliwasisitiza waendelee kuchukua tahadhari na kupeana taarifa za mara kwa mara pale wanapokuwa na hofu hasa juu ya uwepo wa magonjwa ya milipuko kwa sababu wilaya hiyo inapakana na nchi jirani ya Malawi hivyo kuna mwingiliano mkubwa wa watu.





## Bil.3/- kuboresha huduma afya Bahi

**Na Renatha Msungu, BAHI**

SERIKALI imetoa Sh. bilioni tatu kwa Wilaya ya Bahi kwa ajili ya kuboresha miundombonu ya afya kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali ya wilaya.

Mkuu wa wilaya hiyo, Mwanahamisi Munkunda, alisema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akihimiza wananchi kushiriki katika chanjo ya surua, rubella na polio kwa Mkoa wa Dodoma.

Alisema fedha hizo zimesaidia kwa kiwango kikubwa zitaleta mapinduzi kwenye sekta ya afya.

Munkunda alisema kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 1.5 zilitolewa kwa ajili ya kujenga vituo vitatu vya afya vya Bahi Mjini, Mndemu na Chifutuka ambavyo tayari vimeanza kutoa huduma.

"Vituo hivyo pamoja na mambo mengine, vitatoa huduma za upasuaji, vipimo mbalimbali, mama na mtoto na kulaza wagonjwa ambao awali walikuwa wakienda Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Dodoma zaidi ya kilometa 60 kupata huduma hizo," alisema.

Pia alisema Sh. bilioni 1.5 zimeelekezwa kwa ajili ya kujenga hospitali ya wilaya ambayo haikuwapo na kwamba awali kituo cha afya cha Bahi kilitumika kama hospitali ya wilaya.

Alisema itakapoanza kutoa huduma hospitali hiyo itasaidia wananchi wengi ambao walikuwa wakikosa huduma muhimu za afya na vipimo vikubwa.

Munkunda alisema kutokana na kuboreshwa kwa huduma za afya wilayani humo vifo na magonjwa vitapungua ili wananchi washiriki vyema kwenye shughuli za maendeleo.

Mkuu huyo alisema kusogezwa kwa huduma za afya kwa wananchi kumesaidia kutotumia muda mwingi kusaka huduma za afya.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, Danford Chisoma. alisema wilaya yake sasa imeboreshewa miundombinu ya huduma za afya hivyo wananchi wanatakiwa kufika kwenye zahanati na vituo vya afya ili kupata huduma.

Chisoma aliwataka wananchi kutimiza wajibu wao katika kuchangamkia fursa hiyo kwa ajili ya kupata huduma za afya katika maeneo yote zinapopatikana karibu nao.

# Wazazi waonywa tabia kuozesha watoto mapema

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

WAZAZI wametakiwa kuacha tabia ya kuwaozesha watoto wao pindi wanapohitimu kidato cha nne badala yake wahakikishe wanasaidia kutimiza ndoto zao za elimu.

Diwani wa Kilimani jijini Dodoma, Neema Chiwanga, alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mahafali ya nane ya Shule ya Sekondari ya Sechelela.

Alisema kumekuwapo na tabia ya baadhi ya wazazi kuwaozesha watoto wao mapema pindi wanapomaliza kidato cha nne bila kujua wanakatisha ndoto zao.

"Hapa ninazungumzia wanafunzi wa jinisia zote mbili kwa sababu wote hawa bado watoto wadogo. Hata kama kuna wengine wamefikia umri wa miaka 18, bado ni wadogo wanahitaji kupewa msaada wa kimawazo ili kufikia kiwango cha juu cha elimu," alisema.

Chiwanga alibainisha kuwa wanapomaliza mitihani watakuwa na muda mrefu nyumbani na washauri wa karibu kwao ni familia zao hasa wazazi, hivyo wana jukumu la kuhakikisha wanawalinda ili wasiingie kwenye mikono ya watu wasio sahihi.

Alishauri watakapokuwa wakisubiri matokeo ya kidato cha nne, wasomeshwe mafunzo ya muda mfupi ya ufundi ili kujiongezea ujuzi.

Aliyataja baadhi ya mafunzo hayo kuwa ni ufundi wa aina mbalimbali, ushonaji na mafunzo ya kompyuta.

Chiwanga pia aliwataka wahitimu hao watakapokuwa nyumbani kuhakikisha wanaishi vizuri na jamii inayowazunguka na kuepuka kujiingiza kwenye vikundi vya ulevi na kihalifu.

"Hapa shuleni mlikuwa mnaishi kwa kutunzwa vizuri, lakini huko uraiani mtakuwa huru, wakati mwingine mzazi hajui uko wapi. Ukijiingiza huko umeshapotea, hutaweza kutimiza malengo yako ya elimu," alisema.

Awali, akisoma risala ya wahitimu, Omari Macheda alisema wamejiandaa vizuri kufanya vizuri katika mitihani yao.

Mkuu wa Shule hiyo, Grace Shilly, alisema shule hiyo inakabiliwa na upungufu wa vyumba vya madarasa na nyumba za walimu. Alisema kwa sasa shule ina nyumba moja huku walimu waliopo ni 37.

Shilly alitaja changamoto nyingine kuwa ni ubovu wa miundombinu ya barabara ya kuingia shuleni hapo, ukosefu wa mashine ya kutolea nakala na kukosekana kwa huduma ya maji shuleni hapo.



Diwani wa Kata ya Kilimani, Neema Chiwanga, akizungumza na wazazi na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Sechelela ya jijini Dodoma, katika mahafali ya nane ya shule hiyo, yaliyofanyika mwishoni mwa wiki. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wakulima Mpwapwa wapewa somo tabianchi

**Na Peter Mkwavila, MPWAPWA**

WAKULIMA wilayani Mpwapwa mkoani Dodoma wametakiwa kuzingatia ushauri wa kitaalamu ili kulima kilicho chenye tija na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Wito huo ulitolewa jana na Ofisa Kilimo na Ushirika wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Maria Lesharu, alipokuwa akizungumza na wakulima wa kijiji cha Inzomvu Kata ya Kimagai wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mkulima yaliyoandaliwa na Chama cha Kilimo cha Mboga na Matunda (Taha).

Lesharu alisema ili kilimo kiwe na tija na wapate mazao mengi lazima wazingatie ushauri wa wataalamu kutokana na ukanda wa mazao.

Aliwataka kutolima kilimo cha mazoea kwa kulima zao moja kila msimu jambo ambalo linasababisha wapate mavuno kidogo huku wakiwa wamepoteza nguvu nyingi.

"Tunapozungumzia kufikia Tanzania ya viwanda, mkulima mdogo anahusika moja kwa moja katika kuzalisha malighafi zitakazotumika viwandani. Tukiendelea kulima kwa mazoea hatutaweza kulifikia soko," alisema.

Ofisa huyo alisema ni muhimu wakaunganisha nguvu kwa kujiunga kwenye vikundi ili kufikia malengo makubwa.

Ofisa Miradi wa Taha, Elianchea Shang'a, alisema chama hicho kinajihusisha na kuendeleza kilimo cha mboga, matunda na maua na kinalenga kumjengea uwezo mkulima mdogo kuondokana na kilimo cha mazoea na kulima kilimo ambacho kitamsaidia kujikwamua na umaskini.

Alisema Taha inaboresha mazingira wezeshi ya biashara ya mazao ya matunda, mboga na maua kwa kutoa ushauri na taarifa za masoko kwa wakulima wadogo wa kati na wakubwa.

Naye mkulima wa matikiti maji wilayani Mpwapwa, Aidan Ulaya, alisema aliamua kulima zao hilo kwa lengo la kufanya mabadiliko ya kilimo na kuachana na kilimo cha mazoea.

Mkulima huyo aliomba serikali kuongeza wataalamu wa kilimo vijijini na kuwekeza kilimo cha umwagiliaji kwa kuwa ndich chenye tija.

Pamoja na kuchukua uamuzi huo, alisema kuwa bado kuna na changamoto kubwa ya masoko ya mazao.

Pia alisema changamoto kubwa inayowakabili wakulima wengi vijijini ni kukosa taarifa sahihi za masoko na kuuza mazao yao kwa walanguzi ambao huwapunja wakulima.



# Wanahabari wanawake kufundishwa kujiamini

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

SERIKALI imesema kuna haja ya kuwapatia waandishi wa habari wanawake mafunzo ya kujiamini ili kuwaepusha na udhalilishaji wakiwa nje na ndani ya ofisi zao.

Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Mahmoud Thabit Kombo, aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua mafunzo ya siku moja ya wanawake na vyombo ya habari.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na Shirika la Internews kwa kushirikiana na Chuo cha Habari na Mawasiliano ya Umma Zanzibar (ZJMMC).

Alisema pamoja na waandishi wa kike kuwa na elimu kubwa na ya kutosha lakini wanakosa kujiamini na kuruhusu kufanyiwa udhalilishaji wakiwa ofisini au hata nje ya ofisi katika shughuli zao za kazi.

Aidha, alisema kuwa kupitia mjadala huo ni vyema wakaanzisha somo la kujiamini ili kuwajenga wanahabari wanawake kujiamini na kujitambua.

Pia aliwataka waandishi hao wa habari kujikita katika uandishi wa uchumi na jamii ili kujenga uchumi imara na kuleta maendeleo.

Alisema kuwa katika utafiti alioufanya hivi karibuni aligundua kuwa waandishi wengi wamekuwa wakiandika zaidi habari za siasa kuliko za uchumi na za kijamii.

Hivyo, alisema kupitia mafunzo hayo ni vyema wakafanya majadiliano kuhusu kuandika habari za kiuchumi hasa ikizingatiwa kuwa hivi sasa nchi inataka kujengwa kwenye uelekeo wa uchumi wa viwanda.

"Waandishi wa habari zaidi wamejikita katika taarifa za siasa kuliko uchumi na kijamii na kusahau kuwa siasa imara hujengwa na nchi yenye uchumi bora na jamii inayojua iliyo na taarifa mbalimbali," alisema.



Washiriki wa Kongamano la Wajasiriamali Wanawake Zanzibar, wakishangilia hotuba ya Mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mwanamwema Shein (hayupo pichani), wakati wa ufunguzi uliofanyika, Tunguu, Wilaya ya Kati Unguja wikiendi. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Serikali yaelezea malengo ya Mbweni

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

SERIKALI imeeleza kuwa lengo la kujenga Chuo cha Ufundi Mbweni ni kutoa vijana wenye ujuzi na mbinu zitakazowawezesha kushiriki kikamilifu katika kazi za uzalishaji na kukuza uchumi wa nchi.

Akizungumza katika mahafali ya tano ya Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia Naibu Waziri wa Habari Utalii na Mambo ya Kale, Choum Kombo Khamis, alisema.

Alisema kwa sasa Zanzibar inajivunia kuwapo kwa wataalamu hao wanaoongezeka siku hadi siku.

Alisema kwa sasa vijana wenye utaalamu wa masuala mbalimbali ya ufundi ikiwamo uhandisi wa mitambo na gari, mafuta na gesi wameongezeka na kufikia 1,700 kwa mwaka 2019 kutoka vijana 57 mwaka 1967 kilipoanzishwa chuo hicho.

Vilevile aliwaomba wahitimu watakaobahatika kuajiriwa watumie vyema ujuzi wao katika kujenga nchi na wale wasiopata ajira wajiendeleze kwa kujiajiri wenyewe ili kupambana na umaskini.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Dk. Idriss Muslim Hijja, alisema serikali imeshaidhinisha kutolewa mafunzo ya uhandisi wa matengenezo ya ndege na urubani kwa chuo hicho ili kuweza kukuza soko la anga visiwani Zanzibar.

Akisoma risala kwa niaba ya wahitimu hao, Annuar Asaa Hamad, aliiomba serikali kuandaa utaratibu wa kuwapatia nafasi za udhamini wa masomo nje ya nchi kila mwaka ili kuongeza elimu zaidi pamoja kuziomba baadhi ya taasisi ikiwamo za serikali zinazokataa kuchukua wanafunzi kwa ajili mafunzo ya vitendo kuacha kuwakatalia nafasi za kujifunza.

Jumla ya wanafunzi 448 wamehitimu mafunzo katika fani mbalimbali ikiwamo stashahada ya uhandisi mawasiliano, habari na biashara, maabara ya sayansi na teknolojia.

# Waziri apigia debe uzazi wa mpango

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Hamad Rashid Mohamed, amesifia uzazi wa mpango kuwa ni salama tena unamwezesha mwanamke kujifungua salama na kupata watoto wenye afya bora na akili timamu.

Alisema hayo jana ofisini kwake Mnazimmoja wakati wajumbe wa Chuo Kikuu cha Al Azhar nchini Misri, walipoitembelea Wizara ya Afya.

Alisema amefurahishwa na ujumbe huo ambao utasaidia kuongeza juhudi katika jamii zenye lengo la kuhamasisha uzazi wa mpango visiwani Zanzibar na Pemba.

Alisema ujumbe huo umeeleza mfumo wa uzazi wa mpango ambao unaotumika nchini Misri kuwa ni utaratibu wa njia za Kiislamu ambao huweza kuwaweka mama na mtoto katika hali salama.

Alifahamisha kuwa mfumo huo wanaoutumia umefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika kupiga hatua ya uzazi bora na salama hadi kuwa ni nchi ya kwanza katika uelewa wa uzazi wa mpango.

Aidha, alisema ujumbe huo utaisaidia Zanzibar kupata taaluma sahihi ya uzazi wa mpango kwa njia za kidini na kisayansi kwa kuandaa muhadhara na kutoa udhamini wa mafunzo ya muda mrefu nchini Misri kwa kuwa madaktari na wauguzi kutoka Tanzania.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) Tanzania, Jackline Mahon, alisema iko haja ya kuwajali kinamama wajawazito ili wajifungue wakiwa na afya iliyo bora.

Aidha, alisema pamoja mama ni lazima pia kuwajali watoto wao hivyo shirika limeweza kusaidia boti kwa ajili ya uzazi salama kwa mama na mtoto visiwani.

Ujumbe kutoka Chuo Kikuu cha AL Azhar nchini Misri, ulisema mtazamo wa uzazi wa mpango kwa njia ya Kiislamu unasaidia kumweka mama na mtoto katika afya bora na humwepusha na madhara ya uzazi yanayoweza kujitokeza kwa kuzaa bila mpangilio tena papo kwa papo.

Uzazi wa mpango humwezesha mama na mtoto kuwa na afya bora na malezi bora ambayo huongeza mapenzi na kupelekea kukua mwili na kiakili ya mtoto huyo.

# Milioni 1.2 wanufaika mikopo ya mifuko

**Na Happy Severine, SIMIYU**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye ulemavu), Jenista Mhagama, amesema takribani wajasiriamali 1,237,984 wamenufaika na mikopo ya mitaji iliyotolewa na mifuko ya fedha katika programu za uwezeshaji wananchi.

Mhagama alisema hayo jana, wakati wa kilele cha maonyesho ya mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi yaliyoandaliwa na Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kushirikiana na mifuko mbalimbali ya kifedha, ambayo yalihitimishwa Mjini Bariadi.

Alisema tangu kuanzishwa kwa baraza hilo, jumla Sh. bilioni 388.4 zimetolewa na mifuko hiyo katika kuwasaidia wajasiriamali na Watanzania wote kukuza kipato na kuongeza thamani ya bidhaa zao.

Aliongeza ili baraza liongeze idadi ya utoaji mikopo na mtaji kwa wananchi, ni lazima mifuko hiyo ikapanua wigo na kusogeza huduma zake katika wilaya na vijiji ambako ndipo wananchi wengi wana uhitaji.

Pia aliitaka mifuko hiyo kuendelea kutoa mikopo kwa wananchi kwa riba nafuu tofauti na taasisi nyingine za fedha, huku akiwaasa wananchi wanaokopeshwa kurejesha kwa wakati ili kutoa fursa kwa wengine kupata mikopo hiyo.

"Ingawa baraza kwa kushirikiana na mifuko hiyo ya kifedha inafanya vizuri, lakini taasisi za kifedha ziendelee kutoa mikopo yenye riba nafuu ili wakopaji waweze kumudu kurejesha kwa wakati," alisema Mhagama.

Katibu Mtendaji wa baraza hilo, Beng'i Issa, alieleza kuwa baraza limekuwa likiratibu maonyesho ya wajasiriamali kupitia mifuko ya kifedha kikanda kwa miaka mitatu sasa ili kusaidia kuwaunganisha na fursa na masoko yaliyopo.

Issa alisema mbali na hilo, baraza kupitia mifuko hiyo imeweza kusaidia wajasiriamali kukuza ueleza juu ya vigezo vya upatikanaji wa huduma za mitaji na kuwekeza katika miradi yenye tija ambayo itawasaidia kukuza pato lao na la taifa.

Nao baadhi ya wajasiriamali waliowezeshwa na mifuko hiyo, Emanuel Paschael, Mary Joseph na Happy Msuya waliishukuru serikali na mifuko hiyo kwa kuwapatia mikopo ambayo kwa sasa inawasaidia kuendesha shughuli zao ya ujasiriamali wenye tija.

# Kampeni yaanza CCM kurejesha majimbo 2

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kilombero mkoani Morogoro, kimezindua kampeni ya kurudisha majimbo mawili ya uchaguzi ambayo yanaongozwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

Majimbo hayo ni Kilombero na Mlimba. Kilombero linaongozwa na Peter Lijualikali wakati Mlimba linaongozwa na Susan Kiwanga ambao waliyachukua katika uchaguzi wa mwaka 2015 baada ya kugawanywa lilikuwa Jimbo la Kilombero likishikiliwa na CCM.

Akizindua kampeni hiyo, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, Mch. Getrude Rwakatare, alisema kutokana na utekelezaji wa Ilani ya chama hicho uliofanywa na Rais John Magufuli, wananchi wamerudisha imani na chama hicho na hakuna sababu ya kuongozwa na wapinzani.

Rwakatare ambaye alikuwa akizungumza na viongozi wa chama hicho katika tarafa za Mgeta na Ifakara na kuwakabidhi baiskeli 300 kama sehemu ya vitendea kazi, alisema kilichobaki ni ushirikiano wa viongozi hao kushawishi wananchi.

Alisema kilichosababisha CCM kupoteza majimbo hayo ni baadhi ya wanachama kuwa na tamaa na uchu wa madaraka, hivyo kuwapa nafasi wapinzani kuwashawishi wananchi kuwapigia kura.

Alisema CCM imeona makosa hayo na kujipanga upya ikiwamo kutoa msaada huo ili kurahisha utendaji kwa kuanzia katika uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu mwakani.

"Kila katibu kata na katibu tawi watapata baiskeli hizi nilizotoa leo kwa ajili ya shughuli ya chama kwenda hapa na pale," alisema.

Naye Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kilombero, Clarence Dismas, alisema utendaji wa serikali umerudisha moyo kwa wananchi ikilinganishwa na miaka ya nyuma na kusababisha upinzani kuchukua nafasi katika wilaya hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, James Ihunyo, aliwapongeza wananchi wa wilaya hiyo kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika daftari la wapigakura na kuwataka kutofanya makosa kuchagua viongozi wabovu.



Baadhi ya wazazi na walezi waliojitokeza kuhudhuria chanjo ya surua, rubella na polio inayotolewa kwa watoto wenye umri wa miezi 9 hadi miaka mitano katika Kituo cha Afya Buzuruga jijini Mwanza jana, wakiwa wamepanga foleni huku wengine wamekaa chini baada ya kusimama kwa muda mrefu. **PICHA: ELIZABETH FAUSTINE**

# 'Kangomba' kusakwa usiku na mchana

**Na Hamisi Nasiri, MTWARA**

MKUU wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, amewataka wakuu wa wilaya wa mkoa huo kutumia vyombo vya ulinzi na usalama kwenye maeneo yao kuwasaka wafanyabiashara wote maarufu kama 'kangomba'.

Ameagiza kukamatwa wafanyabiashara hao wanaonunua korosho nje ya mfumo rasmi wa stakabadhi mazao ghalani kwa wakulima, na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria mara moja.

Byakanwa alitoa agizo hilo alipokuwa akizungumza na wanahabari kuhusu zao la korosho na jinsi mkoa ulivyojipanga kudhibiti ununuzi holela msimu wa 2019/2020.

Alisema wakuu wa wilaya wasisite kutumia vyombo vya ulinzi na usalama vilivyopo kwenye wilaya zao kufanya msako usiku na mchana kuwasaka watu wote wanaonunua korosho kinyume cha sheria au utaratibu.

Byakanwa alieleza kuwa baadhi ya 'kangomba' wameanza kuzunguka zunguka vijijini kwa wakulima kwa ajili ya kununua korosho kwa bei ya Sh. 1,000 kwa bakuli moja yenye ujazo wa zaidi ya wastani wa zaidi ya kilo.

Alisema wakuu hao wa wilaya watumie muda wao kwenda vijijini kuwakamata na kuwafikiasha kwenye vyombo vya sheria wanunuzi hao haramu.

Alisema serikali katika msimu huu wa korosho imejipanga madhubuti kupambana na 'kangomba' ambao wamekuwa na tabia ya kuwalangua wakulima.

Alisema kwa sasa 'kangomba' wanadaiwa kupita kwa wakulima kununua korosho, atakayebainika atakamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Shaibu Bakari, mkulima wa korosho wilayani Nanyumbu, alisema wakulima wameshaanza kukusanya korosho kutoka shambani na kupeleka kwenye vyama vya msingi.

Alisema wanaiomba serikali kuharakisha minada ya korosho ili wakulima waweze kuuza mapema.

Fatuma Hassan, mkulima wilayani Masasi, alisema wanunuzi wote ambao watanunua wahakikishe wanawalipa wakulima kwa wakati kama utaratibu unavyotaka.

HABARI KIMATAIFA

# Wakatoliki waandamana, kisa ufisadi

**KINSHASA,** Congo

WAKRISTO wa Kikatoliki katika Jamuhuri ya Kidemokrasi ya Kongo (DRC) wamefanya maandamano katika maeneo mbalimbali nchini humo kupinga ufisadi.

Maandamano hayo ambayo yaliitishwa na Kamati ya Katoliki ya Walei ambao waliwataka Raia wa Congo kuingia mitaani kupinga vitendo vya ufisadi na ukosefu wa hai za kisheria.

Walei ambao ni wakristo wa kawaida DRC wanaaminiwa kuwa ndio waliomshinikiza aliyekuwa Rais wa nchi hiyo, Joseph Kabila kuacha azma yake ya kugombea muhula wa tatu madarakani.

Hii ni mara ya kwanza kwa Kamati ya Walei kuitisha maandamano chini ya utawala wa Rais wa sasa, Felix Tshiseledi.

Wakatoliki waliitisha maandamano hayo ya amani baada ya kupotea kwa dola milioni 15 kutoka Benki ya Taifa ya DRC na kuwekwa katika benki ya biashara kabla ya kutoweka kabisa.

**Walei wa Kikatoliki pia waliwatolea wito wananchi waliosita kuchukua uamuzi unaofaa kwa sababu mapambano dhidi ya matatizo haya ni suala la kitaifa.**

Licha ya kilio cha wananchi ambao uliwataka wahusika wachukuliwe hatua, Rais Tshisekedi wala mahakama hawajatoa maelezo ya kutosha kwa umma juu ya sakata hiyo.

Wakatoliki hao walieleza kuwa wanakataa mtindo wa kutokomeza rushwa uliotawala katika tawala zilizopita.

Walei wa Kikatoliki pia waliwatolea wito wananchi waliosita kuchukua uamuzi unaofaa kwa sababu mapambano dhidi ya matatizo haya ni suala la kitaifa.

Awali Gavana wa Mji wa Kinshasa, Gentiny Ngobila, pamoja na Kamati ya Uratibu ya Walei (CLC) walikubaliana kusitisha maandamano hayo mjini Kinshasa ili kuzuwia, yasifanyika Oktoba 19 Jumamosi ambayo ni siku ya ilipofanyika operesheni Kin Bopeto.

Hata hivyo, maandamano hayo yaliendelea katika maeneo mengine ya nchi kama ilivyopangwa.

Akizungumza na Shirika la Utangazaji la BBC mmoja wa viongozi wa Wakatoliki hao, Isidore Ndaywele Nziem alisema kuwa wanakerwa na ufisadi uliokithiri, ukiukaji wa sheria kwa kutowaadhibu wahalifu na kudorora kwa mfumo mzima wa sheria nchini humo.

Kamati ya Walei wa Kikatoliki DRC (CLC) imevipongeza vyama vya kisiasa, makundi ya raia, mashirika yasiyo ya kiserikali waliopaza sauti zao kuunga mkono maandamano hayo.

Katika taarifa yake CLC iliwataka wananchi kutojihusisha na aina yoyote ya ghasia, kuchoma magurudumu, na kuweka vizuizi vya barabarani, kutotumia lugha ya matusi, kutorusha mawe na vitu vingine au kufanya uporaji wowote wa mali wakati wa maandamano hayo.

Wanasema wanataka kutumia kusanyiko hilo kama mfano wa kutumia uhuru kwa uwajibikaji ili kuijenga jamii ambayo ni bora kuishi.

Si mara ya kwanza kwa Kanisa Katoliki kuitisha maandamano nchini humo kupinga kile ambacho linaona kuwa hakifai kwa jamii ya Wakongomani.

Mwanzoni mwa mwaka jana Maaskofu wa Kanisa hilo nchini humo waliitisha maandamano dhidi ya Rais Kabila, kumshinikiza aondoke madarakani na kutangaza kuwa hatawania urais katika uchaguzi wa mwaka 2018.

Mwishoni mwa mwaka 2017 kanisa hilo nchini DRC pia liliitisha maandamano yaliyosababisha vifo vya waandamanaji saba baada ya makabiliano kati ya polisi na waandamanaji.

Polisi wa kupambana na ghasia walikabiliana na waumini wa kanisa hilo waliokuwa wamemaliza ibada ya kuwaombea waumini waliouawa na kusababisha baadhi yao kujeruhiwa kwa hofu kuwa wangeandamana jijini Kinshasa.

Maaskofu wa Kanisa Katoliki wakati huo walisema, hawatachoka kushinikiza mabadiliko nchini DRC, na kumshinikiza Rais Kabila ambaye alikuwa madarakani tangu mwaka 2001.

Ufaransa inaamini kuwa maandamano hayo na msukumo wa walei wa Kikatoliki ni mojawapo ya sababu zilizomsukuma Rais mstaafu Kabila kusitisha nia yake ya kugombea muhula wa tatu madarakani. **BBC**

## Wanasayansi watafuta dawa ya saratani

**LONDON,** Uingereza

WANASAYANSI wa Uingereza na Marekani wameungana kutafuta dalili za mapema za ugonjwa wa saratani katika juhudi za kugundua na kutibu kabla ya kujitokeza.

Wataalamu hao wanapanga kuzalisha saratani katika maabara ili kubaini mwonekano wake siku ya kwanza.

Hii ni moja ya tafiti zinazopewa kipaumbele na muungano huo wa kimataifa wa wanasayansi wanaofanya shughuli za ugunduzi wa mapema wa saratani.

Kufanya kazi pamoja katika mradi huo kunamaanisha watu wanaougua saratani watafaidika zaidi.

Kwa pamoja wanasayansi hao wanalenga kufanya uchunguzi kama vile wa damu, pumzi na kupima mkojo ili kuwabaini wagonjwa walio katika hatari zaidi, kuimarisha mbinu ya ugunduzi wa mapema wa saratani na kuangazia kwa jumla dalili zisizonekana za ugonjwa huo.

Lakini wamekiri kuwa hatua hiyo ni kama kutafuta sindano gizani na huenda ikachukua miaka 30.

Watafiti kutoka jijini Manchester Uingereza wanakuza tishu za matiti ya binadamu kwenye maabara na seli za kinga za synthetic ili kuona ikiwa wanaweza kuona mabadiliko ya mapema kabisa, ambayo yanaweza kusababisha saratani.

Prof. Rob Bristow anasema ni sawa na kuwa na tishu hai inayoishi nje ya mwili wa mgonjwa.

Wanasayansi hao wanasema, utafiti kuhusu ugunduzi wa mapema wa ugonjwa huo umefanywa kwa kiwango kidogo na kwamba changamoto inayotokana na ukosefu wa kufanyia majaribio matokeo ya utafiti kwa watu wengi imerudisha nyuma juhudi za kufikia tiba kamili. **BBC**



Mwana wa Mfalme Harry akiwa na mke wake Meghan. **PICHA: REUTERS**

## Prince Harry na Meghan wayakataa magazeti ya udaku

**LONDON,** Uingereza

MWANA Mfalme, Prince Harry na mkewe wamesema kuwa hawatakubali magazeti ya udaku ya Uingereza kuharibu maisha hao.

Harry aliyasema hayo wakati akifanya mahojiano na kituo cha Televisheni cha ITV wakati wa ziara yao nchini Afrika waliyoifanya Oktoba.

Prince Harry aliiambia ITV kuwa mengi ya mambo ambayo yanachapishwa katika magazeti ya udaku siyo ya kweli, akiongeza kuwa hatokubali kuingizwa katika hujuma iliyomuua mama yake.

Alisema kumbukumbu ya kifo cha Princess Diana ilikuwa bado anakikumbuka kila siku kunavyokucha na sio kwamba yeye mwenyewe amejawa na hofu.

Nyota wa zamani wa Televisheni ya Marekani, Meghan Markle alisema wakati rafiki zake walikuwa na furaha ya yeye kuwa na mahusiano na Harry.

Alisema marafiki zake wa Uingereza walimwonya kuwa asiolewe na Harry kwa sababu magazeti ya udaku ya Uingereza yatamuharibu maisha yake.

Akizungumza namna anavyoweza kukabiliana na ufuatiliaji mzito wa magazeti haya, Meghan amejibu: "Ukweli ni kuwa nimekuwa kwa muda mrefu nikimwambia H – hivyo ndivyo ninavyomwita, haitoshi kuwa utanusurika katika jambo, hiyo siyo maana ya maisha. Inatakiwa upate mafanikio".

Mapema mwezi huu wana wa mfalme hao walifungua mashtaka dhidi ya gazeti la udaku la Uingereza, The Mail on Sunday kwa kuingilia maisha yao ya faragha, akidai kuwa kinyume cha sheria walichapisha barua aliyomwandikia baba yake. Kila wakati, Harry alisema namna wanavyomfanyia Meghan hakuna tofauti na vile magazeti hayo yalivyomfanyia mama yake. **VOA**

# Wakutana kuandaa ajenda mkutano mawaziri SADC

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MAKATIBU wakuu wa sekta na maofisa waandamizi wa wizara zinazoshughulika na mazingira, maliasili na utalii wamekutana jijini Arusha kwa ajili ya kuweka ajenda za mkutano wa mawaziri wa sekta husika kwa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Miongoni mwa mambo yanayojadiliwa katika kikao hicho cha awali ni mpango mkakati wa pamoja wa kukabiliana na ujangili kwa nchi za SADC, hoja inayopaswa kuungwa mkono na nchi wanachama.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Adolf Mkenda, amesema nchi moja ni vigumu kupambana na ujangili, hivyo kuna haja ya nahitaji kuunganisha nguvu kwa nchi zote ili kufanikisha juhudi za kupambana na ujangili.

"Tunahitaji kuwa na mpango mkakati wa kukuza utalii katika nchi za SADC, hii ni moja kati ya ajenda muhimu zitakazojadiliwa," alisema Prof. Mkenda.

Mkurugenzi wa Idara ya Chakula, Kilimo na Maliasili kutoka Sekretarieti ya SADC, Domingos Zephania Gove, alisema wanahitaji kutembea pamoja kama nchi za SADC katika kuweka mikakati kwenye masuala ya mazingira, utalii na wanyamapori.

Gove alisema wanahitaji kuthibitisha programu za pamoja za kukuza utalii na kusimamia maliasili katika ukanda husika.

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhandisi Joseph Malongo, alisema watajadili mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa pamoja.



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) Taifa, Freeman Mbowe na viongozi wengine wa chama hicho, wakitoka kusikiliza kesi inayowakabili katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Maofisa Ustawi Jamii walivyookoa mil. 6.5/-

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAOFISA Maendeleo ya Ustawi wa Jamii nchini, wameokoa Sh. milioni 6.5 za ujenzi wa vyumba vitatu vya maabara vya Shule ya Sekondari Iyumbu jijini Dodoma, baada ya kushiriki ujenzi wa kumwaga jamvi.

Ujenzi huo ambao ulianza Desemba 2018, unatarajia kukamilika mwakani ili wanafunzi waliochukua mchepuo wa sayansi waanze kuvitumia kwa mafunzo kwa vitendo.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Jamii katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Patrick Golwike, alisema kazi ya maofisa na wataalamu wa maendeleo ya jamii na sio kutoa mikopo peke yake bali kusimamia miradi ya maendeleo kiufanisi inayotekeelezwa na serikali.

Aliwataka maofisa hao kutambua wajibu wao ili kuhakikisha miradi ya maendeleo inafanyika kikamilifu.

"Moja ya kazi za maofisa maendeleo ni pamoja kusimamia miradi, hivyo ni lazima tuamshe ari kwa wananchi kushiriki katika miradi ya maendeleo," alisema Golwike.

Alisema wao kama Chama cha Maofisa Maendeleo nchini (CODEPATA) kabla ya mkutano mkuu, wameamua kushiriki kiwamo kutoa mifuko 120 ya saruji ambayo imesaidia kuweka jamvi katika vyumba hivyo na maabara.

Alisema lengo lao ni kuona kila mwananchi anatambua umuhimu wa miradi ya maendeleo ambayo inaanzishwa na wao wanasaidia kuiendeleza.

Akitoa taarifa ya ujenzi wa vyumba vya maabara, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Iyumbu, Vicent Leo, alisema ujenzi huo ulianza Desemba 2018,wakiwa na lengo la kukidhi mahitaji ya wanafunzi katika masomo ya sayansi.

Alisema ujenzi wa shule hiyo utasaidia kupunguza adha ya wanafunzi kutembea kilomita 24 kwenda Shule ya Sekondari Kisasa kujifunza kwa vitendo.

"Tunawashukuru maofisa maendeleo kwa kujitokeza kuchangia ujenzi wa vyumba vya maabara,tunaomba na wengine wafanye hivyo," alisema Leo.

Alisema wanaamini pamoja na nguvu kazi ya wananchi wa eneo hilo na wadau wanaojitokeza vyumba hivyo hadi kufikia mwakani vitakuwa vimekamilika.

Naye Ofisa Tarafa wa Wilaya Dodoma, Neema Nyalege ambaye aliyemwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, aliwapongeza maofisa maendeleo kutokana na jitihada walioonyesha katika kuchangia maendeleo kwenye ujenzi huo.

Alisema vyumba vya maabara katika sekondari ni muhimu hivyo ni vema wananchi kwa kushirikiana na wadau kuamka kufanya shughuli za maendeleo hususani za ujenzi wa vyumba hivyo ambavyo ni muhimu kwa wanafunzi kusoma kwa vitendo.

## Waziri aeleza mikakati ya kuboresha sekta kilimo

**Na Mathias Canal**

SERIKALI imesema inatekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) ambayo ni utekelezaji wa Mpango wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo nchini (TASFIP) unaolenga kukuza kilimo kwa asilimia 6 kwa mwaka.

Imesema kwa kuzingatia hatua hizo, Wizara ya Kilimo imekusudia kuleta mageuzi ya kilimo kutoka mtazamo uliopo wa kilimo cha kujikimu hadi kufikia uendeshaji wa kilimo kwa mfumo wa kibiashara.

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, aliyasema hayo jana wakati akizungumza kwenye ufunguzi wa programu ya kuimarisha uzalishaji, kuongeza thamani pamoja na uzalishaji bora wa mazao ya viungo katika Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro.

Hasunga (pichani) aliyataja maeneo ambayo yanahitaji utekelezaji wa haraka akisema la kwanza ni utekelezaji wa azma ya serikali kuendeleza kilimo kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) kwa kusimamia thabiti nguzo ya programu hiyo ikiwamo usimamizi endelevu wa matumizi ya maji na ardhi.

Alisema lengo la ASDP II ni kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo ili kuongeza uzalishaji na tija, kilimo cha kibiashara, kuongeza pato kwa wakulima hivyo ni lazima kuwekwa mkakati madhubuti wa utekelezaji ili kufikia nalengo yaliyokusudiwa.



Vilevile, alisema serikali imekusudia kuboresha mazingira wezeshi, uratibu, ufuatiliaji na tathmini katika sekta ya kilimo, hivyo wataalamu katika Wizara ya Kilimo wanapaswa kuongeza kasi ya uwajibikaji ili kutimizi azma hiyo.

Alisema wizara itaweka mkakati madhubuti wa kuhakikisha kuwa bei ya mazao inaimarika huku akisisitiza kuwa kwa ushirikiano na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji atahakikisha wakulima wanapata masoko ya mazao yao.

Alisema kuwa Wizara ya Kilimo imetayarisha Mkakati wa Taifa wa miaka 10 wa Usimamizi wa Mazao baada ya kuvunwa.

Alisema kuwa mkakati huo umeandaliwa ili kuendana na malengo endelevu ya Dunia ya kutokomeza njaa ifikapo 2030, kuhakikisha usalama wa chakula na lishe na kukuza kilimo endelevu kama lengo la pili la Umoja wa Mataifa kati ya malengo 17.

Mkakati huo utakuwa mwongozo kwa sekta za umma na binafsi katika kukabiliana na changamoto ya upotevu wa mazao baada ya mavuno. Aidha, mkakati huo umezingatia mabadiliko yanayoendelea ya kitaasisi na kisera.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD, MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD** tutauza kwa mnada wa hadhara nyumba za wadaiwa sugu zilizopo Bunda, SCOLA MLINDA RUBEN (mnada-05/11/2019), JACKSONI SANAWA MAIGE (mnada 06/11/2019), MUSSA JIJA ISONZO (mnada 07/11/2019). Lengo ni kufidia/kupunguza deni la mkopo wanalodaiwa. Mnada utafanyika Tarehe kama zilivyo mbele ya majina na mahali dhamana zilipo. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD : 0744594358 BUNDA Office: 0717065445/0767340054**

215471002

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**AGNESS T. NKIMA** anatangaza kupotea kwa result slip yenye index namba P0798-0501 iliyotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2019 katika shule ya Sekondari Korogwe Teachers Collage Center.
Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa: KOR/RB/6482/2019**

215470402

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu : +255 26 2324455
Fax: 255 26 2323233
Barua pepe : ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,

40470 Dodoma

21/10/2019.

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumanne tarehe **22/10/2019** Kampuni ya **Mussa holdings** itapitisha gari lenye vipimo vya tofauti kutoka Moshi kuelekea Kingori. Gari lenye namba za usajili T277ALQ.
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:-
   Urefu - 9.7
   Upana - 3.0
   Kimo - 3.0
3. Njia itakayotumika ni Moshi hadi Kingori kupitia Bomangombe –Kia gari litasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:00jion)

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

215470902

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO…OF 2019**
**In the matter of the Estate of the late JOSEPH ALPHONCE TARIMO**
**AND**
**In the matter of the Application for letters of Administration by**
**EDITHA EMILY MARANDU AND ERICK JOSEPH TARIMO**

**GENERAL CITATION**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit on 23rd day of SEPTEMBER, 2019 before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner. Objections to the grant should be filed on or before 01st day of OCTOBER, 2019. The will of the said deceased is deposited and open for inspection of the court.
Date: 23 Day of 9….2019.

IN THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL
FOR RUNGWE
AT TUKUYU.
MISC.APPLICATION NO. 58 OF 2018
(from Misc.Application no.58/2017)
JOSEPH ANYELWISYE...................APPLICANT
VERSUS
FREDRICK MWAIPUNGU.........RESPONDENT

DRAWN ORDER

WHEREFORE,the Applicant prays for the following order against the respondent that;
The rulling in misc.Application no. 58/2017 be reviewed as to costs.

This matter is coming for rulling on 14/03/2019 before Majengo Chairman in presence of Applicant's Representative.

THIS TRIBUNAL DOTH HEREBY ORDER THAT;
1. This matter is granted, the applicant will his costs in the said misc.Application no. 58/2017
2. The respondent is condemned to pay costs of this matter.

Given Under My Hand and Seal of this Tribunal,
this 14 day of March, 2019.

215470202

## KUPOTEA KWA KADI

**MOHAMED ENTERPRISES (T) LTD** anatangaza kupotea kwa kadi tano za pikipiki aina ya BAJAJ –BOXER zenye usajili wa namba zifuatazo MC 357 CHC, MC 813 CFL,MC 464 CGD, MC 971 CDY, MC 665 CCY.

Yeyote atakaezionа hizi kadi atoe taarifa kituo chcochocte cha Polisi.

Polisi Taarifa:
DAR/CEN/RB/851013/2013

115470302

## KUPOTEA KWA KADI

MOHAMED ENTERPRISES (T) LTD anatangaza kupotea kwa kadi tano za pikipiki aina ya BAJAJ –BOXER zenye usajili wa namba zifuatazo MC 357CHC, MC 813CFL,MC 464CGD, MC 971CDY, MC 665CCY.

Yeyote atakaeziona hizi kadi atoe taarifa kituo chcochocte cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**DAR/CEN/RB/851013/2013**

115470302

## KUPOTEA KWA KADI

**MOHAMED ENTERPRISES (T) LTD** anatangaza kupotea kwa kadi tano za pikipiki aina ya BAJAJ –BOXER zenye usajili wa namba zifuatazo MC 680CFK,MC 483CFF,MC 201CGA, MC 151CGA, MC 148CFKC.
Yeyote atakaeziona hizi kadi atoe taarifa kituo chcochocte cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**DAR/CEN/RB/851013/2013**

115470302

*Uza,*
*Chenye Thamani*
*Kubwa Kwa Kutangaza*
*Nasi Kwa Bei Poa*
*Tupigie 0767 223311*

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie
0767 223 311

Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO

# LAMPARD: GIROUD SAHIHI KUKOSA FURAHA CHELSEA



**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard anajiandaa kuzungumzia majaliwa ya Olivier Giroud ya dirisha dogo la Januari kama mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa bado hana furaha kwa kutopata nafasi nyingi zaidi za kucheza.

Huku Tammy Abraham akiwa ndio chaguo la kwanza la Lampard kwenye safu ya ushambuliaji msimu huu, hiyo inamaana kwamba, Giroud amekuwa hana nafasi ya kuanza na aliingizwa akitokea benchi katika mechi mbili za Ligi Kuu.

Akizungumza wakati akiwa na Ufaransa kwenye mechi za kimataifa wiki iliyopita, Giroud alisema atajiandaa kuondoka klabuni hapo kama hatapewa nafasi ya kucheza.

Lampard anaelewa mkanganyiko wa mchezaji huyo wa zamani wa Arsenal na akikubali kwamba, hatakiwi kumwangalia zaidi Abraham kwa kuwekwa kama chaguo la kwanza.

"Nilikuwa na mazungumzo mazuri na Oli kabla hajaondoka na mara zote nawaheshimu wachezaji, lakini hasa kwa wachezaji ambao wapo kwenye miaka ya mwanzoni mwa 30," amesema Lampard.

"Alionekana hayupo sawa wakati alipozungumza na mimi na pia aliponukuliwa akiwa na timu ya Taifa ya Ufaransa.

"Hakutakiwa kutokuwa na furaha na kukubali kwa kutopata nafasi ya kucheza. Hivyo ndivyo wachezaji wazuri wanavyofanya. Nafikiri kama nilivyosema kwa Oli, atapata nafasi ya kucheza."

# Ozil: Hata iweje siondoki Asernal

**LONDON,** England


MESUT Ozil amesisitiza kwamba, hana mpango wa kuondoka Arsenal kwa siku za karibuni na atabaki kwenye timu hiyo hadi mkataba wake utakapofika tamati hata kama Kocha Unai Emery ataendelea kumpiga benchi.

Tangu kwenye dirisha lililopita la majira ya joto, Ozil alihusishwa na mpango wa kuachana na timu hiyo ya Emirates kabla ya sasa kwenye kipindi hiki cha kuelekea usajili wa dirisha la Januari, jina la nyota huyo likitajwa tena kwamba anaweza kuachana na Arsenal.

Kuna sababu nyingi zinazomfanya Ozil kung'ang'ania Arsenal hata kama hachezi.

Kwanza ni ule mshahara wake wa pauni 350,000 kwa wiki, lakini pili ni vile alichokishuhudia ndani ya miaka kadhaa kwenye kikosi hicho, ambapo mara zote wale wachezaji waliokuwa wakitamba ndani ya jezi za Arsenal walikwenda kuwa wepesi na wa ovyo walipohamia timu nyingine.

Ozil hataki limkumbe hilo, anasubiri 'azeekezeeke' kwanza.






# *Mourinho: Klopp kataka nyama, akapewa samaki*

**MANCHESTER,** England

JOSE Mourinho amesema kwamba, Jurgen Klopp "hakukipenda chakula alichoandaliwa" wakati timu yake ya Liverpool ilipocheza na Manchester United, juzi Jumapili.

Mourinho alisema: "Klopp alipenda nyama na akapewa samaki," kwa hiyo hakufurahi.

Klopp alidai kwa miaka minne aliyokuwa Liverpool, timu hiyo ya Old Trafford imekuwa na tabia ya kucheza soka ya kujilinda kila wanapokutana.

Adam Lallana alisawazishia Liverpool katika sare 1-1 dhidi ya Manchester United kwenye Uwanja wa Old Trafford Jumapili pamoja na vinara hao kuendeleza rekodi ya kutokufungwa katika Ligi Kuu England.

Sare hiyo inaifanya Liverpool kuongoza ligi kwa tofauti ya pointi sita kwa mabingwa watetezi Manchester City.

Klopp alidai kwa miaka minne aliyokuwa Liverpool, timu hiyo ya Old Trafford imekuwa na tabia ya kucheza soka la kujilinda kila wanapokutana.

Klopp alisema: "Tumepata pointi inatosha. Tangu nilipotua England, Man United wamekuwa wakicheza kwa mtindo huu. Kila mmoja anajianda kwa ajili ya mchezo, lakini timu moja inajipanga kwa kazi moja tu kujilinda. Hatujapoteza chochote, tumepata pointi, wacha maisha yaendelee."

Baada ya kauli hiyo ya Klopp, kocha wa zamani wa Man United, Jose Mourinho aliyefundisha timu hiyo ya Old Trafford kuanzia 2016 hadi 2018 - alimjibu kocha huyo wa Liverpool.

Mourinho alisema: "Hakupenda chakula alichoandaliwa. Alitaka nyama, akapewa samaki.

"United iliingia uwanjani na mbinu ya kupanga ukuta mgumu uliokuwa na wakabaji watano, ilikuwa ngumu kupita," alisema Mourinho.

# Tottenham inampigania Pochettino - Alderweireld

**LONDON,** England

BEKI wa Tottenham, Toby Alderweireld amesisitiza Spurs bado "wanampigania" kocha wao, Mauricio Pochettino wakati klabu hiyo ikipitia kwenye wakati mgumu kwa sasa.

Spurs walilazimishwa sare ya kufungana bao 1-1 na Watford Jumamosi, na kukiacha kikosi hicho cha Pochettino bila ushindi katika mechi tatu kwenye mashindano yote.

Majaliwa ya Pochettino yamezua maswali hapo Tottenham huku sasa ikiwa nafasi ya saba kwenye msimamo, huku pia wakiwa walifungwa mabao 7-2 na Bayern Munich kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kabla ya mapumziko ya mechi za kimataifa.

Hata hivyo, Alderweireld amesema Spurs ipo nyuma ya Pochettino, ambaye aliiongoza Tottenham kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

"Kuna timu uwanjani na unaona sisi tukipigana," amesema mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji, Alderweireld.

"Kila mmoja yupo nyuma ya klabu na kocha, vinginevyo tusingeweza kujituma na kupigana uwanjani kama tunavyofanya."

Alderweireld aliongeza: "Nafiriki hatukufanya maamuzi sahihi. Na mwisho wa siku walikuwa na mpira mrefu ambao ukawafanya wafunge bao. Ni vigumu, si hasi, lakini kipindi cha pili tulibadili mchezo.

"Tulifanya mengi mazuri. Tungeweza kufunga mabao mengi. Tunahitaji kuimarika na kuimarika zaidi. Ni wachezaji wale wale wa msimu uliopita na tunatakiwa kuondoka kwenye hali hii."

Tottenham itacheza na Red Star Belgrade leo Jumanne kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.






# BALE, MODRIC KUIKOSA GALATASARAY UEFA LEO

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane amewaacha Gareth Bale na Luka Modric kwenye kikosi cha Real Madrid kilichosafiri kwenda kucheza na Galatasaray kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kuumia kwenye mechi za kimataifa.

Madrid itakuwa dimbani leo Jumanne kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Galatasaray.

Baada ya kufunga wakati Wales ikitoka sare ya kufungana bao 1-1 na Croatia mjini Cardiff, Bale aliondoka uwanjani akiwa anachechemea na baadaye iliripotiwa kwamba aliuumia, wakati Modric alitolewa nje baada ya kuumia wakati akiichezea nchi yake ya Croatia.

Wawili hao wanaungana na mshambuliaji, Mariano Diaz ambaye ameumia kigimbi na Lucas Vazquez ambaye pia ni majeruhi.

Los Blancos walipoteza kwenye mchezo wao wa kwanza kwa mabao 3-0 kutoka kwa Paris Saint-Germain na walilazimishwa sare ya kufungana mabao 2-2 na Club Brugge pale kwenye dimba la Santiago Bernabeu, na kuwaacha wakishika mkia kwenye kundi lao.

Mchezo wa leo Jumanne unawapa nafasi vijana hao wa Zidane nafasi ya 'kufufuka' baada ya kukumbana na kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Mallorca kwenye La Liga Jumamosi na kocha wa Madrid, Zidane atakuwa akitegemea kupata huduma ya Toni Kroos, Eden Hazard na Dani Carvajal.

# Klopp: Utd walijilinda tu

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp ameijia juu Manchester United kwa sababu anaamini walijiandaa kwa kulinda tu kila wanapocheza na Liverpool baada ya sare ya Jumapili ya kufungana bao 1-1 katika Uwanja wa Old Trafford.

Liverpool ilifanikiwa kupata pointi moja kuweza kuendeleza rekodi ya kutopoteza mchezo kwa bao la dakika za majeruhi la kusawazisha la Adam Lallana, akifuta lile la Marcus Rashford.

Bao la Rashford liliibua utata wakati Liverpool walikuwa wakiamini kwamba, Divock Origi alifanyiwa madhambi na Victor Lindelof, lakini liliruhusiwa baada ya mapitio ya teknolojia ya usaidizi wa maamuzi kwa njia ya video, VAR.

Vinara wa ligi hiyo, Liverpool walikuwa na mchezo mzuri na walimaliza wakiwa na takwimu ya umiliki wa mpira kwa asilimia 68, ingawa walipiga mashuti mara tatu langoni kwa wapinzani wao.

Bado Klopp, ambaye alisisitiza hilo halikumsumbua, hangeweza kuisaidia kuweza kupata ushindi kwa mfumo wa United.


"Hainichanganyi," alisema. "Mimi si mtu ambaye huwa naangalia na kufikiria zaidi kuhusu staili.

"Ni ukweli kwamba, wakati tunakuja hapa, huwa wanalinda tu. Ni sawa, hakuna shutuma, ndio ukweli.

"Wakati United inapocheza dhidi ya Liverpool, mara zote unaweza kufikiri timu zote zitacheza kwa staili hii."



# DONDO SOKA
## MAGAZ LAYA



# GUARDIOLA: CITY HAIJAWA TAYARI UBINGWA WA UEFA

**Watu wanasema kuhusu Ligi ya Mabingwa, lengo hilo bado hatujawa tayari...**

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER City bado haijawa tayari kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, kwa mujibu wa Kocha Pep Guardiola.

**City ilijibu kipigo cha mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Wolves kabla ya mapumziko ya mechi za kimataifa kwa kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Crystal Palace Jumamosi.**

Mabingwa mara mbili mfululizo wa Ligi Kuu, City wapo pointi sita nyuma ya vinara ambao hawajapoteza hata mechi moja kwenye ligi hiyo msimu huu Liverpool, kuelekea mchezo wao wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Atalanta.

Baada ya kutawala soka la England, City ina matumaini ya taji hilo la Ulaya, lakini Guardiola anaamini timu yake haijakaribia kuweza kubeba ubingwa huo wa Ligi ya Mabingwa.

"Watu wanasema kuhusu Ligi ya Mabingwa, lengo hilo. Bado hatujawa tayari," alisema Guardiola, ambaye kikosi chake cha City kilipoteza katika kila mechi ya robo fainali ya misimu miwili iliyopita.

"Tulitengeneza sana, hatukuruhusu bao, lakini inaweza kujizatiti. Tumefunga sana kwa misimu miwili iliyopita na sina hofu kuhusu hilo, lakini tunapaswa kuendelea, kufanyia kazi hilo."

Gabriel Jesus alifunga katika ushindi huo walioupata kwenye Uwanja wa Selhurst Park, ambapo mshambuliaji huyo wa Brazil bao lake hilo likiwa la 50 kwake katika kikosi cha City tangu alipotua hapo akitokea Palmeiras mwaka 2017.

"Yeye [Jesus] atakuwa na muda mrefu wa kucheza na kwa akili yake mara zote atakuwa na mafanikio. Ni ni mwenye njaa, atakuwa mshambuliaji muhimu duniani na tuwenye bahati kuwa naye," Guardiola alisema.

"Gabriel mara zote alikuwa mzuri kuanzia mwanzoni. Kwa bahati mbaya alikuwa na majeraha mawili makubwa. Msimu uliopita ulikuwa mgumu kwake, baada ya Kombe la Dunia haikuwa rahisi, lakini ni imara.

"Ni namba nane kwa Brazil. Klabu ilileta mchezaji wa kushangaza, mchanga kwa bei nzuri. Moja ya usajili mzuri.

"Kushindana na Sergio [Aguero] pengine ni kitu kigumu zaidi. Sergio ni mkongwe, mchezaji mwenye hasira ya kushangaza, lakini Gabriel ni mpole.

"Ni mshindani, anakubali maamuzi na kila vipindi vya mazoezi anahaka kama mnyama, lakini ni kinda na anaweza kujizatiti."

## ZISIKUPITE

### WANUKIA REAL MADRID

REAL Madrid inamfuatilia winga wa Borussia Dortmund na England, Jadon Sancho, 19, pamoja na mshambuliaji Mnorway, Erling Braut Haaland, 19, ambaye anaichezea Red Bull Salzburg. ***(El Desmarque, via Mail)***

### KOEMAN AITAKA BARCA

KOCHA wa Uholanzi, Ronald Koeman angependa siku moja kuinoa Barcelona na ana kipengele katika mkataba wake kinachoziruhusu klabu kumchukua baada ya michuano ya Euro 2020, kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Soka wa Shirikisho la Soka la Uholanzi, Nico-Jan Hoogma. ***(Fox Sports, via Marca)***

### SOLSKJAER AMTAKA WERNER

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer anavutiwa na kumsajili mshambuliaji wa RB Leipzig, Mjerumani Timo Werner, ambaye hivi karibuni amekuwa akihusishwa na Liverpool. ***(Express)***

### YAMTAKA MNIGERIA

MASHUSHUSHU wa Newcastle United wanamfuatilia mshambuliaji wa Lille na Nigeria, Victor Osimhen, 20. ***(Chronicle)***

### LAMPARD AMPOZA GIROUD

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard amesema anamtaka mshambuliaji Mfaransa Olivier Giroud, ambaye hana furaha kutokana na kukosa nafasi kikosi cha kwanza, kubaki Stamford Bridge. ***(Telegraph)***

### UNITED YAMFUATA GOMES

MANCHESTER United inajiandaa kutoa ofa mkataba mpya kwa kiungo Muingereza Angel Gomes, 19, huku Barcelona nayo ikivutiwa naye. ***(Sun)***

### AIFUNGUKIA EVERTON

BEKI wa Paris St-Germain, Thomas Meunier, 28, amesema angeweza kujiunga na Everton majira ya joto, lakini nyota huyo wa kimataifa wa Ubelgiji aliweka kando mpango huo kutokana na klabu hiyo kukosa nafasi ya kushiriki michuano ya Ulaya. ***(Het Laatste Nieuws, via Mirror)***

### NKETIAH AMPA HOFU EMERY

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery ni mwenye hofu kuhusu mshambuliaji wa England U-21, Eddie Nketiah kukosa muda wa kucheza Leeds United anayoichezea kwa mkopo. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 bado hajaanza mechi yoyote kwa timu hiyo ya Championship. ***(Mirror)***

### CHELSEA KWA MALINOVSKYI

CHELSEA imemwongeza kiungo wa Atalanta na Ukraine, Ruslan Malinovskyi, 26, katika orodha yao ya wanaotaka kuwasajili majira ya joto. ***(Express)***

### ROWETT KUINOA MILLWALL

MILLWALL imepiga hatua ya mazungumzo na Gary Rowett ambapo itashuhudiwa kocha huyo wa zamani wa Birmingham City, Derby County na Stoke City, akitua kuinoa klabu hiyo. ***(Telegraph)***

HABARI MICHEZO

# WAKENYA WANG'ARA ROCK CITY MARATHON, SERIKALI YAFUNGUKA

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI msimu wa kumi wa mbio za Rock City Marathon ukihitimishwa kwa kushirikisha mamia ya wanariadha kutoka ndani na nje ya nchi, serikali imesema ipo haja ya kufanya tathmini ili kupima mchango wa mbio za aina hiyo katika kuinua sekta ya utalii hapa nchini ili iweze kuwekeza nguvu zaidi katika kuziboresha.

**Akizungumza wakati wa kilele cha mbio hizo zilizofanyika kwenye viunga vya jengo la biashara la Rock City Mall, jijini Mwanza mwishoni mwa wiki, ambapo ilishuhudiwa wanariadha kutoka nchini Kenya wakiendelea kutamba, Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla alisema wingi wa wawashiriki kutoka ndani na nje ya nchini ni kiashirio tosha kuwa mbio hizo zikitumika vizuri kutangaza utalii zitachochea ukuaji wa sekta hiyo muhimu kiuchumi.**

"Nimeshuhudia mamia ya washiriki kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini wamekuja kushiriki mbio hizi, tayari hiyo ni sehemu ya utalii wa ndani. Zaidi imeshuhudiwa ushiriki wa wenzetu kutoka nje ya nchini ikiwamo Kenya, Rwanda na wengine nje ya Bara la Afrika nao wamekuja."

"Ili kupata mchango hasa wa mbio kama hizi kwenye Sekta ya Utalii na ukuaji wa uchumi naagiza ufanyike utafiti wa kisayansi ili serikali tujue namna ya kuziunga mkono ziendelee kufanya vizuri zaidi," aliagiza Dk. Kigwangalla ambaye alishiriki kukimbia mbio za Km. 21.

Tangu kuanzishwa kwa mbio miaka 10 iliyopita zimekuwa zikivutia zaidi washiriki kutoka mataifa ya Kenya na Rwanda ambapo ilishuhudiwa mwanariadha kutoka Kenya, Ibrahimu Too akiibuka mshindi wa mbio za Km. 42 upande wa wanaume baada ya kutumia muda wa saa 2:18:34 akifuatiwa na Wakenya wenzake Willium Koskei na John Muthui walitumia muda wa saa 2:19:06 na 2:21:30 kila mmoja.

Mtanzania pekee kwenye 10 bora wanaume alikuwa Hamis Athumani aliyefanikiwa kushika nafasi ya nne huku akitumia muda wa saa 2:21:36.

Kwa upande wa wanawake katika mbio hizo za Km. 42 ilishuhudiwa mwanariadha Elilither Tamui kutoka Kenya akiibuka mshindi baada ya kutumia muda wa saa 2:42:50 akifutiwa na Wakenya wenzake Joan Rotich (2:46:07) na Lydia Wafula (2:48:57) ambapo Watanzania Fabiola John na Zainabu Hamis walifanikiwa kushika nafasi ya sita na ya 10.

Katika mbio za Km. 21, mshindi wa kwanza upande wa wanaume ni Bernard Musau kutoka Kenya aliyetumia muda wa saa 01:11:26 akifuatiwa na Ochieng Julius kutoka Uganda aliyetumia muda wa saa 01:11:36 huku mshindi wa tatu akiwa ni Alex Nizemana kutoka Rwanda akitumia muda wa saa 01:12: 21.

Kwa upande wa wanawake katika mbio hizo za Km. 21 mshindi wa kwanza hadi wa nne wote ni kutoka Kenya ambao ni Ester Kakuri aliyetumia muda wa saa 1:21:44 , Vane Nyaboke (1:22:13), Ronah Nyabochoa (1:23:10) na Martha Njoroge (1:23:17), huku mshindi wa tano ni Grace Jackson kutoka Tanzania aliyetumia muda wa saa 1:24:23

Akizungumzia matokeo hayo Mshauri wa Masuala ya Ufundi wa mbio hizo, John Bayo pamoja na kuwapongeza wanariadha kutoka Kenya kwa kufanya vizuri alisema Tanzania haikupata ushiriki wa wanariadha wakubwa kutokana na wengi wao kushiriki kwenye mbio za kimataifa na hivyo kutoa mwanya kwa wanariadha hususan wa Kenya kuweza kutamba kwenye mbio hizo.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangalla (katikati) akitoa zawadi ya fedha taslimu kiasi cha Sh. milioni nne kwa mshindi wa mbio za Rock City Marathon Km. 42, kwa upande wa wanawake, Elilither Tamui kutoka Kenya aliyeibuka mshindi baada ya kutumia muda wa saa 2:42:50. Wengine ni pamoja na Meneja Uhusiano wa Kampuni ya Kuhifadhi Mafuta ya TIPER, Emmanuel Kondi (kulia), ambao ni miongoni mwa wadhamini wakubwa wa mbio hizo zilizofanyika mwishoni mwa wiki kwenye viunga vya jengo la biashara la Rock City Mall jijini Mwanza. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Aussems: Tupo tayari kuivaa Azam*

**Na Mwandishi Wetu**

TUMEIMARIKA! Hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Patrick Aussems, kuelekea mchezo wao dhidi ya Azam FC, unaotarajiwa kuchezwa kesho kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Aussems alisema kuwa kikosi chake kimejiandaa vema kuwakabili Azam FC na mechi za kirafiki walizocheza, zimesaidia kuwaweka imara kuwavaa wapinzani hao.

Kocha huyo alisema kwamba wamejiandaa kukabiliana na ushindani katika mchezo huo kutokana na ubora walionao wachezaji wa Azam FC.

"Tuko tayari kwa mchezo huo, ni mchezo muhimu na utakaokuwa na ushindani, Azam ni timu nzuri, tunalijua hilo," alisema kocha huyo raia wa Ubelgiji.

Kipa Beno Kakolanya, alisema kuwa licha ya kuwafunga Azam katika mechi ya Ngao ya Jamii, wamejipanga kupambana ili kuendeleza rekodi yao ya ushindi msimu huu.

"Ni kweli mechi iliyopita tuliwafunga, lakini Azam si wabaya, walitupa ushindani katika muda wote wa mchezo," Kakolanya aliongeza.

## Kocha Polisi alilia umakini

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya kupata kichapo cha mabao 5-0 kutoka kwa Zimamoto, Kocha Msaidizi wa Polisi, Awesu Maulid, amesema kufanya vibaya kwa timu yake katika mchezo huo wa Ligi Kuu Zanzibar, kumetokana na wachezaji kutokuwa makini kila wanapokuwa na mpira.

Maulid aliliambia gazeti hili kuwa pia wachezaji wake wanakosa utulivu wanapokaribia lango la wapinzani wao na hivyo kushindwa kufunga mabao.

"Tatizo letu kubwa ni kukosa utulivu, hali hii inatufanya tunakaribisha mashambulizi ya mara kwa mara katika lango letu, kama wachezaji wangekuwa wanatulia, naamini tunao uwezo wa kushinda na kukaa kwenye nafasi nzuri katika msimamo wa ligi," alisema Maulid.

Kocha huyo alisema pia safu ya ulinzi katika kikosi chake bado inacheza bila kuelewana na hapo ndipo wanaporuhusu washambuliaji kufunga kirahisi.

"Tunapata matokeo mabaya kila tukishuka dimbani, mechi yetu ya tano tulifungwa mabao 5-0 dhidi ya Mlandege, lakini pia tumefungwa 5-0 dhidi ya Zimamoto, ni matokeo mabaya sana, lakini walimu tutajitahidi ili kuhakikisha tunafanya vizuri kabla ya kwenda dirisha dogo," alisema kocha huyo.

Aliongeza kuwa wanawaandaa wachezaji wao kutokata tamaa na kuendelea kujituma kwa sababu bado ligi iko katika mzunguko wa kwanza.

## Mwambusi ageukia ubutu wa mastraika

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADA ya timu ya Mbeya City kuchabangwa mabao 2-0 na Biashara United kutoka mkoani Mara, Kocha wa timu hiyo, Juma Mwambusi amelalamikia safu yake ya ushambuliaji akidai kuwa inashindwa kutumia nafasi zinazotengenezwa.

Akizungumza baada ya mechi hiyo iliyozikutanisha kwa mara ya kwanza timu hizo katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya tangu Biashara ilipopanda Ligi Kuu, Mwambusi alisema timu yake ilitengeneza nafasi nyingi kuliko wapinzani wake.

Alisema endapo washambuliaji wake wangekuwa makini na kuzitumia vizuri nafasi zilizotengenezwa kulikuwa na uwezekano wa kupata ushindi wa mabao 4-2.

Mwambusi alisema pamoja na matokeo hayo ambayo hayakuwafurahisha mashabiki wa timu hiyo, hatakata tamaa kwa madai kuwa ana uhakika wa kufanya vizuri katika mechi zinazofuata na kurejesha furaha hiyo.

Hata hivyo, alisema timu hiyo inaendelea kutengenezwa kutokana na kuwa na wachezaji wengi wapya ambao pia ni wachanga.

Michezo
Jumanne Oktoba 22, 2019
Nipashe



'City haijawa tayari ubingwa Uefa' UKURASA 30



Mshambuliaji wa Liverpool, Roberto Firmino, akijaribu kufunga kwa kichwa katikati ya 'msitu' wa mabeki wa Manchester United kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa katika Uwanja wa Old Trafford juzi na kumalizika kwa sare ya bao 1-1. **HABARI UK. 29**

# Yanga: Mbao daraja la Pyramids Kirumba

## Zahera asema morali wa mechi hiyo ya Caf itapatikana leo wakishuka dimbani huku akiwataka...

**Na Somoe Ng'itu**

SAFARI ya kuwania ufalme wa Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajia kuendelea kwa wawakilishi pekee wa nchi waliobaki kwenye mashindano ya kimataifa, Yanga kukutana na wenyeji wao, Mbao FC katika mechi ya ligi hiyo itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, alisema wachezaji wake wako imara na tayari kwa mchezo huo ambao wanahitaji kupata ushindi ili kuongeza morali kuelekea mechi yao ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Pyramids kutoka Misri.**

Zahera (pichani), kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), alisema kila mchezaji anafahamu umuhimu wa mechi hiyo na wamejiandaa kwenda kupambana ili malengo yao ya kuondoka na pointi tatu yaweze kutimia.

"Tumejiandaa na tumejipanga vizuri, mechi itakuwa nzuri na itakuwa na ushindani, wao wanaijua Yanga, na sisi tunawajua, tutapambana ili kupata matokeo mazuri, nimewaambia kikubwa akili zao, ziwe katika mechi hii ya kesho (leo), na si mechi zilizopita," alisema Zahera.

Alisema kikosi chake kimekamilika, baada ya wachezaji wote waliokuwa kwenye timu ya Taifa (Taifa Stars), kuungana na wenzao ili kujinoa kuwakabili wenyeji wao.



Naye Mratibu wa timu hiyo, Hafidh Saleh, alisema hali ya hewa ya Mwanza ni nzuri na jana asubuhi kikosi chao kilifanya mazoezi kwenye Uwanja wa Nyamagana wakati jioni kilijifua kwenye Uwanja wa CCM Kirumba.

Aliwataja wachezaji watakaokosekana katika mchezo huo kuwa ni pamoja na Juma Mahadhi, Issa Bigirimana, Cleofas Sospeter na Mohammed Banka.

Yanga ambayo mechi yake ya mwisho ilipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Coastal Union, ina pointi nne na imecheza michezo mitatu wakati Mbao FC yenye pointi tano, imeshuka dimbani mara tano.

Ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, inatarajia kuendelea tena kesho kwa vinara, Simba ambao pia ni mabingwa watetezi kuvaana na Azam FC kwenye Uwanja wa Taifa jijini.

# Ndayiragije rasmi Stars? Aachia Azam

**Na Somoe Ng'itu**

UONGOZI wa Azam FC umemtangaza kocha wake wa zamani, Mromania Aristica Cioaba kuwa mrithi mpya wa Mrundi Etienne Ndayiragije, ambaye wameachana naye rasmi katika klabu hiyo.

Uamuzi wa Azam FC umefikia hatua hiyo baada ya kuona Ndayiragije anahitaji muda zaidi wa kukiandaa kikosi cha timu ya Taifa (Taifa Satrs), ambayo amefanikiwa kuipeleka kwenye fainali za Kombe la Mataifa Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Cioaba aliwasili nchini juzi na jana alisaini mkataba mpya wa kuanza kuitumikia timu hiyo ambayo kesho inatarajia kukutana na mabingwa watetezi katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza jana jijini, Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin "Popat", alisema wanaamini uamuzi wao utakuwa na faida kwa nchi na wanamtakia Ndayiragije mafanikio zaidi akiwa na Taifa Stars. Popat alisema Azam FC imempa mkataba wa mwaka mmoja Mromania huyo na endapo atafanya vizuri zaidi, wataendelea kuwa naye kwenye klabu hiyo.

Taarifa za ndani zinaeleza kuwa, tayari TFF ilishaanza kufanya mazungumzo na Ndayiragije, pamoja na Azam FC ambayo ndiyo ilikuwa na mkataba na kocha huyo. Imeelezwa kuwa, tangu kutimuliwa kwa Mnigeria Emmanuel Amunike, TFF imeshapokea maombi zaidi ya 200 kutoka kwa makocha mbalimbali duniani ambao wameonyesha nia ya kuifundisha Taifa Stars.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002